

## **Unyambulishaji wa Vitenzi Katika Kigĩchūgũ**

**Magdalene Wangu Gituru**

**Tasnifu hii imewasilishwa katika Shule ya Mafuzu ili kutosheleza baadhi ya  
Mahitaji ya Shahada ya Uzamili ya Kiswahili**

**CHUO KIKUU CHA CHUKA  
SEPTEMBER, 2019**

## UNGAMO NA IDHINI

### Ungamo

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa madhumuni ya shahada katika Chuo Kikuu chochote.

Sahihi

Tarehe

10/09/2019

Magdalene Wangu Gituru  
AM12/19165/15

### Idhini

Tasnifu hii imetahiniwa, ikapitishwa na kuwasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa Chuo Kikuu.

Sahihi

Tarehe

10/09/2019

Prof. John M. Kobia  
Idara ya Fani  
Chuo Kikuu cha Chuka

Sahihi

Tarehe

10/09/2019

Dkt. Allan Mugambi  
Idara ya Fani  
Chuo Kikuu cha Chuka

## **HATILINZI**

Haki zote zimehifadhiwa na hairuhusiwi kunakili, kurudufisha, kuhifadhi kwa mifumo ya kieletroniki au kutoa vipengele fulani kwa namna yejete ile bila idhini ya mwandishi na Chuo Kikuu cha Chuka.

## **TABARUKU**

Utafiti huu natabarukia familia yangu akiwemo mwanangu mpendwa Stacey Nyawira, wazazi wangu Kellen Wawira na John Gituru kwa malezi yao mema na elimu waliyoniwesha kupata.

## **SHUKRANI**

Namshukuru Maulana kwa kunijalia uwezo na hekima katika vitengo vyote vya masomo. Pili, natoa shukrani za dhati kwa wasimamizi wangu Prof. John M. Kobia na Dkt. Allan Mugambi kwa ushauri wenu murua amba o mwekuwa mwangaza wangu katika kukamilisha utafiti huu. Kila wakati mlipoongea nami mlinitia shime na hamu ya kuendelea na safari iliyodhahirika kwangu kuwa ngumu. Asanteni sana. Aidha, ningependa kumshukuru Prof. John M. Kobia kwa kunifaa kwa vitabu na makala ya kitaaluma yaliyonisaidia sana katika utafiti huu.

Nawashukuru wahadhire wangu katika kozi zote kwa jumla amba waliniwezesha na kunitia shime ya kuendelea na kazi hii. Hao ni Dkt. Allan Mugambi, Bw. Enock Matundura, Bw. Kimathi Muembu, Bw. Mutahi Miricho na Bw. Sebastian Mbogo.

Siwezi kusahau kumshukuru mwanangu Stacey Nyawira kwa subira na uvumilivu wake hasa nilipokuwa nikishughulikia kazi hii. Ndugu zangu amba ni Alice, Titus na Peter pia nawashukuru kwa kunipa moyo wa kutia bidii licha ya changamoto nilizozipitia katika kazi hii. Shukrani zangu ziwaendee wazazi wangu Kellen Wawira na John Gituru kwa kunielimisha. Pia siwezi kuwasahau wanafunzi wenzangu; Mbungu, Hilda, Mbeere, Susan, Mwendwa, Mutegi, Faith, Mutwiri, Langat, Stella na Irene kwa majadiliano yenu yaliyonichochea kutia juhudhi. Aidha, shukrani kwa wote walioikosoa kazi hii kwa minajili ya kuiimarisha, Mungu awakirimu na hekima zaidi. Wote walionisaidia kwa njia moja au nyingine Mwenyezi Mungu awabariki. Mwisho, ningependa kutoa shukrani kwa Chuo Kikuu cha Chuka kwa ufadhili katika kazi hii.

## **IKISIRI**

Unyambulishaji wa vitenzi ni mojawapo ya masuala yanayoshughulikiwa katika taaluma ya mofolojia katika lugha nyingi za Kiafrika. Mofolojia ni tawi la isimu linaloshughulikia umbo la ndani la neno ambalo hujishughulisha na unyambulishaji wa vitenzi. Vitenzi ni maneno ambayo lazima yawepo katika sentensi ili ikamilike kimaana. Utafiti huu umeshughulikia unyambulishaji wa vitenzi vya Kigīchūgū kwa malengo ya kufafanua mifanyiko inayohusika katika utaratibu wa unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū na kutathmini kanuni zinazoruhusu au kuzuia mifanyiko hiyo ya unyambulishaji. Katika uainishaji wa Guthrie, Kigīchūgū ni mojawapo ya lugha za Kiafrika ambayo hudhihirisha unyambulishaji. Kigīchūgū kinawekwa katika kundi la E hasa katika E51 linalojumuisha lugha za Kibantu ambazo zimeimarika katika mofolojia ya uundaji na unyambulishaji wa vitenzi. Utafiti huu uliongozwa na mihimili ya nadharia ya Mofolojia Leksia iliyoasisiwa na Kiparsky na kuendelezwa na Katamba na Stonham, yaani mihimili ya Ngazi Leksia, Kufuta Mabano, Kuhifadhi Muundo, Kwingineko na Mzunguko Sheria. Nadharia ya Mofolojia Leksia ni nadharia zalishi na nyambulishi. Nadharia ya Mofolojia Leksia huonyesha uhusiano wa sheria zinazojenga maumbo ya kimofolojia na sheria zinazodhibiti namna maumbo haya yanavyotamkwa. Kanuni ya Kioo kwa mujibu wa Baker pia iliongoza utafiti huu kwani inaeleza kuwa unyambulishaji wa vitenzi katika lugha za Kibantu hufuata mpangilio maalum wa unyambulishaji. Data ya sampuli ya vitenzi vya Kigīchūgū ilitumika katika utafiti ambapo mtarifiti alizalisha kimaksudi vitenzi sitini (60) kutokana na sentensi za Kigīchūgū ambavyo vilitumika katika utafiti kwa kuwa ana uelewa na umilisi wa Kigīchūgū. Mtarifiti alienda nyanjani katika kata za Kabare, Baragwi, Karumandi, Ngariama na Njukini. Kata hizi zilichaguliwa kimaksudi kwani zina wazungumzaji halisi wa Kigīchūgū. Vitenzi hivi viliwekwa katika kauli sita za unyambulishaji na kuainisha mifanyiko inayohusika katika utaratibu wa unyambulishaji kwa kutumia jedwali la mnyambuliko wa vitenzi. Maana zinazowakilishwa na maumbo ya unyambulishaji pia zilijadiliwa. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa Kigīchūgū ni lugha ambishi kwani huchukua viambishi awali na tamati. Upachikaji wa viambishi tamati katika vitenzi vya Kigīchūgū ulichangia katika kuongeza maana za vitenzi. Matokeo ya utafiti pia yalionyesha kuwa Kigīchūgū hukubali mifuatano ya viambishi nyambulishi viwili, vitatu na hata vinne. Matokeo ya utafiti huu yatachangia katika kuongeza maarifa ya kiutafiti yanayohusu sarufi ya Kigīchūgū. Aidha, yatasaidia kuhifadhi Kigīchūgū kama mojawapo ya lugha za Kiafrika katika maandishi. Utafiti pia utachangia katika kuwanufaisha watafiti wa baadaye watakaoshughulikia Kigīchūgū.

## ABSTRACT

This research focuses on analysis of verb derivation in Kigīchūgū dialect with an objective of expounding on the processes involved in the process of verbal extensions in Kigīchūgū and defining the rules that allow or inhibit the processes. The findings of this study confirm clearly that this research was biased towards morphology since it focuses on the study of words, their internal structure and the changes they undergo when altered to form new words. The study majored on derivational morphology, especially verbal extensions, which are concerned with verb formation, involving the addition of affixes to the bases. This research was guided by the tenets of the Lexical Morphology Theory: The Strict Cycle Condition, Bracket Erasure Convection, Elsewhere Condition, Structure Preservation and Blocking. Lexical Morphology is a theory of rules and derivations. The study was also be guided by the Mirror Principle since it states that verb derivation in Bantu languages follow a linear order of affixes derived from a syntactic structure. The research adopted two methods of data collection mainly field research and also the researcher used her intuitive knowledge as a native speaker of Kigīchūgū to generate verbs in the Kigīchūgū which were later used for analysis. The data generated was complemented by going to the field to get Kigīchūgū sentences with verbs used by people within specific context. This research was conducted in Gichūgū Sub-County, Kirinyaga County, Kenya. The research covered five wards; Kabare, Baragwi, Karumandi, Njukini and Ngariama. These wards were purposively chosen because they are inhibited by native Kigīchūgū speakers. Guthrie classifies Kigīchūgū as part of zone E labelled E51 which belongs to the Bantu language and they are said to be rich in both inflectional and derivational morphology. Kigīchūgū has a rich derivational morphology just like the other Bantu languages. The data for the study was in form of sixty (60) verbs which the researcher generated. The data was analysed qualitatively and presented by; describing six affixes namely the applicative, the causative, the passive, the reciprocal, the reverive and the stative, giving examples of how they were realised and the possible combinations of the extensions. The findings of the research show that Kigīchūgū is an agglutinating language. The suffixes attached to the root of the verb help in changing the meaning of the host verbs. The research shows that Kigīchūgū verbal extensions can take three categories of co-occurrences namely: co-occurrences of two extensions, three extensions and four extensions. The rules that allow or inhibit these extensions were also explained in details. The findings of the study will contribute to the body of existing knowledge in Kigīchūgū language as well as contributing to further study by scholars.

## YALIYOMO

<b>UNGAMO NA IDHINI.....</b>	<b>ii</b>
<b>HATILINZI.....</b>	<b>iii</b>
<b>TABARUKU.....</b>	<b>iv</b>
<b>SHUKRANI.....</b>	<b>v</b>
<b>IKISIRI .....</b>	<b>vi</b>
<b>ABSTRACT.....</b>	<b>vii</b>
<b>YALIYOMO.....</b>	<b>viii</b>
<b>ORODHA YA MAJEDWALI .....</b>	<b>xi</b>
<b>ORODHA YA VIFUPISHO NA ALAMA.....</b>	<b>xii</b>

### **SURA YA KWANZA: UTANGULIZI .....1**

1.1 Usuli wa Mada .....	1
1.2 Suala la Utafiti.....	7
1.3 Malengo ya Utafiti .....	8
1.4 Maswali ya Utafiti.....	8
1.5 Umuhimu wa Utafiti.....	8
1.6 Upeo wa Utafiti .....	8
1.7 Maelezo ya Istilahi .....	10

### **SURA YA PILI: MWAUO WA MAANDISHI.....11**

2.1 Unyambulishaji wa Vitenzi katika Kiswahili.....	11
2.2 Unyambulishaji wa Vitenzi katika Lugha Nyingine za Kiafrika .....	14
2.3 Maandishi kuhusu Lugha ya Kikuyu .....	21
2.4 Maandishi kuhusu Kigīchūgū.....	23
2.5 Misingi ya Kinadharia.....	25
2.6 Hitimisho .....	31

### **SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI .....32**

3.1 Eneo la Utafiti .....	32
3.2 Mpango wa Utafiti .....	32
3.3 Walengwa wa Utafiti.....	32
3.4 Vifaa vya Utafiti.....	32
3.5 Utafiti wa Maktabani.....	33

3.6 Sampuli na Usampulishaji.....	33
3.7 Maadili ya Utafiti .....	34
3.8 Ukusanyaji wa Data .....	34
3.9 Uchanganuzi wa Data.....	35

**SURA YA NNE: MIFANYIKO YA UTARATIBU WA UNYAMBULISHAJI  
WA VITENZI KATIKA KIGICHŪGŪ .....36**

4.1 Utangulizi .....	36
4.2 Fonimu za Kigichūgū .....	36
4.2.1 Konsonanti za Kigichūgū .....	36
4.2.2 Irabu za Kigichūgū .....	38
4.3 Vitenzi vya Kigichūgū .....	41
4.4 Unyambulishaji wa Vitenzi vya Kigichūgū .....	42
4.4.1 Kauli ya Kutenda (TDA) .....	43
4.4.2 Kauli ya Kutendwa (TDW) .....	45
4.4.3 Kauli ya Kutendesha (TSH) .....	46
4.4.4 Kauli ya Kutendana (TDN) .....	47
4.4.5 Kauli ya Kutendeka (TDK) .....	47
4.4.6 Kauli ya Kutendua (TDU) .....	48
4.5 Mfuatano wa Viambishi Nyambulishi katika Kigichūgū.....	49
4.5.1 Mfuatano wa Viambishi Nyambulishi Viwili .....	50
4.5.2 Mfuatano wa Viambishi Nyambulishi Vitatu.....	59
4.5.3 Mfuatano wa Viambishi Nyambulishi Vinne .....	66
4.6 Kanuni za Mfuatano wa Viambishi Nyambulishi .....	68
4.6.1 Kanuni ya Kiambishi Nyambulishi {-w-} .....	68
4.6.2 Kanuni ya Viambishi Nyambulishi {-řr-} na {-er-} .....	68
4.6.3 Kanuni ya Viambishi Nyambulishi Radidi.....	69
4.6.4 Kanuni ya Kiambishi Nyambulishi {-an- } .....	70
4.7 Hitimisho.....	70

**SURA YA TANO: MAANA ZINAZOWAKILISHWA NA MAUMBO YA  
UNYAMBULISHAJI WA VITENZI KATIKA  
KIGICHUGU .....71**

5.1 Utangulizi .....	71
5.2 Kauli ya Kutenda.....	71

5.3 Kauli ya Kutendwa.....	73
5.4 Kauli ya Kutendesha .....	75
5.5 Kauli ya Kutendana.....	77
5.6 Kauli ya Kutendeka.....	78
5.7 Kauli ya Kutendua.....	80
5.8 Hitimisho.....	84
<b>SURA YA SITA: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>86</b>
6.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti.....	86
6.2 Hitimisho.....	88
6.3 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye.....	88
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>89</b>
<b>KIAMBATISHO I: TAKWIMU ZA TASNIFU .....</b>	<b>93</b>
<b>KIAMBATISHO II: JEDWALI LA USAILI WA VITENZI VYA KIGĪCHŪGŪ .....</b>	<b>94</b>
<b>KIAMBATISHO III: MNYAMBULIKO WA VITENZI VYA KIGĪCHŪGŪ ...</b>	<b>95</b>
<b>KIAMBATISHO IV: BARUA YA IDHINI YA UTAFITI .....</b>	<b>97</b>
<b>KIAMBATISHO V: KIBALI CHA UTAFITI.....</b>	<b>98</b>
<b>KIAMBATISHO VI: RAMANI YA KAUNTI YA KIRINYAGA IKIONYESHA ENEO LA UTAFITI.....</b>	<b>99</b>

## **ORODHA YA MAJEDWALI**

Jedwali 4.1: Konsonanti za Kigīchūgū .....	37
Jedwali 4.2: Utamkaji wa Konsonanti za Kigīchūgū.....	37
Jedwali 4.3: Irabu za Kigīchūgū .....	39
Jedwali 4.4: Utamkaji wa Irabu za Kigīchūgū.....	39

## ORODHA YA VIFUPISHO NA ALAMA

#:	Mipaka ya neno
/ /:	Mipaka ya fonimu
[ ]:	Mipaka ya foni
{ }:	Mipaka ya mofu
→:	Hubadilika kuwa
<b>I</b>	Kiishio
<b>Ka:</b>	Kiambishi awali
<b>Kt:</b>	Kiambishi tamati
<b>ktw:</b>	kitendwa
<b>K-V:</b>	Konsonanti-Vokali
<b>ML:</b>	Mofolojia leksia
<b>Nf:</b>	Nafsi
<b>Ng:</b>	Ngeli
<b>Nj:</b>	Njeo
<b>Nz:</b>	Nazali
<b>SZ:</b>	Sarufi zalishi
<b>T:</b>	Kitenzi
<b>TDA:</b>	Kauli ya kutendea
<b>TDK:</b>	Kauli ya kutendeka
<b>TDN:</b>	Kauli ya kutendana
<b>TDU:</b>	Kauli ya kutendua
<b>TDW:</b>	Kauli ya kutendwa
<b>TSH:</b>	Kauli ya kutendesha
<b>TUKI:</b>	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
<b>YE:</b>	Kiyeyusho


## **SURA YA KWANZA UTANGULIZI**

### **1.1 Usuli wa Mada**

Kwa mujibu wa Lyons (1968), mtaalamu Plato alibainisha waziwazi kategoria mbili kuu za maneno ambazo ni vitenzi na nomino. Kwa upande mwingine, Mgullu (1999) anasema kuwa maneno yanaweza kuainishwa katika makundi manane. Makundi hayo ni: Nomino, Vitenzi, Vivumishi, Viwakilishi, Vielezi, Vihuishi, Vihisishi na Viunganishi. Kategoria hizi ni muhimu kwani ni viungo muhimu katika sentensi za Kiswahili na za lugha zingine.

Wataalamu wengi wameshughulikia dhana ya vitenzi. Kwa mfano, Mgullu (1999), akirejelea dhana ya vitenzi anasema kuwa vitenzi ni aina ya maneno ambayo hutumika kama sehemu muhimu ya kiarifu cha sentensi na huarifu au hueleza jambo fulani linalohusu kiima cha sentensi. Kihore, Massamba na Msanjila (2012), wanaeleza kuwa kitenzi ni aina ya neno linalotoa taarifa juu ya tendo linalofanyika au linalotendwa na kiumbe au kitu. Kitenzi ni neno ambalo huarifu au hueleza kuhusu jambo linalozungumziwa katika sentensi. Ngowa (2008) anaeleza kwamba kitenzi ni aina ya neno ambalo hutumika kama kiarifu cha sentensi. Anasema kwamba kitenzi huarifu jambo linalofanywa na mtu, mnyama au kitu kingine chochote. Kauli hii imetiliwa mkazo na Munene (2011), ambaye anashikilia kuwa kitenzi hueleza juu ya tendo au hali. Kwa hivyo, kitenzi ni neno la lazima katika sentensi ili sentensi iweze kukamilika. Hii ina maana kwamba vitenzi ni maneno ya pekee ambayo ni lazima yawepo katika sentensi ili sentensi iweze kukamilika na kuelewaka. Kitenzi kikuu kikiondolewa katika sentensi basi sentensi hukosa maana kamili. Hii ina maana kwamba katika Kigīchūgū vitenzi ni vipashio vya lazima na haviwezi kudondoshwa katika mazingira yoyote yale.

Kwa mujibu wa Gawasike (2012), dhana ya uambikaji ambayo ina maana ya upachikaji wa mofu kabla na baada ya mzizi wa neno imegawika katika sehemu mbili; uambilishi na unyambulishaji. Anaeleza kuwa mgawanyo wake ni mzizi wa neno. Anatumia kielelezo kifuatacho kufafanua dhana ya uambikaji:



Kielelezo hiki kinaonyesha kuwa uambikaji ni dhana ya juu (kiambajengo cha juu) ikiundwa na viambajengo sisisi ambavyo ni uambishaji na unyambulishaji. Unyambulishaji ni mojawapo ya mifanyiko inayotokea katika kitenzi. Aidha Waihiga (1999) anafafanua kuwa unyambulishaji hutokana na vitenzi viwili ambavyo ni **nyambua** na **nyumbua**. Anaeleza **kunyambua** kama kukata kitu vipande vipande na **kunyumbua** kama kuvuta vitenzi ili kuvirefusha hivyo kuunda kauli mbalimbali za unyambulishaji. Kwa mujibu wa Kihore, Massamba na Msanjila (2012), unyambulishaji ni upachikaji wa viambishi kwenye mzizi ili kuunda maneno mapya. Wanaendelea kusema kuwa katika lugha ya Kiswahili kuna viambishi nyambulishi ambavyo hutumika katika uundaji wa vitenzi vipyta. Kihore, Massamba na Msanjila (keshatajwa) wanafafanua unyambulishaji wa vitenzi kama utaratibu wa uundaji wa vitenzi vipyta katika lugha kwa kuongeza viambishi nyambulishi kwenye maumbo ya mzizi. Utaratibu huu hufanyika katika hatua kama vile:

- a) Pig-w-a
- b) Pig-an-a
- c) Pig-i-a
- d) Pig-i-an-a
- e) Pig-i-w-a
- f) Pig-an-ish-a

(Asili: Kihore, Massamba na Msanjila, 2012: 122)

Kihore, Massamba na Msanjila (2012) wanaeleza kuwa hatua ya kwanza ni ile ya kiambishi kinachofuata mzizi moja kwa moja kama inavyodhihirika katika mifano a), b) na c); na hatua ya pili ni ya kiambishi nyambulishi cha pili kutoka kwenye mzizi kama inavyodhihirika katika mifano d), e) na f). Kihore, Massamba na Msanjila

(keshatajwa) waneleza kuwa kila umbo lililonyambuliwa lina maana tofauti japokuwa maana hiyo inafungamana na maana ya msingi inayodokezwa na mzizi. Kwa mfano;

- a. -w- Kiwakilishi cha tendo kumpata mpokeaji.
- b. -an- kiwakilishi cha tendo kuhusisha watu, vitu au mambo sawa.
- c. -i- kiwakilishi cha tendo linalopitia kuelekea lilipoelekezwa.
- d. -ish- kiwakilishi cha kusababisha tendo litendeke.

Munene (2011) anaeleza kuwa unyambulishaji ni hali ya kulipa neno maana nyingine kwa kuliongezea viambishi fulani. Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kwamba unyambulishaji wa vitenzi katika lugha ni suala lisiloepukika. Hivyo basi, utafiti huu ulishughulikia unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū ukiwa na lengo la kuonyesha mifanyiko mbalimbali ya unyambulishaji na maana zinazowakilishwa na mifanyiko hiyo.

Unyambulishaji wa vitenzi huchanganuliwa katika kiwango cha Isimu cha Mofolojia. Taaluma ya mofolojia inaweza kugawanya katika matawi makuu mawili; yaani mofolojia ya uundaji wa maneno na mofolojia ya unyambulishaji wa vitenzi (Katamba na Stonham, 1993). Aidha, Katamba na Stonham (keshatajwa) anaeleza kuwa mkondo wa kwanza hujishughulisha na uundaji wa maneno mapya ambayo ni leksimu, tofauti na maneno awali, aidha kwa kubadilisha maana kulingana na viambishi vilivyopachikwa au kwa kubadilisha kundi la neno huku mkondo wa pili ukishughulikia taratibu za kuongeza maana fulani za kisarufi katika maneno bila kuunda leksimu mpya.

Mgullu (1999) anasema kuwa mofolojia inapewa sura mbili: Mofolojia kama taaluma ya isimu ambayo ina jukumu la kuyachunguza maneno ili kuelewa maumbo yake yalivyo na mofolojia kama kiwango kimojawapo cha kila lugha. Mofolojia ya unyambulishaji wa maneno hushughulikia zaidi ile minyambuliko ya maneno ambayo huwekwa kwenye mizizi ya maneno kuwakilisha maana mbalimbali lakini unyambulishaji huo usibadili aina ya neno hilo (Mgullu, 1999). Mgullu (keshatajwa) anasema kuwa kila lugha inao utaratibu wake wa kunyambua maneno ya aina aina katika lugha hiyo. Kwa kurejelea maelezo ya Mgullu (keshatajwa), jamii mbalimbali za lugha huwa na taratibu bainishi za kunyambua vitenzi katika lugha husika.

Heine na Mohlig (1980) wanatilia mkazo kuwa lugha nyingi nchini Kenya zina utaratibu fulani wa unyambulishaji wa vitenzi. Wanasema kuwa nchini Kenya lugha zinaweza kugawika katika makundi mawili: Kundi la kwanza ni la lugha zilizopungukiwa katika mofolojia ya uundaji wa maneno ambazo wataalamu hawa wanasema kuwa huwa na kauli chache za unyambulishaji wa vitenzi. Kundi la pili ni la lugha zilizoimarika katika mofolojia ya uundaji wa maneno na ambazo huwa na kauli nyingi za unyambulishaji wa vitenzi. Baadhi ya kanuni za unyambulishaji wanazozitambua ni pamoja na kauli ya kutendwa, kutendesha, kutendea, kutendua, kutendana mionganoni mwa zingine.

Kigīchūgū ni mojawapo ya lugha za Kikuyu inayozungumzwa katika Kaunti ya Kirinyaga nchini Kenya. Kaunti hii hupakana na Kaunti ya Nyeri upande wa Kaskazini Magharibi, Kaunti ya Murang'a upande wa Magharibi na Kaunti ya Embu upande wa Mashariki na Kusini. Kaunti ya Kirinyaga imegawanywa katika Kaunti ndogo tano; Kirinyaga ya Mashariki, Kirinyaga Magharibi, Kirinyaga ya Kati, Mwea Mashariki na Mwea Magharibi. Kigīchūgū huzungumzwa na wakaazi ambao hupatikana katika Kaunti ndogo ya Kirinyaga Mashariki kama inavyodhahirika katika ramani katika kiambatisho V (Uk 92).

Kwa mujibu wa Mutahi (1983) Kigīchūgū ni mionganoni mwa lahaja za mashariki. Lahaja zingine ni kama vile, Kiembu, Kimbeere, na Kindia. Mutahi (keshatajwa) anasema kuwa wazungumzaji wa lahaja ya Kigīchūgū huwa kati ya mto Rupingazi na Thiba. Anasema kuwa Rupingazi huwatenga Wagichūgū na Waembu nao Thiba huwatenga na Kindia. Anaendelea kusema kuwa mpaka halisi kati ya Ndia na Gīchūgū ni mto Rutui. Kulingana na sensa za mwaka wa 2009, tarafa ya Gīchūgū ambayo ndiyo kitovu cha wazungumzaji halisi wa Kigīchūgū ilikuwa na wazungumzaji elfu mia moja ishirini na nne, mia sita sabini na mbili (124,672). Kulingana na Mipango ya Maendeleo ya Kaunti ya Kirinyaga mwaka wa 2018-2022, wazungumzaji wa Kigīchūgū mwaka wa 2019 wanakisiwa kuwa elfu mia moja arobaini na nne, mia nane arobaini na nane (144,848). Uainishaji wa Guthrie (1967) ulipangilia lugha ya Kikuyu katika kundi la E51. Kwa mujibu wa Nurse na Philippson (2003), lugha ya Kibantu ni kundi la lugha ambalo ni tawi la lugha za Niger-Kongo. Wanatambua kwamba jamii za Kibantu huishi Afrika. Katika maelezo yao,

wanatambua Kikuyu mionganoni mwa lugha za Kibantu. Wanaendelea kusema kuwa lugha za Kibantu zimeimariika sana katika mofolojia ya uundaji wa maneno na mofolojia ya unyambulishaji wa vitenzi.

Lugha ya Kikuyu ni mojawapo ya lahaja za Kibantu ambayo huzungumzwa na jamii ya Wakikuyu ambao, kulingana na sensa za mwaka wa 2009, wanakisiwa kuwa milioni saba wanaoishi nchini Kenya. Wataalamu ambao wameshughulikia lugha ya Kikuyu wanahitilafiana kuhusu idadi ya lahaja. Mionganoni mwa wataalamu hao ni kama vile Mutahi (1983) ambaye anatambua lahaja saba za lugha ya Kikuyu; lahaja za Kusini na lahaja za Kaskazini, Kindia, Kimathira, Kigīchūgū, Kiembu na Kimbeere. Kutokana na maelezo ya Mutahi (1983), Kigīchūgū ni mojawapo ya lahaja za lugha ya Kikuyu. Kamau (1996) anasema kuwa lugha ya Kikuyu ina lahaja tano: Kikabete, Kimurang'a, Kinyeri, Kigīchūgū na Kindia. Ruri (2011) anaunga mkono mawazo ya Kamau (keshatajwa) kwamba lugha ya Kikuyu ina lahaja tano. Kwa mujibu wa Ruri (keshatajwa), wazungumzaji wa lugha za Kindia na Kigīchūgū huchukuliwa kuwa si Wakikuyu halisi kwa kuwa lugha hizi hazijaandikiwa othografia. Ruri (keshatajwa) anatilia mkazo maoni ya Mutahi (keshatajwa) kuwa wazungumzaji wa lugha ambazo hazijaandikiwa othografia hujikaza kuzungumza lugha ilioandikiwa othografia ili kuthibitisha kwamba wao ni Wakikuyu halisi. Katika maelezo yake Ruri (keshatajwa), Wandia na Wagīchūgū ni baadhi ya walioathiriwa na hali anayoizungumzia Mutahi. Lugha inayozungumzwa na Wagīchūgū haitumii [h] na badala yake hutumia [b]. Sauti [h] hupatikana katika lugha zingine za Kikuyu. Sauti [k] pia hutumiwa katika lugha ya Kigīchūgū ikilinganishwa na lugha zingine ambazo hutumia sauti [g]. Kwa mfano:

<b>Kigīchūgū</b>	<b>Kimurang'a</b>	<b>Kiswahili</b>
<u>k</u> ūthambia	guthambia	kusafisha
<u>k</u> ūthaka	guthaka	kucheza
<u>k</u> ūbūra	ku <u>h</u> ura	kuchapa

(Asili: Ruri, 2011: 6)

Kutokana na maelezo ya wataalamu kama vile Mutahi (1983), Kamau (1996) na Ruri (2011), tunaweza kusema kwamba Kigīchūgū ni lugha mojawapo ya lugha za Kiafrika. Hii ni kwa sababu Kigīchūgū kinao wazungumzaji asilia, kina sauti za irabu

na konsonanti ambazo hutumiwa katika mazungumzo na vilevile kina eneo la kijiografia ambapo hutumiwa kuendesha shughuli mbalimbali.

Vitenzi vya Kigīchūgū hubainisha dhahiri kwamba Kigīchūgū ni lugha ya Kibantu hivi kwamba vitenzi vingi huishia kwa irabu {a} kama ilivyo katika vitenzi vingine vya Kibantu (Katamba na Stonham, 1993). Kwa mfano katika lugha ya Kigīchūgū;

<b>Mzizi</b>	<b>Kiishio</b>	<b>Kitenzi</b>	<b>Maana</b>
/meny/	/a/	menya	jua
/in/	/a/	ina	imba
/rīm/	/a/	rīma	lima
/būr/	/a/	būra	chapa

Kigīchūgū vilevile ni lugha tonishi. Toni katika maneno ya Kigīchūgū huleta mabadiliko katika maana. Kwa mfano maneno # ūria# (maziwa, ziwa), #kūrīa# (kiashiria cha mahali, kitenzi) yanaweza kuwa na maana mbili kutegemea toni.

Schadeberg (2003) anaeleza kuwa vitenzi vya Kibantu vina uwezo mkubwa wa mzizi kubeba viambishi aidha vya nafsi, njeo, urejeshi na hata viambishi vya unyambulishaji. Kutokana na maelezo yake Schadeberg (keshatajwa), kitenzi cha Kigīchūgū kina uwezo mkubwa wa kubeba viambishi kuliko aina zingine za maneno katika lugha hii. Kama ilivyo katika Kiswahili, vitenzi vya Kigīchūgū huchukua viambishi awali na viambishi tamati hivyo basi utafiti huu ulishughulikia viambishi tamati kwani ndivyo hupachikwa baada ya mzizi wa vitenzi katika mfanyiko wa unyambulishaji.

Kwa mujibu wa Mgullu (1999), kiambishi ni istilahi ambayo hutumiwa hasa katika uwanja wa mofolojia kueleza sehemu mbalimbali za maneno ambazo huongezewa katika mizizi ya maneno. Massamba, Kihore na Msanjila (2012) wanasema kuwa viambishi ni mofimu zinazoambatanishwa kwenye mzizi wa neno ili kuwakilisha hali au dhana mbalimbali zinazofungamana na neno pamoja na mofimu hizo. Kwa mfano;

- a. Pote-*le-a*
- b. Pig-*an-ish-w-a*
- c. Pat-*an-ish-w-a*

(Asili: Massamba, Kihore na Msanjila 2012: 54)

Katika mifano hii, wataalamu hawa wanatambua vipashio viliivoandikwa kwa herufi za mlazo kama viambishi ambavyo vimeambikwa baada ya mzizi ili kuleta dhana ya unyambulishaji. Hali hii hudhihirika katika lugha ya Kigīchūgū ambapo viambishi tamati huweza kuambikwa baada ya mzizi. Kwa mfano;

kw+end+wa→pendwa

kw+end+a+na→pendana

kū+būr+ith+i+a→pigisha

Katika mifano hii, {kū}, {wa}, {na}, {ith} na {i}, ni viambishi ambavyo vimeongezewa kwenye mzizi wa neno. Hartman (1972) anafafanua mzizi kama mofimu fulani katika neno ambayo huwakilisha taarifa ya kileksia iliyo muhimu zaidi katika neno hilo. Kwa mujibu wa TUKI (1990: 50), mzizi ni sehemu ya neno ambayo haibadilikibadiliki. Kwa mfano, -chez- ni mzizi katika maneno chezana, chezwa, chezeka, chezesha na kadhalika. Kwa hivyo utafiti huu umejikita katika unyambulishaji wa vitenzi vya Kigīchūgū kwa kutilia maanani mtazamo wa mofolojia leksia.

## 1.2 Suala la Utafiti

Unyambulishaji wa vitenzi ni suala muhimu linaloshughulikiwa katika mofolojia. Tafiti mbalimbali ambazo zimefanywa kuhusu unyambulishaji wa vitenzi zimeshughulikia mfumo wa vitenzi kwa jumla. Ingawa tafiti hizi zimejikita katika lugha moja maalum, hazijatathmini kanuni zinazoruhusu au kuzuia mifanyiko ya unyambulishaji wa vitenzi. Kadri mtafiti ajuavyo, lahaja ya Kigīchūgū ni lugha ya Kibantu na hukubali unyambulishaji wa vitenzi. Hii ni kwa sababu, lahaja ya Kigīchūgū ni mfano wa lugha ambishi. Baadhi ya viambishi vinavyopatikana katika lahaja hii ni vya unyambulishaji. Viambishi hivyo ndivyo huongeza maana katika vitenzi vya Kigīchūgū. Kulingana na ujuzi wa mtafiti, hakuna utafiti ambao

umefanywa kuhusiana na unyambulishaji wa vitenzi vya Kigīchūgū. Hivyo basi, utafiti huu ulinuia kufafanua mifanyiko iliyohusika katika utaratibu wa unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū.

### **1.3 Malengo ya Utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo:

- i. Kufafanua mifanyiko na mfuatano wa maumbo yanayohusika katika utaratibu wa unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū.
- ii. Kujadili maana zinazowakilishwa na maumbo ya unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū.

### **1.4 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu ulinuia kujibu maswali ya utafiti yafuatayo:

- i. Ni mifanyiko na maumbo gani yanayodhihirika katika unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū?
- ii. Ni maana zipi ambazo huwakilishwa na maumbo ya unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū?

### **1.5 Umuhimu wa Utafiti**

Kwa kutathmini unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū, utafiti huu utachangia katika kuongeza maarifa ya kiutafiti yanayohusu sarufi ya Kigīchūgū. Utafiti huu pia utawasaidia wanaisimu kujua na kuelewa jinsi unyambulishaji wa vitenzi unavyojitokeza katika lugha ya Kigīchūgū. Pia, utafiti huu utawafaa wanafunzi wa ngazi mbalimbali za kielimu katika Kiswahili na lugha nyinginezo za Kiafrika kufahamu namna mnyambuliko hubadili kitenzi na maana yake. Vilevile utafiti huu utawanufaisha wanaleksikografie ambao wanahusika na uundaji wa kamusi za lugha za Kibantu hasa Kigīchūgū kwa kuonyesha jinsi kauli mbalimbali hunyambuliwa katika Kigīchūgū.

### **1.6 Upeo wa Utafiti**

Utafiti huu ulijikita katika mofolojia ya maneno hasa mofolojia ya unyambulishaji wa vitenzi vya Kigīchūgū. Katika utafiti huu, tulifafanua jinsi pana uhusiano wa mofolojia na fonolojia katika maumbo mbalimbali ya vitenzi. Hata hivyo, viwango

vingine vya lugha kama semantiki vimehusishwa pale ambapo mchango wake umesaidia kufikia malengo ya utafiti huu. Utafiti ulijadili unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū katika kauli za kutendea, kutendeka, kutendwa, kutendana, kutendua na kutendesha. Kauli hizi zilichaguliwa kwani ni kauli za kimsingi katika Kigīchūgū na ndizo zina uwezo wa kukubali mifanyiko iliyoshughulikiwa katika utafiti huu. Hata hivyo, lugha ya Kiswahili ina kauli ya kutendama na kutendata ambazo hazikushughulikiwa katika utafiti huu kwani hazipatikani katika Kigīchūgū na hazina wingi wa vigezo vya kimofolojia. Utafiti huu pia umebainisha jinsi viambishi tamati upachikwa katika mzizi wa vitenzi vya Kigīchūgū ili kuleta dhana ya unyambulishaji na kauli tofauti. Vitenzi vilivyotumiwa katika utafiti huu ni vitenzi vikuu kwa sababu vinaweza kunyambuliwa katika kauli mbalimbali za unyambulishaji wa vitenzi vya Kigīchūgū. Data ya utafiti huu ilipatikana kutoka maeneo ya Kabare, Baragwi, Njukiini, Ngariama na Karumandi. Haya ni maeneo ambayo yana wazungumzaji asilia wa Kigīchūgū.

## **1.7 Maelezo ya Istilahi**

Katika utafiti huu, istilahi zifuatazo zilitumiwa kumaanisha:

- Fonimu:** Kundi la sauti katika Kigīchūgū na huwakilishwa kwa / / .  
Kwa mfano sauti /a/.
- Fonolojia:** Tawi la isimu ambalo hushughulikia uchambuzi wa mfumo wa sauti zinazotumiwa katika Kigīchūgū.
- Kigīchūgū:** Hii ni mojawapo ya lugha za Kibantu inayozungumzwa na Wakikuyu kutoka Kaunti ya Kirinyaga.
- Kitenzi:** Neno ambalo hueleza juu ya tendo au hali katika Kigīchūgū.
- Mifanyiko:** Taratibu zinazofuatwa katika unyambulishaji wa vitenzi vyta Kigīchūgū.
- Mofimu:** Sehemu ndogo ya tamko iletayo maana kamili kisarufi katika Kigīchūgū.
- Mofolojia:** Tawi la isimu linaloshughulikia muundo na uamilifu wa maneno katika Kigīchūgū. Katika utafiti huu tutashughulikia mofolojia ya Kigīchūgū.
- Mofu:** Umbo la neno ambalo huwakilisha mofimu na ambalo hudhihirika kifonolojia na kiothografia katika Kigīchūgū.
- Mzizi:** Umbo la msingi la vitenzi vyta Kigīchūgū ambalo halina kiambishi chochote na halibadilikibadiliki.
- Silabi:** Kipashio cha kifonolojia ambacho hufuma mwambatano wa fonimu unaojumuisha, kwa kawaida, sauti ya vokali katika Kigīchūgū.
- Uambikaji:** Upachikaji wa mofu kabla na baada ya mzizi wa vitenzi vyta Kigīchūgū.
- Uambishaji:** Upachikaji wa viambishi awali kwenye mzizi wa vitenzi ili kuunda maneno mapya.
- Unyambulishaji:** Upachikaji wa viambishi tamati kwenye mzizi wa vitenzi ili kuunda maneno mapya ya Kigīchūgū. Ni hali ya kuvipa vitenzi vyta Kigīchūgū maana nyingine kwa kuviongezea viambishi tamati.

## **SURA YA PILI**

### **MWAUO WA MAANDISHI**

#### **2.1 Unyambulishaji wa Vitenzi katika Kiswahili**

Mgullu (1999) anasema kwamba unyambulishaji wa maneno hushughulikia zaidi ile minyambuliko ya maneno ambayo huwekwa kwenye mizizi ya maneno kuwakilisha maana mbalimbali lakini unyambulishaji huo usibadili aina ya neno hilo. Anaendelea kusema kuwa katika lugha ya Kiswahili, mzizi wa neno ni mofimu ambayo ni sehemu muhimu zaidi ya neno na ambayo katika lugha nyingi inaweza kukaa peke yake kama neno kamili. Mizizi inaweza kuwekwa pamoja na kuunda neno. Mgullu (keshatajwa) anasema kwamba unyambulishaji vitenzi aghalabu huwa na uamilifu wa kisarufi na neno ambalo hupatikana baada ya minyambuliko huwa haliwezi kuwa leksimu au kuonekana kuwa ni neno tofauti na lile neno la awali. Alishughulikia kauli kadha za unyambulishaji miongoni mwazo: Kauli ya kutenda, kutendwa, kutendewa, kutendeka, kutendesha, kutendea, kutendana, kauli dumishi na kauli ya kutendua. Maelezo ya Mgullu (keshatajwa) yalifaa utafiti huu kwa kuwa yalitoa utaratibu wa unyambulishaji wa vitenzi ambao ulitumika kwa kuongoza unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū. Tofauti ya kazi ya Mgullu (keshatajwa) na kazi hii ni kwamba maelezo yake hayakuhusisha nadharia katika uchanganuzi wake lakini utafiti wetu umeongozwa na nadharia ya Mofolojia leksia.

Unyambulishaji usio na mipaka na unyambulishaji wenyewe mipaka umeelezwa na Khamisi (2008). Akimnukuu Guthrie (1962:203), Khamisi (2008) anasema kuwa unyambulishaji wenyewe mipaka huathiri tabia ya kitenzi kisintaksia kwa kuongeza yambwa, kupunguza yambwa au kutofanya chochote kile kwenye kitenzi. Anaendelea kuzungumzia aina za minyambuliko kama fanyizi, mufidi, ambatani, nafsi, tendwa, uwezo, tuamo na nyume ambayo hupelekea kitenzi kuteua kategoria za maneno. Maelezo ya Khamisi (keshatajwa) yametoa mwongozo katika kazi hii kwani umeshugulikia unyambulishaji ambao ndiyo dhana tuliyoshughulikia. Hata hivyo, utafiti huu ulijikita kwenye unyambulishaji wa vitenzi vya Kigīchūgū ili kubaini athari yake kisemantiki ikilinganishwa na utafiti wa Khamisi (2008) uliojadili jinsi unyambulishaji huathiri kitenzi kisintaksia katika lugha ya Kiswahili.

Akishughulikia vinyambuo vitenzi vya Kiswahili, Kiango (2008) anasema kwamba, michakato yote ya unyambulishaji inatawaliwa na kanuni za kifonolojia na

kimofolojia. Alizungumzia kanuni za unyambulishaji vitenzi kwa nia ya kuonyesha ubora na udhaifu katika kanuni hizo. Anaendelea kusema kuwa kanuni au michakato ya unyambulishaji vitenzi ambazo zinatumwiwa katika mizizi au mashina ya vitenzi zinazalisha aina mbalimbali za unyambuaji tenzi. Baadhi ya aina hizo ni kama vile unyambuzi-tendea, unyambuzi-tendana, unyambuzi-hali, unyambuzi-tendeshana unyambuzi-tendwa. Maelezo ya Kiango (keshatajwa) yalifaa utafiti huu kwani yamefanua kanuni za kuzalisha vinyambuo-tenzi ambazo ndizo zilitumika katika uanishaji wa unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū.

Katika utafiti wake, Gichuru (2010) alichanganua nomino ambatani za Kiswahili kwa madhumuni ya kuainisha taratibu pamoja na kanuni zinazohusika katika uundaji wa maumbo hayo. Katika utafiti wake, mihimili ya mofolojia leksia ilimwongoza. Utafiti wake Gichuru (keshatajwa) ulifaidi utafiti huu kwani tafiti zote zimejikita kwenye taaluma ya mofolojia ingawa yeye aliegemea katika tawi la mofolojia ya uundaji wa maneno na utafiti huu ulijikita katika tawi la mofolojia ya unyambulishaji wa vitenzi.

Akishughulikia njia mbalimbali zinazotumika katika lugha ya Kiswahili kuunda msamati wake, Kawasike (2012) anafafanua njia mbili ambazo ni pamoja na uambishaji na unyambulishaji. Anafafanua dhana hizi na kutumia dhana ya uambikaji kwa kujadili uhusiano uliopo baina ya uambishaji na unyambulishaji. Anaendelea kusema kuwa uambikaji ni upachikaji wa mofu kabla na baada ya mzizi wa neno. Aidha anasema kuwa uambikaji ni dhana ya juu ambayo imegawanyika katika sehemu mbili; uambishaji na unyambulishaji. Anasema kuwa msingi wa mgawanyo wake ni mzizi wa neno. Katika makala yake analenga kupendekeza matumizi ya uambikaji ili kutanzua utata ambao umekuwepo katika dhana za uambishaji na unyambulishaji. Utafiti wake Kawasike (keshatajwa) umefaidi utafiti huu kwani amelishughulikia suala la uambikaji katika vitenzi ambapo anagundua kwamba ni upachikaji wa mofu baada ya mzizi, na utafiti huu pia unahusu uambikaji wa viambishi katika mizizi ya vitenzi.

Katika makala yake Mwita (2014), alishughulikia dhima ya kiambishi cha kauli ya kutenda ya kitensi cha Kiswahili. Katika kazi yake aliongozwa na kauli ‘najivunia kuwa Mkenya’ iliyojibowi kwa kauli ‘Navumilia kuwa Mkenya,’ iliyokusudiwa

kuzusha hisia za kizalendo. Mwita (keshatajwa) alilenga kuchunguza usarufi au utosarufi wa matumizi ya vitenzi #**najivunia** # na #**navumilia**# kwa mtazamo elezi na mtazamo elekezi. Katika makala yake, Mwita (keshatajwa), alitambua kuwa kitendi cha Kiswahili kina maumbo mbalimbali ya kauli ya kutendea. Maumbo haya ni kama vile {i} ambalo hutumika kwenye vitenzi vyenye irabu /a/, /i/ au /u/ kwenye mzizi, umbo{e} ambalo hutumika kwenye vitenzi vyenye irabu /e/ na /o/ kwenye mzizi, umbo {li} ambalo kama {i} hutumika kwenye vitenzi vyenye mzizi unaoishia kwa irabu /a/, /i/ na /u/ na umbo {le} ambalo hutumika kwenye vitenzi vyenye mzizi unaoishia kwa irabu /e/ na /o/. Makala ya Mwita (keshatajwa) vilevile ilizingatia dhima mbalimbali za kauli ya kutendea katika lugha ya Kiswahili. Kazi yake Mwita (2014), ni tofauti na utafiti huu kwani alijikita tu kwenye kauli ya kutendea hasa kwa kushughulikia vitenzi viwili; Najivunia na Navumilia ilhali utafiti huu ulizingatia kanuni sita za unyambulishajina kuangazia vitenzi vifikapo sitini (60). Kazi yake Mwita (keshatajwa) ilifaa utafiti huu kwani ilitoa mwongozo zaidi kuhusiana na kauli ya kutendea ambayo ni mojawapo ya kauli zilizoshughulikiwa katika utafiti.

Mbwillow (2017), akifafanua tofauti kati ya uambishaji na unyambulishaji katika Kiswahili, anaeleza kuwa maneno ya lugha asilia ya binadamu huundwa kwa njia mbalimbali. Anaeleza njia kama vile, uradidi, kubuni, uambatanishaji na uambatizi kwa maana ya uambishaji na unyambulishaji. Anaeleza kuwa uambikaji ni kitendo cha upachikaji au uongezaji wa mofu au viambishi kabla au baada ya mzizi wa neno, kiini au shina la neno. Anasisitiza kuwa njia kuu ya uundaji wa maneno iwe ni uambikaji kisha uambishaji na unyambulishaji ziwe ni aina ya uambikaji na tofauti yake kuu iwe ni pahala pa upachikaji. Anafafanua unyambulishaji kama mchakato wa upachikaji wa mofu/viambishi baada ya mzizi wa neno na shina. Katika kazi yake, anaeleza kuwa uambishaji na unyambulishaji huunda maneno mapya. Anaeleza kuwa uambishaji na unyambulishaji zote zaweza kutobadili kategoria ya neno bali zikatanua maana ya neno husika. Mbwillow (keshatajwa) anaeleza kuwa unyambulishaji hudokeza kauli mbalimbali. Anafafanua kauli ya kutenda, kutendewa, kutendeka na kutendeana. Anatoa mfano wa neno # lima# na kufafanua kama ifuatavyo;

- lim-i-a (kauli ya kutendea)
- lim-w-a (kauli ya kutendwa)
- lim-ik-a (kauli ya kutendeka)
- lim-i-an-a (kauli ya kutendeana)

Mbwillow (keshatajwa) anaeleza kuwa si kila neno au kategoria ya maneno ya Kiswahili ambapo uambishaji na unyambulishaji hutokea. Anasema kuwa ni rahisi kuambisha katika vitenzi vyote vya Kiswahili. Kazi ya Mbwillow (keshatajwa) ilifaa utafiti huu kwani alishughulikia suala la unyambulishaji dhana ambayo pia ilishughulikiwa katika utafiti huu. Hata hivyo, tofauti ya kazi yake na utafiti huu ni kuwa kazi yake ilihusu dhana ya uambikaji kama dhana kuu ilhali utafiti huu ulihusu mifanyiko na mifuatano ya maumbo ya unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū.

## **2.2 Unyambulishaji wa Vitenzi katika Lugha Nyingine za Kiafrika**

Watafiti wengi wameshughulikia suala la unyambulishaji wa vitenzi katika lugha mbalimbali. Maringah (1987) alichunguza muundo wa kitenzi cha Kimbeere. Aliainisha vipashio mbalimbali vya kitenzi cha Kimbeere kama vile; nyakati, ngeli, mnyambuliko na virejeshi. Utafiti wake ulifaa utafiti huu kwani alishughulikia muundo wa kitenzi cha lugha ya Kibantu kama ilivyoshughulikiwa katika Kigīchūgū. Vilevile, utafiti wake ulijikita katika vitenzi aina ya maneno ambayo pia inashughulikiwa katika kazi hii. Kwa hivyo, kazi yake ilisaidia kuongeza ufahamu wa lugha za Kibantu na pia kutoa mwongozo kuhusu unyambulishaji wa vitenzi. Tofauti kati ya utafiti wa Maringah (keshatajwa) na huu ni kuwa, utafiti huu umeshughulikia viambishi tamati tu katika vitenzi ilhali utafiti wake ulishughulikia pia viambishi awali na tamati. Pili, utafiti huu umeshughulikia mifanyiko na maumbo yanayohusika katika unyambulishaji pamoja na maana zinazowakilishwa na maumbo hayo kinyume na utafiti wake ulioshughulikia muundo tu.

Akishughulikia Kirai Tenzi cha Kiswahili na Ekegusii kimofosintaksia, Oichoe (2005) alifafanua jinsi muundo na upatanishi wa kisarufi unavyojitokeza katika Kirai Tenzi kwa kutumia nadharia ya Uminimalisti. Katika kazi yake Oichoe (keshatajwa) amelinganisha vipashio vya Kirai Tenzi kimuundo katika lugha hizi mbili kama vile vipashio kama Nomino, Vielezi, Viwakilishi huku akiangalia uhusiano wa kitenzi na vipashio hivyo. Alibaini kwamba vitenzi vya Kiswahili sanifu na Ekegusii huchukua viambishi tamati. Alibainisha kuwa viambishi vinyambuzi vinachukua nafasi sawa katika vitenzi katika lugha hizi. Hata hivyo, anasema tofauti kuu katika unyambulishaji kati ya Kiswahili na Ekegusii ni kwamba lugha ya Kiswahili ina viambishi vingi na alomofu nyingi zinazosimamia baadhi ya kauli zake. Kazi yake

imefaa utafiti huu kwani aligusia unyambulishaji wa vitenzi kwa kuzingatia kauli kama vile, kutendea, kutendesha, kutendwa, kutendana mionganii mwa zingine hivyo basi kutoa mwanga katika utafiti huu. Tofauti ya utafiti wa Oichoe (keshatajwa) na huu ni kuwa utafiti wake ni wa kimofosintaksia kwa lengo la kukagua sifa za Kirai Tenzi na huu ni wa kimofofonolojia kwani umeshughulika na mifanyiko mbalimbali ya vitenzi vya Kigīchūgū. Vilevile utafiti wake uliongozwa na nadharia ya Uminimalisti kinyume na huu ulioongozwa na Nadharia ya Mofolojia Leksia na Kanuni ya Kioo.

Unyambulishaji wa vitenzi ya Kigryama umeshughulikiwa na Ngowa (2008) huku akionyesha jinsi Kigryama ni lugha ya Kibantu kwa kurejelea dhana ya kitensi. Katika utafiti wake, anatumia mtazamo wa fonolojia leksishi ambaa ni mtazamo wa fonolojia zalishi. Mtazamo huu unatambua kuwa uambishaji wa maneno unaandamana na mageuzi au sheria za kifonolojia za kiwango kimoja. Katika utafiti wake anashughulikia muundo wa ndani wa kitensi akiégemea pia katika eneo la mofolojia. Anatambua kwamba kitensi cha Kigryama kina uwezo mkubwa wa kubeba viambishi kuliko aina zingine za maneno. Amezingatia kikamilifu jinsi kanuni za fonolojia leksishi zimetumiwa ili kuongoza unyambulishaji wa vitenzi. Ametambua kanuni hizi kama vile ngazi leksia, mzunguko wa sheria, kuhifadhi muundo, kufuta mabano na ufinyu wa sifa. Kazi yake Ngowa (keshatajwa) inatoa mawazo muhimu katika utafiti huu kwa vile ambavyo amezingatia unyambulishaji wa vitenzi katika lugha za kibantu. Tofauti ni kuwa utafiti wake unajihuisha na kufafanua kanuni na sheria zinazodhibiti mageuzi ya vitenzi pekee lakini utafiti huu ulifafanua mifanyiko pamoja na maana zinazowakilishwa na mifanyiko mbalimbali ya unyambulishaji.

Akishughulikia unyambulishaji wa vitenzi katika lugha ya Runyankole, Asiimwe (2011) alijadili mofimu za Utendea, Usababishi, Utendeka na Utendwa. Alibainisha kuwa unyambulishaji wa vitenzi katika Runyankole, mojawapo ya lugha za Kiafrika, unahuisha mizizi ya vitenzi ambapo mofimu nyambulishi hupachikwa. Anatambua kwamba mofimu nyambulishi za usababishi hupokezwa kitensi kwanza kabla ya utendwa. Anaeleza kuwa usababishi huunda kitensi elekezi kutokana na kile ambacho sielekezi kwa sababu vitenzi elekezi tu ndivyo vinaweza kupokea utendwa. Utafiti wa Asiimwe (keshatajwa) ulifaa utafiti huu kwani watoa kielelezo katika mifanyiko

inayohusika katika unyambulishaji wa vitenzi. Hata hivyo, uafiti wake unatofautiana na huu kwani wake unahu su kauli tano za unyambulishaji wa vitenzi na huu unahu su kauli sita. Utafiti wa Asiiimwe (keshatajwa) uliongozwa na nadharia mbili; Kiolezo na kanuni ya Kioo kinyume na utafiti wetu unaoongozwa na Nadharia ya Mofolojia Leksia na pia Kanuni ya Kioo.

Kwa upande mwingine, Munene (2011) alishughulikia kitensi cha Kichuka ili kudhihirisha iwapo kinasheheni mofimu za kisarufi katika umbo lake. Anasema kuwa kitensi cha Kichuka kina mofimu kama vile za ubainishi, njeo, yambwa, mzizi, unyambulishaji, mofu-jenzi na viishio vingine ambavyo hujitokeza kama viambishi awali na viambishi tamati. Anasema kuwa vitenzi vya Kichuka vina hali ya kunyambuka, yaani vinaweza kutengeka katika sehemu zake ili kupata shina au mzizi wa neno ambao unaweza kunyambuka kwa njia ya kuambishwa viambishi vya mnyambuliko na kuibua maneno yenyе maana mbalimbali. Alitumia kitensi cha Kichuka #makuringana# (wamepigana) kutuonyesha jinsi vitenzi vya Kichuka hupendelea sana kutumia mnyambuliko ama urefushaji wa maneno kwa kutumia viambishi kuonyesha uhusiano wa kisarufi kati ya neno na maana zake. Anakitenga kitensi hiki katika mofu mbalimbali kama:

/ma-ku-ring-an-a/

{ma}-mofu ya mtenda nafsi ya tatu

{ku}-mofu ya kuainisha njeo ya wakati uliopita muda mrefu

{-ring-}-mzizi wa neno ulio na maana ya kitensi

{-an-}- mnyambuliko (hali ya kutendana)

{a}-kiishio cha kitensi.

(Asili: Munene 2011: 44)

Ufafanuzi wa Munene (keshatajwa) unadhihirisha kwamba mofu {-an-} katika viambishi vinavyotokea baada ya mzizi ni kiambishi cha mnyambuliko. Anasema kuwa kitensi cha Kichuka kinaweza kuambishwa viambishi awali ambapo viambishi hivyo hubeba maana za kisarufi. Utafiti wake Munene (keshatajwa) umetoa mwelekeo bora wa utafiti huu. Maelezo yake yamesaidia zaidi utafiti kwa jinsi ambavyo yametoa utaratibu wa miundo ya vitenzi vya Kichuka ambavyo vitatumika kwa kuongoza mnyambuliko wa vitenzi vya Kigīchūgū. Kinyume na utafiti wa

Munene (keshatajwa), ulioongozwa na mihimili ya Nadharia ya Sarufi Zalishi Geuza Umbo, utafiti huu uliongozwa na mihimili ya Nadharia ya Mofolojia Leksia.

Katika kazi yake, Charwi (2013) alishughulikia unyambulishaji wa vitenzi katika Kikuria akiwa na lengo la kueleza matokeo ya vitenzi vya Kikuria baada ya unyambulishaji na idadi ya viambishi vinavyoweza kuwekwa pamoja kwenye kitenzi. Katika kazi yake, alichanganua unyambulishaji wa vitenzi ili kuonyesha dhana ya uelekezi unavyojitokeza na kuonyesha upekee na ufanano wa lugha ya Kikuria na lugha nyingine za Kibantu kama vile, Kinyambo, Kinyamwezi, Kibosho miongoni mwa lugha zingine. Utafiti wa Charwi (keshatajwa) ulilenga kufafanua athari za unyambulishaji kisintaksia. Aidha, anagundua kuwa vitenzi vya Kikuria kama ilivyo kwenye lugha nyingi za Kibantu huwa na sifa tofauti tofauti kulingana na aina ya kitenzi. Kwa mfano, anasema kuwa vitenzi si elekezi havihitaji yambwa wakati vitenzi elekezi huhitaji yambwa moja au mbili kulingana na asili ya kitenzi chenyewe. Katika kazi yake anatambua kauli ya utendea, usababishi, utendano, utendwa na utendeka. Anaeleza kuwa athari ya vitenzi hivi hutofautiana kutokana na aina za viambishi vilivyopachikwa kwenye mizizi ya vitenzi hivyo. Utafiti wa Charwi (keshatajwa) ulifaa utafiti huu kwani amebainisha kauli mbalimbali za unyambulishaji wa vitenzi ambazo pia zimeshughulikiwa katika utafiti huu. Hata hivyo, utafiti wake unatofautiana na huu kwani alilenga kuonyesha athari za unyambulishaji kisintaksia hususan dhana ya uelekezi lakini utafiti huu ulionyesha athari ya unyambulishaji kisemantiki.

Gitonga (2014) alishughulikia upatanishi katika sentensi ya lahaja ya Kichuka ili kuchunguza uhusiano uliopo baina ya viambajengo katika sentensi, hasa uhusiano wa kiupatanishi kati ya virai nomino na virai vitenzi. Katika utafiti wake, Gitonga (keshatajwa) alibainisha kategoria miundo katika Kichuka ambapo alieleza kuhusu nomino, kivumishi, kiwakilishi na kitenzi. Katika vitenzi, alionyesha kuwa Kichuka huwa na kitenzi kielekezi na kisoelekezi dhana ambayo hupatikana baada ya mnyambuliko. Anaeleza kuwa kitenzi cha Kichuka ndicho chenye uwezo wa kunyambuliwa zaidi kuliko kategoria zingine za maneno. Anatoa mfano wa kitenzi #ntagūkanirie# (nilikuonya) ili kubainisha viambishi. Anachanganua viambishi ifuatavyo,

/n- ta- gũ- kan- iri- e/  
{n}- mofu ya nafsi ya kwanza umoja  
{ta}- mofu ya wakati uliopita hali timilifu  
{gũ}- mofu ya mtendwa/ kitendwa  
{kan}-mzizi  
{iri}-kauli ya mnyambuliko  
{e} – kiishio

Katika utafiti wake, Gitonga (keshatajwa) alishughulikia pia upatanishi katika sentensi radidi ya Kichuka, ambapo anatambua kwamba sentensi ya aina hii huwa na kitenzi kinachorudiwa mara mbili. Utafiti wake Gitonga (keshatajwa) ulifaa utafiti huu kwani aligusia suala la vitenzi elekezi na sielekezi dhana ambayo ilishughulikiwa katika utafiti huu hasa katika kauli ya kutendea. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na huu kwani utafiti wake Gitonga (keshatajwa) ulijikita katika kiwango cha isimu cha sintaksia kinyume na utafiti huu uliojikita katika kiwango cha isimu cha mofolojia.

Buberwa (2014) alichunguza ruwaza za kimofolojia za majina ya mahali ya Kihaya kwa kuchanganua vijenzi mbalimbali vinavyojenga majina hayo kwa kuongozwa na nadharia ya Mofolojia Leksika. Buberwa (keshatajwa) alibaini kuwa majina ya mahali ya Kihaya yameundwa kwa vijenzi mbalimbali na akachanganua majina yenye muundo wa nomino, majina ya mahali nyambulishi na majina ya mahali yenye muundo wa videnzi. Buberwa (keshatajwa) alitambua kwamba baadhi ya majina ya mahali ya Kihaya yaliundwa kutokana na unyambulishaji wa videnzi. Alitumia miundo mitatu tofauti kuonyesha majina ya mahali yanayotokana na videnzi. Miundo hii ni pamoja na; Kiambishi-ngeli, mzizi na Kiambishi nominishi [ng+Mz+K/no], muundo wa Kiambishi-ngeli, mzizi, kiambishi cha utendea na kiambishi nominishi [ng+Mz+tda+K/no] na muundo wa Kiambishi-tangulizi, kiambishi-ngeli1, kiambishi-ngeli2, mzizi, kiambishi cha utendana, kiambishi cha utendea na kiambishi nominishi [Kt+ng1+ng2+Mz+tn+tda=K/no]. Buberwa (2014) alitoa mifano mbalimbali ya majina ya Kihaya yenye viambishi vya utendea -er- na -ir- na vya utendana –an-vinavyojitokeza kabla ya kiambishi nominishi –o. Mifano hii ni kama vile,

Kagabiro- ka-gab-**ir**-o (mahali pa kugawia/ kutoa sadaka kwa Mungu)

Katerero- ka-teer-**er**-o (mahali pa kupigia)

Omwishuuraniro- O-mu-i-shuur-**an-ir**-o (mahali pa kusalimia)

Makala ya Buberwa (keshatajwa) ilifaa utafiti huu kwani kwa kiasi aligusia kauli za unyambulishaji za utendea na utendana katika ujenzi wa majina ya Kihaya. Kauli hizi zinaonyesha viambishi vya unyambulishaji ambavyo vipo katika Kigīchūgū. Makala ya Buberwa (keshatajwa) pia yalitoa mwongozo kuhusiana na Nadharia ya Mofolojia Leksia ambayo ni mojawapo ya nadharia iliyotumiwa katika utafiti huu. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na makala ya Buberwa (keshatajwa) kwani alijikita katika mofolojia ya uundaji wa majina na utafiti huu ulijihuisha na mofolojia ya unyambulishaji wa vitenzi.

Akishughulikia mofosintaksia katika uambishaji wa vitenzi, Gatamu (2014) alichunguza jinsi viambishi vya nyakati na hali vinavyojitokeza katika vitenzi vya Kimbeere. Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya Uminimalisti. Katika utafiti wake, Gatamu (keshatajwa) alichunguza nyakati katika Kimbeere kwa kuzingatia wakati uliopo na wakati ujao. Utafiti wake pia ulionyesha mifuatano ya nyakati na hali katika ruwaza ya vitenzi. Utafiti wa Gatamu (keshatajwa) ulibaini kuwa Kimbeere kama lugha zingine za Kibantu ni lugha ambishi. Anaonyesha kuwa vitenzi vya Kimbeere huambishwa kwa kuongeza mofimu zenyenye maana kwenye mzizi, ambavyo vinaweza kutokea kabla au baada ya mzizi. Utafiti wake Gatamu (keshatajwa) ulifaaa utafiti huu kwani ulijikita katika mofolojia ya uundaji wa maneno hasa vitenzi, sawa na utafiti huu ambaa ulijikita katika mofolojia ya unyambulishaji wa vitenzi. Tofauti ni kuwa utafiti wa Gatamu ulishughulikia viambishi awali vinavyopachikwa kabla ya mzizi lakini utafiti huu ulishughulikia viambishi tamati ambavyo hupachikwa baada ya mzizi wa vitenzi vya Kigīchūgū.

Mbaka (2015) alishughulikia mofosintaksia ya kauli tendeshi katika sentensi za Gichuka akiwa na lengo la kubaini kanuni zinazotawala katika kauli hii. Katika utafiti wake, anaeleza kuwa mofimu za utendeshi za Gichuka ni /-i-/ au /-ith-/. Katika utafiti wake, anatambua kuwa mofimu hizi za utendeshi huambikwa kwenye vitenzi kuonyesha kuwa mtenda amesababisha mtu au kitu kingine kufanya kitendo. Mbaka (keshatajwa) anasema kuwa kauli tendeshi hutumiwa katika vitenzi vyote vya Gichuka; aidha elekezi au si elekezi. Anatumia mfano kama vile #riria# (liza) na #nyaria# (kausha) ambavyo huwa elekezi kwa kuongeza yambwa. Utafiti wa Mbaka (keshatajwa) ulifaa utafiti huu kwani ulitoa mwongozo katika unyambulishaji katika

kauli ya kutendesha, mojawapo ya kauli zinazoshughulikiwa katika utafiti huu. Hata hivyo, utafiti wa Mbaka (keshatajwa) ni tofauti na utafiti huu kwani ulijikita katika kauli moja ya unyambulishaji kinyume na utafiti huu ulioshughulikia kauli sita za unyambulishaji ambazo ni: Kauli ya kutendea, kutendwa, kutendesha, kutendana, kutendeka na kutendua.

Chiumbo (2016) alishughulikia unyambulishaji wa vitenzi katika Tonga. Katika utafiti wake, alijadili maumbo ya viambishi nyambulishi na mifuatano mbalimbali ya vitenzi katika Tonga huku akiongozwa na nadharia ya Kioo na Kiolezo. Utafiti wake Chiumbo (keshatajwa) ulibaini kuwa vitenzi vya Tonga vina uwezo mkubwa wa kuambishwa viambishi mbalimbali vya unyambulishaji. Alibainisha kuwa katika mfuatano wa viambishi nyambulishi, mofimu za utendeshi na utendea kila wakati hutangulia mofimu nyambulishi nyingine. Utafiti wa Chiumbo (2016) ulifaa utafiti huu kwani tafiti zote mbili zinahusu unyambulishaji wa vitenzi. Vilevile utafiti wake ulitoa mwanga kuhusu mifuatano mbalimbali ambayo huenda ikapatikana katika unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū.

Akishughulikia mofosintaksia katika vitenzi vya Keiyo, Jepkoech (2018) alitambua na kujadili mofimu ambishi na nyambulishi. Alilenga kutambua ruwaza za upachikaji katika mpangilio wa vitenzi na kuchanganua kanuni za kimofosintaksia zinazoathiri upachikaji wa viambishi katika kitensi cha Keiyo. Mtafiti aliongozwa na Nadharia ya Kioo. Katika kazi yake, Jepkoech (keshatajwa) alitambua kwamba mofimu ambishi hutokea mwanzoni mwa kitensi cha Keiyo isipokuwa zile ambazo huonyesha wakati uliopo na hali ya kuendelea. Alitambua pia kuwa mofimu nyambulishi hutokea mwishoni baada ya mzizi. Katika kazi yake, mtafiti alionyesha kuwa mofimu ambishi hufuata utaratibu wa wakati → ukarusho → hali → nafsi → mzizi. Kwa upande mwingine, alionyesha kuwa mofimu nyambulishi huchukua taratibu mbalimbali. Utafiti wa Jepkoech (keshatajwa), ulifaa utafiti huu kwani ulishughulikia unyambulishaji wa vitenzi sawa na utafiti huu. Utafiti wake pia ulitoa mwanga katika Nadharia ya Kioo kwani ni Nadharia ambayo ilitumiwa katika utafiti huu pamoja na Nadharia ya Mofolojia Leksia. Hata hivyo, utafiti wa Jepkoech ni tofauti na huu kwani Keiyo ni lugha ya Kinilotiki ilhali Kigīchūgū ni Kibantu.

### **2.3 Maandishi kuhusu Lugha ya Kikuyu**

Watafiti wengi wametafitia lugha ya Kikuyu. Kwa mfano, Njoroge (1978), alishughulikia suala la mofolojia ya lugha ya Kikuyu kwa mujibu wa Nadharia ya Sarufi Geuza Maumbo Zalishi. Aliangalia taratibu za uundaji wa nomino kutokana na vitenzi katika lugha ya Kikuyu kupitia unyambuaji. Utafiti wa Njoroge (keshatajwa) ni tofauti na huu kwani Njoroge (keshatajwa) alijishughulisha na uundaji wa nomino kupitia unyambulishaji. Katika kazi yake alionyesha jinsi vitenzi huambikwa viambishi awali kabla ya mzizi na viambishi tamati baada ya mzizi. Utafiti wake uliegemea kwenye mofolojia kama ilivyo katika utafiti huu ingawa utafiti huu ulizingatia mnyambuliko wa vitenzi kwa kuongozwa na nadharia ya Mofolojia Leksia na Kanuni ya Kioo.

Akishughulikia mofofonolojia ya Kiswahili sanifu na Kikuyu sanifu, Njuguna (1992) alilenga kuonyesha ufanano uliopo katika sauti za Kiswahili na Kikuyu na kuonyesha mifanyiko ambayo hupitiwa na fonimu hizi. Anatambua mabadiliko ambayo hutokea katika fonimu za Kikuyu kama vile udondoshaji, uyeyushaji, ukakaaishaji na pia uwiano wa vokali. Utafiti wa Njuguna (keshatajwa) ulifaa utafiti huu kwani ulitoa mwongozo kuhusu mabadiliko ambayo hutokea katika irabu za Kigīchūgū kama inavyojadiliwa kwa mujibu wa Nadharia ya M.L. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na huu kwa kuwa umejikita katika kiwango cha Isimu cha fonolojia kinyume na utafiti huu uliojikita katika kiwango cha Isimu cha mofolojia hasa unyambulishaji wa vitenzi.

Mwihaki (1998) alitafiti kuhusu utohozi fonolojia wa maneno mkopo ya Kikūyū kutoka Kiingereza. Alifanya utafiti kwa lengo la kuangazia mageuko yanayotokea katika maneno mkopo hayo. Anaeleza kuwa fonimu ndicho kipengele muhimu katika utohozi fonolojia. Utafiti wa Mwihaki (keshatajwa) uliongozwa na Nadharia ya Fonolojia Zalishi iliyoegejemea katika mtazamo wa Fonolojia Tenganishi na Fonolojia Mizanishi. Kazi ya Mwihaki (keshatajwa) ni muhimu katika utafiti huu kwani alishughulikia lugha ya Kikūyū ambayo pia imeshughulikiwa katika utafiti huu kupitia Kigīchūgū, hivyo basi utafiti wake ulitupa mwanga kuhusiana na lugha hii ya Kikuyu. Tofauti ya utafiti wake na huu ni kwamba alijikita katika utohozi wa maneno na utafiti huu ulijikita katika unyambulishaji wa vitenzi. Tofauti inajitokeza kwani

utafiti wa Mwihaki (keshatajwa) ulilenga lugha mbili tofauti bali huu ulihusu lugha moja ya Kibantu; Kigīchūgū.

Gicheru (1999) katika uchunguzi wake, amelinganisha muundo wa kikundi nomino cha Kiswahili sanifu na ule wa Kikuyu cha Kabete huku akionyesha kufanana na kutofautiana kwake kwa kujikita katika isimu linganishi. Katika utafiti wake ameshughulikia aina za nomino zinazopatikana katika Kiswahili sanifu na Kikuyu cha Kabete pamoja na kufafanua nomino hizo kwa njia ya kiulinganisho. Amelinganisha pia muundo wa vipashio vya kikundi nomino katika lugha hizi mbili huku akifafanua na kulinganisha sheria kiisimu zinazotawala muundo wa vipashio hivyo. Alizingatia pia suala la toni katika lugha hizi. Utafiti wake Gicheru (keshatajwa) ni tofauti na utafiti huu kwa kuwa alijikita katika uchanganuzi wa nomino katika Kiswahili na Kikuyu lakini utafiti huu ulijikita katika unyambulishaji wa vitenzi vya Kigīchūgū.

Katika utafiti wake, Ngamau (2004) alishughulikia upatanisho wa kisarufi katika nomino na vitenzi vya Kikuyu kimfosintaksia, akiongozwa na nadharia ya Uminimalisti. Katika utafiti wake, anatambua kuwa nomino za Kikuyu hutambulishwa kulingana na viambishi vinavyoweza kupachikwa aidha katika umoja au wingi. Katika kazi yake, Ngamau (keshatajwa) anatambua makundi kumi ya ngeli za nomino katika Kikuyu. Katika sura ya tatu, anatambua kuwa Kikuyu ni lugha ambishi kama ilivyo katika lugha zingine za Kibantu. Anatambua kuwa mzizi wa vitenzi hukubali mofimu mbalimbali kama vile za nafsi, nyakati, hali na za mtendwa. Anaendelea kusema kuwa vitenzi hivi huchukua viambishi vya unyambulishaji. Ngamau (keshatajwa) katika utafiti wake, anaeleza kuwa mofimu hizi hazitokei kiholela bali hufuata utaratibu fulani. Anafafanua kitenzi cha Kikuyu kwa kuzingatia kauli ya utendea na kutambua viambishi nyambulishi {-īr-} na {-er-}. Kwa kiasi anadokeza upatanisho katika kauli ya kutendwa. Utafiti wake Ngamau (keshatajwa) ni tofauti na utafiti huu kwani aliegemea katika upatanisho wa kisarufi wa nomino na vitenzi kimfosintaksia kinyume na utafiti huu ambao ulishughulikia mifanyiko inayohusika katika unyambulishaji wa vitenzi vya Kigīchūgū. Hata hivyo utafiti wake ulifaa utafiti huu kwani aligusia kwa kiasi kauli ya kutendea na kutendwa ambazo pia zimeshughulikiwa katika utafiti huu.

Akishughulikia utohozi mofolojia wa maneno mkopo ya Kikūyū kutoka Kiswahili, Waithaka (2009) alilenga kubainisha kanuni na taratibu za kimofolojia zinazohusika katika utohozi, akiongozwa na mtazamo wa fonolojia leksia. Utafiti wake ulizingatia viwango vya fonolojia na mofolojia. Alibainisha kuwa Kikūyū ni lugha ambishi na kuwa uambishaji hudhihirika katika kitenzi arifu kwa wingi ili kueleza hali mbalimbali. Waithaka (keshatajwa) anatambua kuwa aina mbalimbali za viambishi awali na tamati huambikwa kwenye mzizi wa kitenzi kwa madhumuni ya kutoa kauli mbalimbali za kitenzi husika. Katika kazi yake, Waithaka (keshatajwa) alifafanua kuwa viambishi tamati huwekwa baada ya mzizi wa kitenzi kama inavyodhihirika katika viambishi vya unyambulishaji wa vitenzi. Utafiti wa Waithaka (keshatajwa) unafaa utafiti huu kwani unatoa mwelekeo bora kwani ingawa analishughulikia suala la utohozi wa maneno mkopo ya Kikūyū kutoka Kiswahili, amedokeza dhana ya unyambulishaji aliposhughulikia vitenzi vya Kikūyū kwa jumla. Licha ya utafiti wake Waithaka (keshatajwa) na utafiti huu kuongozwa na Nadharia ya Mofolojia Leksia, tofauti ni kwamba utafiti wake unazingatia utohozi wa maneno ilhali utafiti huu umeshughulika na unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū.

#### **2.4 Maandishi kuhusu Kigīchūgū**

Kamau (1996) alilinganisha mifanyiko ya kifonolojia kati ya lahaja za Kindia na Kigīchūgū za lugha ya Kikuyu. Katika utafiti huo, Kamau (keshatajwa) aliweka wazi tofauti zilizopo kati ya lahaja hizi kifonolojia katika vipengele kama vile irabu na konsonanti. Utafiti wa Kamau (keshatajwa) uliongozwa na nadharia ya Fonolojia Zalishi kinyume na utafiti huu unaojikita katika nadharia ya Mofolojia Leksia na Kanuni ya Kioo. Kamau (keshatajwa) alitathmini Mofolojia ya lahaja za Kigīchūgū na Kindia ili kueleza mageuzi ya kifonolojia yanayoathiri konsonanti na vokali kinyume na utafiti huu unaozingatia mnyambuliko wa vitenzi katika Kigīchūgū. Hata hivyo, utafiti wa Kamau (keshatajwa) ulitoa mwelekeo bayana kuhusu mageuzi ya sauti katika lugha ya Kigīchūgū hasa anapozingatia vokali katika lahaja ya Kigīchūgū. Utafiti wake umetoa mwelekeo hasa anapofafanua tofauti kati ya vitenzi vya Kigīchūgū na Kindia. Alibaini kuwa vitenzi vya Kigīchūgū huyeyusha irabu /o/ vinapofuatana na irabu /i/ na badala yake hutumia nusu irabu /w/ kama inavyodhihirika katika kitenzi,

/Kū+ina/→[kwina] (imba). Maelezo yake Kamau (keshatajwa) yamesaidia kutoa mwanga kuhusu uwiano wa vokali katika unyambulishaji wa vitenzi.

Akishughulikia toni kama sifa kuu ya kutofautisha maana katika maneno ya Kigīchūgū, Wachera (2008) alizingatia maneno kama vile: nomino, vitenzi, viwakilishi, vivumishi, vielezi na vihusishi. Utafiti wake unajikita katika kiwango cha fonolojia na mofolojia ya Kigīchūgū. Utafiti wake Wachera (keshatajwa) ulibaiani kuwa toni katika Kigīchūgū huleta tofauti ya maana katika maneno husika. Utafiti wake ulifaa utafiti huu kwa kuwa ulitoa mwongozo kuhusu Kigīchūgū lahaja ambayo ilishughulikiwa katika utafiti huu. Hata hivyo, tofauti ni kwamba utafiti wa Wachera (keshatajwa) ulishughulikia toni lakini utsafiti huu ulishughulikia unyambulishaji wa vitenzi.

Akiweka wazi vitamkwa nya konsonanti za Kindia na kwa kiasi fulani kulinganisha na Kigīchūgū, Ruri (2011) alichanganua maneno katika sauti kwa sababu maneno katika lugha fulani hujengwa kwa vipande sauti ambavyo ni fonimu. Alibainisha na kufafanua konsonanti za lahaja ya Kindia kwa kuzingatia sifa nne bainifu; Ukonsonanti, jinsi ya kutamka, mahali pa kutamkia na ughuna au usoghuna. Tofauti ya utafiti wa Ruri (keshatajwa) na huu ni kuwa aliongozwa na nadharia ya Fonolojia Zalishi kinyume na utafiti wetu unaoongozwa na nadharia ya Mofolojia Leksia na Kanuni ya Kioo. Tofauti pia inajitokeza kwani utafiti wake unajikita katika kiwango cha isimu cha fonolojia kinyume na utafiti huu ambao umejikita katika kiwango cha mofolojia. Hata hivyo, utafiti wake Ruri (keshatajwa) unatoa mwongozo hasa anapofafanua kuhusu fonimu za Kigīchūgū na lahaja zingine za Kikuyu.

Karuru (2012) alishughulikia maneno mkopo ya Kigīchūgū kutoka Kiswahili. Anaeleza kuwa kikuyu na Kiswahili ni lugha za Kibantu na hivyo muundo wa maneno katika lugha hizi mbili unalingana kwa kiasi kikubwa. Katika utafiti wake, Karuru (keshatajwa) anatambua tofauti za fonimu katika lugha hizi mbili ambapo anaeleza kuwa Kigīchūgū kina irabu kumi na nne ilhali Kiswahili kina irabu tano. Kwa upande mwingine, anatambua konsonanti kumi na saba za Kigīchūgū na ishirini na sita za Kiswahili. Katika utafiti wake anaeleza kuwa Kigīchūgū huwa na silabi wazi tu ikilinganishwa na Kiswahili ambacho huwa na silabi wazi pamoja na fungo.

Anaeleza kuwa Kigīchūgū hukopa maneno kutoka Kiswahili aidha kwa kudondo , kuhifadhi au ukakaishaji wa konsonanti. Anatoa mifano kama vile;

<b>Kiswahili</b>	<b>Kigīchūgū</b>
kahawa	Kaoa
kalamu	Karamu
mabati	maβati

Katika utafiti wake, Karuri keshatajwa anaeleza kuwa Kigīchūgū vilevile hukopa maneno kutoka Kiswahili kwa kudumisha irabu, au kwa kuongeza irabu ambapo anatoa mifano kama vile;

<b>Kiswahili</b>	<b>Kigīchūgū</b>
mpira	mūβira
mkate	mūgate
kalia	īkarīra
soma	thoma

Utafiti wake Karuru (keshatajwa) ulifaa utafiti huu kwani ulitoa mwongozo kuhusiana na lahaja ya Kigīchūgū. Hata hivyo, tofauti ni kwamba utafiti wake ulijikita katika nomino mkopo za Kigīchūgū ilhali utafiti huu ulishughulikia unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū.

Kutokana na mapitio ya maandishi ni dhahiri kwamba watafiti wengi wamezingatia unyambulishaji wa vitenzi katika lugha ya Kiswahili na baadhi ya lugha nyingine za Kibantu. Utafiti huu ulizingatia unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū ili kuonyesha mifanyiko inayohusika katika unyambulishaji wake na kufafanua kanuni zinazoruhusu au kuzuia mifanyiko hiyo.

## 2.5 Misingi ya Kinadharia

Utafiti huu ulijikita katika misingi ya nadharia ya Mofolojia Leksia (ML). Kwa mujibu wa Kiparsky (1982) na Katamba na Stonham (1993) nadharia ya Mofolojia Leksia iliibuka kufidia mtazamo wa Chomsky wa sarufi zalishi (SZ) ambao haukutambua kiwango cha mofolojia kama kiwango mahususi cha lugha. Nadharia ya


ML inaonyesha uhusiano wa sheria zinazojenga maumbo ya kimofolojia na sheria zinazodhibiti namna maumbo haya yanavyotamkwa. Katamba na Stonham (keshatajwa) wamefafanua Nadharia ya Mofolojia Leksia kwa kuzingatia uambishi wa maneno kwa jumla vikiwemo vitenzi. Nadharia ya Mofolojia Leksia (ML) inatambua viwango viwili vyta sheria: sheria leksia na sheria kirai. Sheria Leksia ni zile ambazo zinafungamana na kanuni za kifonolojia katika kuunda neno husika kwa namna ambavyo umbo la mzizi hubadilika linapoongezewa viambishi katika neno. Sheria Kirai huathiri kiambishi katika neno kwa kukipitisha mageuzi yanayohusu vokali zinazopatikana. Aghalabu viambishi awali katika maneno ndivyo huathirika na vokali zinazopitia mageuzi katika viambishi hivi ni /u/ na /i/. Inabainika kwamba vokali /u/ na /i/ katika mazingira ya mfululizo wa vokali nyingine ya awali ya mzizi wa neno zinasawiri mageuzi kama vile: Irabu /u/ inapokutana na irabu nyingine isipokuwa yenyewe, nusu irabu /w/ huundwa na irabu /i/ inapokutana na nyingine isipokuwa yenyewe kiyeyusho /j/ (y) huundwa kama inavyodhihirika katika mageuzi yafuatayo katika Kigīchūgū.

/kū/+/ina/	→ [kwina]	(imba)
/kū/+/ingīra/	→ [kwingīra]	(ingia)
/kū/+/enda/	→ [kwenda]	(penda)
/vi/+/ao/	→ [vjao]	(vyao)
/bi/+/aku/	→ [bjaku]	(vyako)

Kutokana na mifano hii, ni dhahiri kwamba sheria kirai ina nafasi kubwa katika mageuzi ya maumbo maneno. Hivyo basi, sheria hii ya mofolojia leksia inaweza kutumiwa kikamilifu kwa kuonyesha bayana unyambulishaji na mageuzi ya maumbo ya vitenzi mahususi. Kwa kifupi, Mofolojia Leksia hushughulikia uwiano kati ya fonolojia na mofolojia ikitilia maanani mofolojia.

ML inahusisha mihimili sita ya uamilifu wa sheria mahususi za kisarufi. (Katamba na Stonham 1993). Mihimili hii ni; , mzunguko wa sheria, , na ufinyu wa sifa. Kwanza, mhimili wa ngazi leksia unazingatia kwamba umbo la neno linaweza kuelezwu kupitia maumbo ya kisarufi yaani mofimu zenye daraja za mahusiano. (Kiparsky, 1982 na Katamba na Stonham, 1993). Kwa mfano, kitende cha Kigīchūgū [kuruga] (kupika) kina maumbo yafuatayo:


### Ngazi leksia katika kitenzi [kuruga]



Maumbo haya yametenganishwa kwa kuzingatia ngazi ambapo kila umbo lina maana bainifu ya kisarufi. Ngazi hizi huwa zenyе mahusiano na zinapotenganishwa haziwezi kutoa maana yoyote. Kwa mfano /rug/ peke yake haina maana yoyote mpaka iunganishwe na kiambishi awali /kū/ pamoja na kiishio /a/ ili kutoa maana ya #kūruga# (kupika). Aidha, kiishio /a/ na kiambishi awali /kū/ havina maana yoyote hadi pale ambapo vinapounganishwa na mzizi /rug/ wa kitenzi husika. Umuhimu wa kanuni hii katika utafiti ni kuwa unyambulishaji hufanywa kwa utaratibu ambao hufanyika kwa hatua.

Pili, wa mzunguko wa sheria husisitiza kuwa sheria za kiwango kimoja za kifonolojia zinaenda sambamba na uambishaji wa kiwango sawa cha kimofolojia. Wakati kiambishi kinachopekwa kwenye mzizi wa neno, mageuzi ya kifonolojia huambatana katika kiwango kilekile kama inavodhihirika katika kielelezo kifuatacho.

## Mzunguko wa sheria



(Asili: Kiparsky 1982:133)

Kanuni ya mzunguko kamili hivyo basi inatawala uamilifu wa sheria. Kiambishi kinapoambikwa kwenye mzizi wa kitenzi, kinaandamana na mageuko ya kifonolojia katika kiwango kile. Aidha kiambishi kingine kikiongezewa, vilevile huandama mageuko ya kifonolojia. Kila ngazi huwa na sheria zake maalum ambazo haziwezi kamwe kurejelewa katika ngazi tofauti, lakini uamilifu huo wa sheria ulihitaji pia kuzingatia kanuni ya kufuta mabano.

Tatu, mhimili wa kufuta mabano unazingatia kwamba wakati sheria ya kiwango kimoja ya kifonolojia imetumika, mabano yake hufutwa mpaka mwishowe neno lenye umbo kamili na maana ya kileksia pamoja na umbo la kimofolojia linapatikana kama inavyodhihirika katika kitenzi [kwina] (kuimba)

[[[kū [in] a]]]- Kitenzi hiki kimetengwa katika maumbo tofauti kwa kutumia mabano.

[[kū [ina]] - Kiishio {a} kina uhusiano zaidi na shina la kitenzi hivyo basi kinachopekwa kwenye mzizi wa kitenzi. Baada ya muungano wa maumbo haya mawili mabano yake yanafutwa ili kusawiri umbo moja.

[kwina]- Katika hatua hii, kiambishi awali kinaungana na shina la kitenzi ili kupata kitenzi sahili. Hata hivyo sehemu hii inatambua mageuzi ya kifonolojia ya uyeyushaji vokali pale ambapo vokali /u/ inageuka na kuwa /w/.

#kwina#- Baada ya maumbo yote kujumuika, mabano hufutwa na kuwa na umbo moja la kitenzi lenye maana kamili ya kileksia. Mhimili huu umetumika kwa sababu umeonyesha kwamba hata baada ya mageuzi ya unyambulishaji wa vitenzi, maumbo mbalimbali huungana na kuwa kitenzi kimoja kamili.

Nne, mhimili wa kuhifadhi muundo hutambua kwamba baada ya mageuzi ya kifonolojia, muundo wa lugha mahususi sharti uhifadhiwe (Katamba na Stonham, 1993). Kwa mfano, muundo wa lugha za Kibantu ukiwemo Kigīchūgū ni ule wa mfuatano wa Konsonanti-Vokali (K-V). Kitenzi cha Kigīchūgū /kū+iya/ [kwiya] (kuiba) kimeweza kutoa kielelezo bora. Uchopekaji wa kiishio {a} unafunga mzizi wa kitenzi kwa vokali. Uyeyushaji wa vokali /u/ katika kiambishi awali unazalisha fonimu changamano {kw} ambayo inatamkwa kama fonimu moja hivyo basi umbo bora la K-V linadumishwa.

Tano, mhimili wa ufinyu wa sifa hupinga uwakilishi wa sifa zenye uziada. Sifa huwa na uziada iwapo kuhusika kwake kunaweza kutabirika. Kwa mfano katika sheria ya udondoshaji na uyeyushaji, sauti zote za vokali huwa ghuna. Kwa hivyo, sifa moja ikitajwa hakutakuwa na haja ya kutaja ile nyingine. Kanuni hii ilitumika pale ambapo sifa za fonimu zilihitajika kuelezwaa baada ya kuambisha viambishi tamati katika vitenzi.

Sita, mhimili wa kwingineko hutumiwa pale ambapo sheria mbili huonekana kushindania nafasi moja. Hali hii hudhahirika katika mofolojia ambapo baada ya uambishi awali katika vitenzi vokali mbili huwa zinafuatana. Jambo hili litokeapo, udondoshaji wa vokali na uyeyushaji wa vokali hutumikizwa (Katamba na Stonham, 1993). Hata hivyo, mhimili wa kwingineko unapendekeza uyeyushaji wa vokali kwa

sababu udondoshaji hutumika katika mazingira mengi. Mfano wa kitenzi [kwina] (kuimba) unadhihirisha uyeyushaji wa vokali. Hii ni kwa sababu kitenzi hiki kina vokali mbili ambazo zinafuatana yaani: [kuina]. Vokali /u/ inapitia uyeyushaji na kuwa /w/ badala ya kudondoshwa. Hata hivyo, mihimili minne ndiyo iliyotumika katika uchanganuzi wa unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū. Mihimili hiyo ni pamoja na; ngazi leksia, kufuta mabano, kwingineko na kuhifadhi muundo.

Nadharia ya ML ilifaa katika utafiti huu kwani ilisaidia kuonyesha jinsi kanuni za kifonolojia na kimofolojia hushirikiana katika unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū. Aidha, ilitusaidia kueleza taratibu za kuongeza viambishi katika vitenzi ili kubainisha maana mbalimbali zinazowakilishwa.

Aidha, Kanuni ya Kioo pia iliongoza utafiti huu. Kanuni hii kulingana na Baker (1985), ni mojawapo ya mihimili muhimu katika nadharia za kiisimu ambayo inadai kwamba mifuatano ya kisintaksia na kimofolojia huwa na uhusiano na ulingano kwa kiasi kikubwa. Baker (keshatajwa) anasema kwamba, iwapo sintaksia na mofolojia ni mojawapo ya sura muhimu katika isimu, basi kanuni zinazotawala katika kiwango cha mofolojia ni lazima ziafiki au ziathiriwe pakubwa na kanuni zinazotawala katika kiwango cha sintaksia. Baker (keshatajwa) anaendelea kusema kuwa unyambulishaji kimofolojia ni lazima uakisi mfuatano wa kisintaksia na kinyume chake. Kwa mujibu wa Baker (1985), unyambulishaji wa vitenzi katika lugha za Kibantu hufuata mpangilio maalum. Kanuni ya Kioo inaeleza kwamba mfuatano wa viambishi nyambulishi huathiriwa na;

- a. Maana za viambishi zinaffaa kujitokeza katika kitenzi husika.
- b. Muundo wa kisintaksia katika lugha husika. Yaani muundo wa viambajengo vya sentensi huathiri utaratibu wa mofimu.
- c. Mifuatano ya mofimu zinazofanya kazi pamoja. Yaani mofimu za uundaji wa maneno zinaffaa kutokea katika upande mmoja wa neno na mofimu za unyambulishaji wa maneno zinaffaa kutokea upande mmoja wa neno. Hali hii inajitokeza katika vitenzi vya Kigīchūgū kama vile, thom-a (soma) thom-**er**-a (somea) thom-**ith-ir-w-a** (someshewa) ambapo mofimu za unyambulishaji zinatokea upande mmoja baada ya mzizi wa neno.

Kwa mujibu wa Baker (keshatajwa) katika Kanuni ya Kioo, anaendelea kusema kuwa lugha mbalimbali hupangilia mofimu hizi katika utaratibu ambao utaakisi miundo kisemantiki. Kanuni hii inaeleza kuwa mofimu ambazo zinaathiri maana katika vitenzi zinafaa kutokea karibu na mzizi wa vitenzi ikilinganishwa na mofimu ambazo hazina uzito kimaana kwa kitenzi husika. Kulingana na Kanuni ya Kioo, mfuatano wa vipengele vya kisintaksia katika lugha huathiri mfuatano wa mofimu na vilevile mfuatano wa vipengele kisintaksia katika sentensi unafaa kuakisi mfuatano wa mofimu husika. Kulingana na Kanuni ya Kioo, maana ya sentensi inafaa kudhihirisha utaratibu na mfuatano wa mofimu nyambulishi katika vitenzi. Kanuni hii ilifaa utafiti huu kwani ilisaidia katika kushughulikia mifanyiko inayohusika na unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū mojawapo ya lugha za Kibantu, na pia ilifaa katika kufafanua maana zinazowakilishwa na mifanyiko hiyo ya unyambulishaji.

## 2.6 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia yaliyoandikwa kuhusiana na utafiti huu. Katika kufanya hivyo, tofauti na uhusiano katika unyambulishaji wa vitenzi zimefanuliwa. Maandishi pia kuhusiana na lugha ya Kikuyu ikiwemo Kigīchūgū yamepitiwa. Maandishi haya yanadhihirisha kuwa Kigīchūgū kimeshughulikiwa kwa ufinyu sana. Kazi mbalimbali ambazo zimepitiwa katika sura hii zilimwezesha mtafiti kuelewa njia za kitaaluma zinazozingatiwa katika tafiti za kiisimu. Mbali na mapitio ya maandishi, nadharia zilizoongoza utafiti zimejadiliwa katika sura hii. Nadharia zilizotumiwa ni ML iliyoasiwa na Kiparsky (1982) na kuendelezwa na Katamba na Stonham (1993) na Kanuni ya Kioo iliyoasiwa na Baker (1985). Misingi ya nadharia hizi imefafanuliwa kwa kina. Sababu ya kuchagua nadharia ya ML na Kanuni ya Kioo ni kuwa nadharia hizi zina nafasi kubwa katika unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū.

## **SURA YA TATU MBINU ZA UTAFITI**

### **3.1 Eneo la Utafiti**

Utafiti huu ulifanyika katika Tarafa ya Gichūgū hasa Kata ya Kabare, Karumandi, Baragwi, Ngariama na Njukiini. Tarafa ya Gichūgū inapatikana katika Kaunti ya Kirinyaga hasa Kaunti ndogo ya Kirinyaga Mashariki. Kigīchūgū hutumiwa katika Kaunti ndogo ya Kirinyaga Mashariki kama lugha ya mawasiliano. Eneo hili lilichaguliwa kwa sababu ndilo lenye wazawa wenye umilisi na uelewa wa Kigīchūgū Vilevile, eneo hili lina wazungumzaji asilia wa Kigīchūgū hivyo basi walichangia katika kutoa vitenzi vya Kigīchūgū ambayo ndiyo data inayostahili katika utafiti huu.

### **3.2 Mpango wa Utafiti**

Utafiti huu ulifanywa kwa kudurusu vitabu, majorida na tasnifu mbalimbali kwa minajili ya mwauo wa maandishi na nadharia za utafiti. Mtafiti alisoma vitabu vinavyohusu nadharia ya Mofolojia Leksia na Kanuni ya Kioo ili kupata uelewa zaidi wa kuzitumia katika utafiti huu. Aidha mtafiti alisoma kwa jumla kazi zilizoandikwa kuhusu mnyambuliko wa vitenzi ili kuelewa mifanyiko inayohusika katika unyambulishaji, kanuni zinazoruhusu na kuzuia mifanyiko hiyo na maana mbalimbali zinazowakilishwa. Mtafiti alichuja mawazo ya watu wengine ili kuyalinganisha na kuyalinganua na utafiti huu.

### **3.3 Walengwa wa Utafiti**

Utafiti huu uliwalenga Wagīchūgū wanaozungumza Kigīchūgū kama lugha yao ya kwanza na kuitumia katika mawasiliano. Walengwa hawa ni wazawa na wana umilisi pamoja na uelewa wa Kigīchūgū. Licha ya tofauti zao za umri, tajriba na vyeo, wakaazi hawa hutumia vitenzi katika sentensi zao ambazo huhusu mambo mbalimbali ikiwemo biashara, kilimo, hisia, hali ya afya mionganoni mwa masuala mengine ya maisha ya binadamu.

### **3.4 Vifaa vya Utafiti**

Data ya utafiti huu ilikuwa vitenzi vya Kigīchūgū na unyambulishaji wake katika kauli mbalimbali. Data katika utafiti huu ilikusanya kupitia jedwali la unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū. Jedwali hili lilipangwa katika kauli sita za unyambulishaji; kauli ya Kutendea, Kutendwa, Kutendesa, Kutendana, Kutendeka

na Kutendua. Vitenzi vilivyozaishwa na mtafiti na alivyopata kutoka kwa wasailiwa vilirodheshwa ili kubaini mifanyiko inayohusika katika unyambulishaji huo na kutathmini maana zinazowakilishwa na mifanyiko hiyo.

### **3.5 Utafiti wa Maktabani**

Utafiti huu ulifanyika maktabani. Mtindo huu ulimwezesha mtafiti kuunga yale yaliyoandikwa kuhusiana na unyambulishaji wa vitenzi. Mtafiti alitembelea maktaba za vyuo vikuu mbalimbali kama vile maktaba za vyuo vikuu vya Chuka, Moi, Kenyatta na Nairobi ili kudurusu kwa kina maandishi kama vile majarida, magazeti, vitabu na tasnifu zilizoandikwa kuhusu suala la unyambulishaji wa vitenzi. Mtafiti pia aliweza kupata na kusoma mengi kuhusu mifanyiko mbalimbali ya unyambulishaji wa vitenzi ambayo ilimwongoza katika utafiti wake wa unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū. Mtafiti pia alisoma zaidi kuhusu nadharia ya M.L na Kanuni ya Kioo ambazo ziliongoza katika uchanganuzi wa data.

### **3.6 Sampuli na Usampulishaji**

Data ya sampuli ya vitenzi vya Kigīchūgū imetumika katika utafiti huu. Sampuli iliyotumika ilikuwa ya Wagīchūgū wanaoishi katika maeneo ya Kabare, Karumandi, Baragwi, Ngariama na Njukiini. Maeneo haya yalishirikishwa katika usampulishaji ili kuwakilisha Wagīchūgū wote bila kuegemea sehemu moja. Maeneo haya vilevile ndiyo yenye wazungumzaji asilia wa Kigīchūgū hivyo data iliyopatikana ni ya kutegemeka. Wasailiwa 20 wenye umilisi na uelewa wa lugha ya Kigīchūgū walitumiwa. Idadi hii ilitumiwa kwa kuwa mtafiti ana umilisi wa lugha ya Kigīchūgū, hivyo alihakiki anachofahamu kuhusiana na unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū. Kwa upande mwengine, wasailiwa hawa walitumiwa ili mtafiti athibitishe data aliyozaisha ya vitenzi vya Kigīchūgū na pia kuondoa mapendeleo katika uzalishaji wa data. Usampulishaji wa makusudi ilitumiwa na watafitiwa walitoa taarifa zao kwa kujaza jedwali la usaili wa vitenzi vya Kigīchūgū. Kwa mujibu wa Chomsky (1957), mzawa wa lugha ana uwezo wa kuzalisha sentensi nyingi sahihi na zisizo na kikomo, kwa hivyo mtafiti alitunga sentensi za Kigīchūgū kisha kuchagua vitenzi sitini (60) ambavyo aliviweka katika kauli sita za unyambulishaji na kuainisha mifanyiko mbalimbali na maana zinazowakilishwa na vitenzi katika lugha ya Kigīchūgū. Idadi hii ilichaguliwali kuepuka uradidi unaoweza kujitekeza kwa

kuchagua idadi kubwa. Usampulishaji makusudi ultimiwa kwa kuwa mtafiti anao umilisi na uelewa wa lugha ya Kigīchūgū. Aidha, Chomsky (1988) anaeleza kuwa mzawa wa lugha huthibitisha kuwa na umilisi wa lugha yake hivyo kuwa na uwezo wa kuzalisha data bila kuwa na upendeleo. Chomsky (keshatajwa) anaeleza kuwa uwezo wa mzawa wa lugha kufahamu sauti katika lugha yake humwezesha kuunda sentensi ambazo maana yake si ya upendeleo au zenyé maana tata.

### **3.7 Maadili ya Utafiti**

Maadili ni masuala ambayo hayaepukiki katika kazi yoyote ile ya kiutafiti. Mtafiti alipata barua ya kuanzisha utafiti kutoka Chuo Kikuu cha Chuka. Mtafiti aliomba kibali cha kufanya utafiti kutoka kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi. Mtafiti alipata idhini kutoka kwa chifu katika jamii ya Wagīchūgū. Mtafiti alishirikiana na viongozi hawa ili kuelekezwa kwa watoa habari wasio watapeli. Utafiti huu ulifanywa kwa uwazi na uadilifu. Mtafiti alizalisha mwenyewe vitenzi sitini (60) vya Kigīchūgū ambavyo vilitumika katika utafiti huu. Mtafiti pia alipata vitenzi kutoka kwa wasailiwa ishirini wanaoishi maeneo ya Kabare, Karumandi, Baragwi, Ngariama na Njukiini ili kuthibitisha vitenzi alivyozalisha. Kwa upande wa wasailiwa, mtafiti alihakikisha kuwa hawabezi, hawashurutishwi kutoa habari na pia hawaulizwi maswali ya kudhalilisha. Usiri ulidumishwa kwa kiasi kikubwa na data iliyotolewa na wasailiwa ilitumika katika utafiti huu pekee. Mtafiti hakubuni vitenzi ambavyo vilivuruga kaida za Kigīchūgū. Data iliyozalishwa ilikuwa ya ukweli na kuaminika na ambayo inaweza kuthibitishwa na watafiti wa baadaye.

### **3.8 Ukusanyaji wa Data**

Ili kupata data ya unyambulishaji wa vitenzi vya Kigīchūgū, mtafiti alishiriki katika kutunga sentensi ambapo alichagua vitenzi sitini (60) katika lugha ya Kigīchūgū ambavyo alivipanga katika jedwali la usaili wa vitenzi vya Kigīchūgū kwa kushughulikia kauli sita za unyambulishaji na kuainisha kanuni za mageuzi katika Kigīchūgū. Idadi hii ilichaguliwa kutumika katika utafiti huu kwa sababu kulingana na Milroy (1987), tafiti za kiisimu, kama ulivyo utafiti huu, zinajulikana kuzalisha data yenye uradidi mwangi. Maoni yake ni kuwa kadri data ilivyo kubwa ndivyo kuna uwezekano wa uradidi. Aidha, kwa mujibu wa Chomsky (1957) mzawa wa lugha ana uwezo wa kuzalisha sentensi nyingi sahihi na zisizo na kikomo hivyo basi mtafiti

kama mzawa na mzungumzaji wa Kigīchūgū aliweza kuzalisha vitenzi ambavyo vilitumika katika utafiti huu.

### **3.9 Uchanganuzi wa Data**

Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kuzingatia viambishi vinavyofuata mzizi wa kitenzi moja kwa moja na pia viambishi nyambulishi nya pili na nya tatu kutoka kwenye mzizi vilijadiliwa. Maumbo yenyе mantiki ya vitenzi vilivyonyambuliwa pia yalishughulikiwa. Uchanganuzi wa data ulihusu vitenzi nya Kigīchūgū kupangwa katika kauli sita za unyambulishaji: Kauli ya kutenda, kutendeka, kutendwa, kutendana, kutendesha na kutendua. Kisha uchanganuzi ulihusisha utambuzi wa kanuni na mifanyiko mbalimbali inayopitiwa na vitenzi wakati wa unyambulishaji, utaratibu wa unyambulishaji wa vitenzi na kanuni zinazoruhusu au kuzuia mageuzi hayo pia zimefanuliwa na kutolewa mifano. Maana zinazowakilishwa na maumbo mbalimbali ya unyambulishaji katika Kigīchūgū pia ilifanuliwa. Data iliwasilishwa kwa maelezo, michoro, majedwali au vielelezo kulingana na malengo ya utafiti huu. Nadharia ya Mofolojia Leksia na Kanuni ya Kioo zilongoza katika uchanganuzi wa data. Nadharia ya M.L ilichangia katika utafiti huu kwani ilitumiwa kuonyesha unyambulishaji na maumbo ya vitenzi mahususi. Aidha ni Nadharia iliyotumiwa kutoa mwongozo wa jinsi viambishi huathirika katika vitenzi nya Kigīchūgū kwa kuvipitishia mageuzi yanayohusu vokali zinazopatikana. Kwa upande mwingine, Kanuni ya Kioo ilichangia katika utafiti huu kwani ndiyo iliyotumika kutoa mwongozo wa kuonyesha mpangilio maalum unaofuatwa katika mfuatano wa unyambulishaji wa vitenzi nya Kigīchūgū.

## SURA YA NNE

### MIFANYIKO YA UTARATIBU WA UNYAMBULISHAJI WA VITENZI KATIKA KIGĪCHŪGŪ

#### 4.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia mofolojia ya mofimu nyambulishi katika vitenzi vya Kigīchūgū. Lengo kuu ni kufafanua mabadiliko ya kimofofonolojia yanayotokea katika unyambulishaji wa vitenzi. Nadharia ya Mofolojia Leksia (Kiparsky, 1982 & Katamba na Stonham, 1993) na Kanuni ya Kioo (Baker, 1985) zimetumiwa kueleza mfuatano wa mofimu nyambulishi katika vitenzi vya Kigīchūgū. Kanuni zinazoruhusu au kuzuia mifuatano ya mofimu nyambulishi pia zilijadiliwa. Kwanza, sura hii imeanza kwa kutoa maelezo machache kuhusu fonimu za Kigīchūgū. Fonimu hizi ; konsonanti na irabu zimeelezwa ili kujenga msingi bora wa unyambulishaji wa vitenzi katika lugha hii.

#### 4.2 Fonimu za Kigīchūgū

Kwa mujibu wa TUKI (1990: 45), fonimu ni kipashio kidogo kabisa cha kifonolojia kinachobadili maana ya neno. Fonimu inaweza kubainishwa kwa kupambanisha jozi za maneno zinazotofautiana kwa sauti moja tu. Kwa mfano,

9. a) [būra]- chapa ————— [gūra]- nunua

b) [teta]- teta ————— [tema]-kata

Katika mifano hii, sauti /b/, /g/, /t/ na /m/ ni fonimu za Kigīchūgū kwani zinatofautisha maana ya maneno husika.

#### 4.2.1 Konsonanti za Kigīchūgū

Konsonanti ni aina ya sauti ambazo hutamkwa kwa kuzuia mkondo hewa kutoka mapafuni, ukipitia katika chemba ya kinywa na chemba ya pua kwenda nje (Kihore, Massamba & Msanjila, 2012). Mgullu (1999) anatambua konsonanti kama foni ambazo wakati wa kutamkwa hewa hutatizwa kwa namna fulani. Wakati mwingine hewa huzuiliwa kabisa na wakati mwingine hutatizwa kiasi au kubanwa kiasi fulani mahali fulani baada ya kupitia kongomeo.

Kigīchūgū hujumuisha mfumo wa konsonanti kumi na saba kama inavyojitokeza katika Jedwali 4.1 lifuatalo:

Jedwali 4.1: Konsonanti za Kigīchūgū

Fonimu	Tahajia	Maneno	Maana
β	b	[βuta]	futa
mb	mb	[thambia]	osha
m	m	[makia]	shitua
t	t	[tuma]	shona
θ	th	[θüküma]	fanya kibarua
nd	nd	[endia]	uza
n	n	[ina]	imba
r	r	[rathima]	bariki
š	c	[šünga]	sinzia
nj	nj	[ĩnjä]	chimba
ny	ny	[nua]	kunywa
j	y	[kaja]	Piga nduru
k	k	[koma]	lala
γ	g	[γüra]	nunua
ŋg	ng	[tongoria]	ongoza
ŋ	ng'	[teŋera]	kimbia
w	w	[batwa]	sakamwa

Konsonanti za Kigīchūgū zinaweza kuainishwa kwa kuzingatia namna ya kutamka na pahali pa kutamkia. Kwa kuzingatia namna ya kutamka, konsonanti za Kigīchūgū zinaweza kuainishwa katika makundi sita: vipasuo, vikwaruzo, ving'ong'o, nazali, kilainisho na viyeyusho. Aina hizi hujitenga katika makundi mawili makuu ambayo ni; vikwamizo na vifulizo. Pahali pa kutamkia pia huainishwa mara tano: midomoni, menoni, ufizini, kaakaagumu, kaakaalaini kama inavyojitokeza katika Jedwali 4.2. Hii ni kwa sababu, kulingana na Ruri (2011), Kigīchūgū hakina konsonanti /h/ ambayo hutamkiwa glotani kama ilivyo katika lahaja nyingine za Kikuyu.

Jedwali 4.2: Utamkaji wa Konsonanti za Kigīchūgū

Jinsi ya kutamka		Mahali pa kutamkia				
		midomo	meno	ufizi	kakaagumu	kaakaalaini
Vikwamizo	Vipasuo	β		t		k
	vikwaruzo		θ		š	γ
Vifulizo	Ving'ong'o	mb		nd	nj	ŋg
	Nazali	m		n	j	ŋ
kilainisho				r		
viyeyusho				j		w


Konsonanti za Kigīchūgū huwa na maumbo mawili: konsonanti zenyе umbo sahili na konsonanti zenyе umbo changamano. Konsonanti sahili huwakilishwa kwa herufi moja katika tahajia. Kwa mfano, /k/, /b/, /m/ na /r/ katika vitenzi

4. #baka#- ‘paka’

18. #inama#- ‘inama’

9. #būra#- ‘chapa’

Konsonanti sahili zinaweza kuonyeshwa katika mchoro kama ifuatavyo:




Kwa upande mwengine, konsonanti changamano huwakilisha mwambatano wa herufi za tahajia na hutamkwa kama sauti moja. Kwa mfano, /th/, /mb/, /ndw/. Mifano katika vitenzi ni kama vile;

41. #rūngwa# - ‘lainishwa’

48. #thambia# - ‘osha’

47. #thama# - ‘hama’

Konsonanti changamano zinaweza kuonyeshwa katika mchoro kama:



#### 4.2.2 Irabu za Kigīchūgū

Kwa mujibu wa Kihore, Massamba na Msanjila (2012), irabu ni aina ya sauti za lugha ambazo hutamkwa bila kuwepo na kizuizi chochote kwenye mkondo hewa utakao mapafuni ukipitia katika chemba cha kinywa na chemba cha pua kwenda nje. Kigīchūgū kina irabu saba ambazo ni: /a/, /e/, /ɛ/, /i/, /o/, /ɔ/ na /u/. Irabu hizi, kama

zilivyoonyeshwa kwenye Jedwali 4.3, zinatumika katika unyambulishaji wa vitenzi vya Kigīchūgū.

#### Jedwali 4.3: Irabu za Kigīchūgū

Fonimu	Tahajia	Maneno	Maana
a	a	andīka	andika
ɛ	e	theka	cheka
i	i	iga	weka
e	ī	rīra	lia
ɔ	o	thoma	soma
o	ū	cagūra	chagua
u	u	tua	chuna

Irabu hizi zinaweza kujitokeza katika mazingira yoyote katika vitenzi vya Kigīchūgū: mwanzoni, katikati na mwishoni. Irabu za Kigīchūgū zinaweza kuainishwa kwa kutegemea mkao wa ulimi katika chemba cha kinywa kama ilivyodhihirishwa katika Jedwali 4.4 lifuatalo:

#### Jedwali 4.4: Utamkaji wa Irabu za Kigīchūgū

Mwinuko wa ulimi	Ulalo wa ulimi		
	mbele	katikati	nyuma
juu	i		u
Kati-juu	e		o
Kati-chini	ɛ		ɔ
chini		a	


Irabu za Kigīchūgū pia zinaweza kuainishwa kwa kutegemea hali ya midomo: mviringo au tandaze. Irabu mviringo ni /o/, /ɔ/ na /u/ nazo irabu tandaze ni /a/, /e/, /i/ na /ɛ/. Kama ilivyo katika konsonanti, irabu za Kigīchūgū pia hudhihirisha maumbo matatu: irabu sahili, irabu ndefu na irabu changamano. Irabu sahili ni zile ambazo huwakilishwa kwa herufi moja. Kwa mfano, katika vitenzi:

52. #thoma# - ‘soma’

37. #ruga# - ‘pika’

34. #rīma# - ‘lima’.


Irabu hizi zinaweza kuonyeshwa katika mchoro kama;



Irabu ndefu ni mseto wa sauti mbili sahili zenyenye muundo sawa. Katika lugha ya Kigīchūgū, irabu pekee ndizo huwa na wakaa mrefu ambapo irabu moja inapotokea mahali pamoja kwa mfululizo. Kwa mujibu wa Mgullu (1999), wakati wa kutamka mfululizo wa irabu moja, mtamkaji huitamka irabu hiyo kwa kuivuta. Kwa mfano,

- |             |  |   |          |
|-------------|--|---|----------|
| 43. #taara# |  | — | ‘dondoa’ |
| 11. #ceera# |  | — | ‘tembea’ |
| 23. #kuua#  |  | — | ‘beba.’  |


Mifano hii ya irabu /aa/, /ee/ na /uu/ katika Kigīchūgū ni irabu ambazo zina wakaa mrefu. Kwa mujibu wa Mgullu (keshatajwa), wakaa ni jumla ya muda unaotumika kutamka sauti. Anaendelea kusema kuwa wakaa unaweza kuwa mfupi, kadri au mrefu. Irabu hizi zinaweza kuonyeshwa katika mchoro kama;



Irabu changamano ni mseto wa sauti mbili sahili zenyenye muundo tofauti. Kwa mfano katika vitenzi,

- |            |  |   |          |
|------------|--|---|----------|
| 53. #thūa# |  | — | ‘kuna’   |
| 29. #nyua# |  | — | ‘kunywa’ |
| 3. #aria#  |  | — | ‘ongea.’ |

Irabu hizi zinaweza kuonyeshwa katika mchoro kama ifuatavyo;



#### 4.3 Vitenzi vya Kigīchūgū

Vitenzi ni aina ya maneno yanayotoa taarifa juu ya tendo linalofanyika au linalotendwa na kiumbe au kitu (Kihore, Massamba na Msanjila, 2012). Kwa upande mwingine, Mgullu (1999) anaeleza vitenzi kama aina ya maneno ambayo hutumika kama sehemu muhimu ya kiarifu cha sentensi na huarifu au hueleza jambo fulani linalohusu kiima cha sentensi. Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa, vitenzi ni maneno ya pekee ambayo ni lazima yawepo katika sentensi ili sentensi iweze kukamilika na kueleweka. Hii ina maana kuwa katika Kigīchūgū, vitenzi ni vipashio vya lazima na haviwezi kudondoshwa katika mazingira yoyote yale.

Vitenzi vya Kigīchūgū ni vya aina mbili; elekezi na sielekezi. Vitenzi elekezi ni vile vinavyoundwa kutokana na mzizi fulani kuambatana na yambwa katika muundo wa tungo. Kwa mujibu wa Habwe na Karanja (2004), kitenzi elekezi ni kitenzi ambacho huhitaji kirai nomino cha mtendwa. Mifano katika Kigīchūgū ni kama vile;

1. a) Ng'ombe nřrarňa nyaki.-elekezi

Ng'ombe anakula nyasi.

- b) Wambui nřagüithia mwana.- elekezi

Wambui ameangusha mtoto.

Vitenzi sielekezi ni vile visivyokuwa na uwezo wa kuambatana na yambwa katika muundo wa tungo. Kwa mujibu wa Habwe na Karanja (keshatajwa), vitenzi sielekezi ni vitenzi ambavyo havihitaji kirai nomino cha mtendwa na huwa vimekamilika katika matumizi yake ya sentensi. Mifano katika Kigīchūgū ni kama vile;

2. a) Kamau nřarňka.-sielekezi

Kamau amemaliza.

b) Ÿbuku nřřrandikwa.-sielekezi

Kitabu kinaandikwa.

Vitenzi elekezi na sielekezi huathiriwa na unyambulishaji. Japokuwa dhana hizi ni za kimiundo zaidi, zina hali ambazo zinaathiri miandamano ya mizizi na viambishi nyambulishi. Kwa mfano, mizizi inayounda vitenzi elekezi inaweza kuandamana moja kwa moja na kiambishi nyambulishi chochote wakati mizizi inayounda vitenzi sielekezi huandamana moja kwa moja na baadhi tu ya viambishi nyambulishi.

#### **4.4 Unyambulishaji wa Vitenzi vya Kigīchūgū**

Unyambulishaji wa vitenzi ni utaratibu wa uundaji wa vitenzi vipyta katika lugha kwa kuongeza viambishi nyambulishi kwenye maumbo ya mzizi (Kihore, Massamba na Msanjila, 2012). Kwa mujibu wa Wesana- Chomi (2013), unyambulishaji ni mchakato au mfanyiko wa kuambatisha kiambishi kimoja au zaidi kwenye mzizi wa vitenzi ili kuunda vitenzi vingine. Ngowa (2008) anasema kuwa katika unyambulishaji wa vitenzi, viambishi tamati vinavyochopekwa katika vitenzi hufuata kanuni bayana itambulikayo kama uwiano wa vokali. Anaeleza kuwa kanuni hii ndio hudhibiti unyambulishaji wa vitenzi. Uwiano wa vokali ni kanuni ya kifonolojia ambayo inahusu utaratibu wa vokali fulani kukubali kuandamana katika mazingira maalum. Vitenzi vya Kigīchūgū kama ilivyojadiliwa katika sura ya kwanza, vina uwezo wa kuambishwa viambishi kwenye mzizi ili kudhihirisha maana tofauti. Uambishaji huu unadhihirika katika vitenzi kama vile un-īk-a, rathim-ith-i-a, bat-īr-a na rūng-w-a katika kiambatisho cha jedwali la mnyambuliko wa vitenzi, Vitenzi vya Kigīchūgū huruhusu uambishaji tamati katika vitenzi husika. Viambishi tamati ni mofimu ambazo hupachikwa baada ya mzizi wa vitenzi katika mfanyiko wa unyambulishaji.

Utafiti huu umeshughulikia unyambulishaji wa vitenzi vya Kigīchūgū kwa kujadili kauli sita za unyambulishaji: kutendea, kutendwa, kutendesha, kutendana, kutendeka na kutendua kwa kutilia maanani mifanyiko inayohusika katika unyambulishaji wa vitenzi. Katika kazi hii, nadharia ya mofolojia leksia (Kiparsky, 1982 & Katamba na Stonham, 1993) na Kanuni ya Kioo (Baker, 1985) zimetumiwa ili kueleza mfuatano wa vinyambulishi katika lugha ya Kigīchūgū na kutathmini kanuni zinazoruhusu na

kuzuia mifanyiko hiyo ya unyambulishaji. Vitenzi hivi vimewekwa katika kauli sita ili kudhihirisha kanuni na sheria zinazotawala mifanyiko ya unyambulishaji katika Kigīchūgū. Kauli hizi ni pamoja na:

#### **4.4.1 Kauli ya Kutendea (TDA)**


Kauli ya kutendea katika Kigīchūgū huweza kuwa na viambishi nyambulishi viwili kutegemea irabu zilizo kwenye mzizi wa kitenzi. Viambishi hivi ni kama vifuatavyo:

##### **a. Kinyambulishi { -īr- }**

Katika Kigīchūgū, kauli ya TDA huchukua mofimu {-īr-} kabla ya irabu ya mwisho kwenye vitenzi katika unyambulishaji. Mofimu hii hutumika iwapo mzizi wa kitenzi una irabu /a/, /i/, / ī /, / ū / au /u/. Kwa mfano,

	<b>Kitenzi</b>	<b>Maana</b>	<b>Kauli ya Kutendea</b>
46.	thak-a	cheza	thak-īr-a
6.	bing-a	funga	bing-īr-a
34.	rīm-a	lima	rim-īr-a
38.	rūg-a	ruka	rug-īr-a
8.	bur-a	panguza	bur-īr-a

Maelezo haya yanaweza kuainishwa kikamilifu kama ifuatavyo:




##### **b. Kinyambulishi {-er-}**


Katika Kigīchūgū, kinyambulishi {-er-} huchopekwa kwenye unyambulishaji wa vitenzi iwapo mzizi wa vitenzi una irabu /e/ na /o/. Kwa mfano,

<b>Kitenzi</b>	<b>maana</b>	<b>Kauli ya Kutendea</b>
52. thom-a	soma	thom- <b>er</b> -a
44. tem-a	kata	tem- <b>er</b> -a
7. boy-a	omba	bo- <b>er</b> -a

Katika mfano wa tatu, sauti /y/ imedondoshwa ili kuondoa mfuatano wa irabu tatu baada ya kuongeza kinyambulishi {-er-}, kwani sauti /y/ ina sifa za irabu ya kutamkwa kwa mfululizo bila hewa kuzuiliwa kwenye ala mbalimbali za kutamkia. Mfuatano wa irabu tatu haukulaliki katika Kig̊ichūgū. Maelezo haya yanaweza kuainishwa katika mchoro kama ifuatavyo:



Kupitia maelezo haya katika kauli ya TDA, viambishi {-i-} na {-e-} vimetumika katika unyambulishaji. Hata hivyo kiambishi {-r-} kimetumika pia ili kuhifadhi muundo wa Kig̊ichūgū wa Konsonanti-Vokali (K-V) kama inavyopendekezwa na Katamba na Stonham (1993) kwamba, baada ya mageuzi ya kifonolojia, muundo wa lugha mahususi sharti uhifadhiwe. Vilevile umbo la kitenzi katika kauli ya kutendea linaweza kuonyeshwa kwa kuzingatia kanuni ya ngazi leksia kama ilivyopendekezwa na Kiparsky (1982) na Katamba na Stonham (1993) katika nadharia ya mofolozia leksia. Umbo hilo ni kama vile,



Kielelezo hiki kinafasiliwa kuwa vitenzi vya Kig̊ichūgū katika kauli ya kutendea huundwa kwa muungano wa viambishi mbalimbai ambavyo havina maana vikiwa peke yavyo hadi vinapounganishwa kuunda kitenzi kinachojitosheleza kimaana. Kwa

upande mwingine, kama anavyosema Waithaka (2009), irabu ya mzizi katika kauli ya TDA hukubaliana na kiambishi nyambulishi kinachofuata. Hali hii ya ukubalifu anairejelea kama uwiano wa vokali. Kutokana na maelezo ya kauli ya TDA katika Kigīchūgū, inabainika kuwa iwapo mzizi wa kitenzi una irabu ya juu yaani /i/ na /u/, basi kinyambulishi cha kati-juu yaani /ɪ/ kilitumika. Vilevile, mzizi wenyewe irabu ya chini /a/, kinyambulishi cha kati-chini /e/ kilitumika.

#### **4.4.2 Kauli ya Kutendwa (TDW)**

Vitenzi katika Kigīchūgū, hupachikwa kiambishi {-w-} katika unyambulishaji ili kudhihirisha kauli ya utendwa. Kiambishi hiki hupachikwa baada ya mzizi wa vitenzi vinavyoishia kwa konsonanti. Kwa mfano,

	<b>Kitenzi</b>	<b>maana</b>	<b>Kauli ya Kutendwa</b>
24.	men-a	chukia	men-w-a
28.	nyit-a	shika	nyit-w-a
13.	cor-a	chora	cor-w-a
26.	mund-a	dunga	mund-w-a

Mifano iliyoonyeshwa hapo juu inadhihirisha kwamba irabu /u/ inayeyushwa na kuwa /w/ baada ya unyambulishaji. Kwa mfano,

/men-u-a/ → [men-w-a]  
 /nyit-u-a/ → [nyit-w-a]  
 /mund-u-a/ → [mund-w-a].

Hii ni kulingana na mhimili wa kwingineko katika nadharia ya ML, ambao unapendekeza kuwa, iwapo katika mofolojia irabu mbili zinafuatana na kushindania nafasi, uyeyushaji utumikizwe (Katamba na Stonham, 1993).

Kwa upande mwingine, baadhi ya vitenzi vya Kigīchūgū vinavyoishia kwa irabu /i/, hupachikwa kinyambulishi {-u-} katika kauli ya kutendwa. Kwa mfano,

	<b>Kitenzi</b>	<b>Maana</b>	<b>Kauli ya Kutendwa</b>	<b>Kitenzi baada ya udondoshai</b>	<b>Kitenzi baada ya uyeyushaji</b>
15.	giri-a	zuia	giri-u-a	gir-u-a	girwa
55.	tini-a	kata	tini-u-a	tin-u-a	tinwa
56.	tongori-a	ongoza	tongori-u-a	tongor-u-a	tongorwa
20.	kethi-a	salimu	kethi-u-a	keth-u-a	kethwa

Katika mifano hii ya vitenzi vya Kigīchūgū, irabu /i/ inadondoshwa na /u/ kuachwa kama kiambishi cha kauli ya kutendwa. Irabu hii inadondoshwa kwa sababu Kigīchūgū hakikubali mfuatano wa irabu tatu. Baada ya udondoshaji, irabu /u/ huyeyushwa na kuwa /w/. Hii ni kulingana na misingi ya Nadharia ya Mofolojia Leksia kanuni ya kwingineko. Kanuni hii ilitumikizwa pale ambapo sheria mbili huonekana kushindania nafasi moja. Hii inadhihirika ambapo irabu /i/ na /u/ zinatumika hivyo basi udondoshaji unatokea katika irabu /i/ na uyeyushaji katika irabu /u/.

#### **4.4.3 Kauli ya Kutendesha (TSH)**

Kauli ya kutendesha katika Kigīchūgū huonyeshwa kwa kiambishi {-ithi-} katika unyambulishaji wa vitenzi. Kwa mfano,

	<b>Kitenzi</b>	<b>Maana</b>	<b>Kauli ya Kutendesha</b>
1.	ak-a	jenga	ak- <b>ithi</b> -a
14.	end-a	penda	end- <b>ithi</b> -a
57.	tum-a	shona	tum- <b>ithi</b> -a
19.	ken-a	furahi	ken- <b>ithi</b> -a
33.	rīb-a	lipa	rīb- <b>ithi</b> -a

Vilevile, kauli ya kutendesha katika Kigīchūgū huonyeshwa kwa kiambishi {-i-} katika baadhi ya vitenzi ambavyo kisemantiki huonyesha anayesababisha kitendo kama mshiriki. Vitenzi hivi kwa kawaida ni vitenzi si elekezi. Kwa mfano,

	<b>Kitenzi</b>	<b>Maana</b>	<b>Kauli ya Kutendesha</b>
42.	rwar-a	ugua	rwar- <b>i</b> -a
17.	in-a	imba	in- <b>i</b> -a
45.	tet-a	teta	tet- <b>i</b> -a
27.	nor-a	nenepe	nor- <b>i</b> -a
50.	thek-a	cheka	thek- <b>i</b> -a

Kutokana na mifano iliyotolewa katika kauli ya TSH, kiambishi nyambulishi {-ithi-} hutumika katika vitenzi elekezi ilhali kiambishi nyambulishi {-i-} hutumika katika vitenzi vya Kigīchūgū ambavyo si elekezi. Hata hivyo wakati mwingine, kiambishi {-

ithi-} huweza kutumika na vitenzi si elekezi pia. Kiambishi {-ithi-} cha kauli ya TSH kinaonekana kuwa kizalishi kwa kiasi kikubwa kuliko kiambishi {-i-} ambacho kinatumika katika vitenzi vichache.

#### **4.4.4 Kauli ya Kutendana (TDN)**

Kauli ya kutendana katika Kigīchūgū huonyesha kuwa wahusika wawili au zaidi wanafanyiana kitendo kimoja. Kauli ya kutendana katika unyambulishaji wa baadhi ya vitenzi katika Kigīchūgū huonyeshwa kwa kiambishi {-an-} kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo.

	<b>Kitenzi</b>	<b>Maana</b>	<b>Kauli ya Kutendana</b>
9.	būr-a	chapa	būr-an-a
23.	kuu-a	beba	ku-an-a
38.	rūg-a	ruka	rūg-an-a
51.	thik-a	zika	thik-an-a
44.	tem-a	kata	tem-an-a

#### **4.4.5 Kauli ya Kutendeka (TDK)**


Kama ilivyoelezwa katika kauli ya kutendea katika sehemu ya 4.4.1, kauli ya kutendeka pia huweza kuwa na viambishi nyambulishi viwili kama ifuatavyo;

##### **a. Kinyambulishi {-ek-}**

Kinyambulishi {-ek-} katika unyambulishaji wa vitenzi vya Kigīchūgū huchopekwa kabla ya kiambishi tamati iwapo mzizi wa vitenzi hivyo una irabu /o/ na /e/. Kwa mfano,

	<b>Kitenzi</b>	<b>Maana</b>	<b>Kauli ya Kutendeka</b>
21.	kom-a	lala	kom-ek-a
31.	oc-a	chukua	oc-ek-a
24.	men-a	chukia	men-ek-a
25.	meny-a	fahamu	meny-ek-a

Maelezo haya yanaweza kusawiriwa kwenye mchoro kama ifuatavyo;




### b. Kinyambulishi {-īk-}

Vitenzi katika Kigīchūgū huchopekwa kiambishi {-īk-} kabla ya kiambishi tamati katika unyambulishaji iwapo mzizi wa vitenzi hivyo una irabu /a/, /i/, /ī/, /ū/ na /u/. Kwa mfano,

	<b>Kitenzi</b>	<b>Maana</b>	<b>Kauli ya Kutendeka</b>
47.	tham-a	hama	tham-īk-a
28.	nyit-a	shika	nyit-īk-a
35.	rīr-a	lia	rīr-īk-a
22.	kūnj-a	kunja	kūnj-īk-a
59.	ug-a	sema	ug-īk-a

Maelezo haya yanaweza kuwakilishwa katika mchoro kama ifuatavyo;



Kama ilivyo katika kauli ya kutenda, kiambishi {-e-} na {-ī-} vimetumika katika unyambulishaji. Hata hivyo, kiambishi {-k-} pia kimetumiwa ili kuhifadhi muundo wa Kigīchūgū wa Konsonanti-Vokali.

#### 4.4.6 Kauli ya Kutendua (TDU)

Vitenzi katika kauli ya kutendua katika Kigīchūgū hutoa maana iliyo kinyume cha kitenzi katika kauli ya kutenda. Viambishi vyta unyambulishaji katika kauli ya kutendua katika Kigīchūgū ni {-ūr-} na {-or-}. Mofimu {-ūr-} hupachikwa kwenye

vitenzi vyenye mzizi wenyewe irabu /a/, /i/, /u/ na /ü/ ilhali {-or-} hupachikwa kwenye vitenzi vyenye mzizi wenyewe irabu /o/. Kwa mfano,

	<b>Kitenzi</b>	<b>Maana</b>	<b>Kauli ya Kutendua</b>
6.	bing-a	funga	bing- <b>ūr</b> -a
1.	ak-a	jenga	ak- <b>ūr</b> -a
57.	tum-a	shona	tum- <b>ūr</b> -a
51.	thik-a	zika	thik- <b>ūr</b> -i-a
22.	kunj-a	kunja	kunj- <b>ūr</b> -a
30.	ob-a	funga (kwa mfano kamba)	ob- <b>or</b> -a
36.	rog-a	roga	rog- <b>or</b> -a

Ingawa vitenzi vya Kigīchūgū katika kauli ya kutendua huonyesha kinyume, ni muhimu pia kutambua kuwa vitenzi hivi vinaweza kunyambulishwa zaidi katika kauli zingine. Kwa mfano,

	<b>tendua</b>	<b>tendea</b>	<b>tendwa</b>	<b>tendesha</b>	<b>tendeka</b>
22.	kunjūra	kunjūrīra	kunjūrwa	kunjūrithia	kunjūka
30.	obora	oborera	oborwa	oborithia	oboka

#### **4.5 Mfuatano wa Viambishi Nyambulishi katika Kigīchūgū**

Unyambulishaji katika vitenzi vya Kigīchūgū huweza kuchukua mwambatano wa viambishi vingi vya unyambulishaji kwa wakati mmoja. Kama wanavyosema Kihore, Massamba na Msanjila (2012:127), viambishi nyambulishi huandamana na mizizi hatua kwa hatua. Hii ina maana kuwa kiambishi huandama kiambishi nyambulishi na kingine au vingine kufanya vivyo hivyo. Wanasema kuwa vitenzi vya Kiswahili vinaweza kufikia hadi hatua nne za unyambulishaji.

Kwa mujibu wa Wesana-Chomi (2013), kitenzi kimoja kinaweza kuchukua vinyambulishi viwili au zaidi. Hata hivyo, anaeleza kuwa vinyambulishi hivi havitokei ovyo bali huongozwa na kanuni mbalimbali ambazo zinahusika katika unyambulishaji huo.

Hyman (2003) anasema kuwa mizizi ya vitenzi katika lugha za Kibantu huweza kuchukua viambishi nyambulishi mbalimbali ili kuwakilisha maana tofauti. Hyman

(keshatajwa) anapendekeza mfuatano wa CARP yaani C- causative (usababishi), A- Applicative (utendea), R- Reciprocal (utendano) na P- Passive (utendwa) ambao hutambua hatua nne za unyambulishaji katika lugha za Kibantu. Kazi hii ilifafanua mifuatano ya mofimu nyambulishi katika Kigīchūgū ili kubaini iwapo inaaafiki au kukiuka ule mfuatano uliopendekezwa na Hyman (keshatajwa).

Kigīchūgū kama lugha zingine za Kibantu hufuata mwambatano wa viambishi vinyambulishi viwili au zaidi. Mifano iliyojadiliwa katika kauli sita za unyambulishaji, inahusu hatua ya kwanza ya viambishi nyambulishi vya Kigīchūgū vinavyofuata mizizi moja kwa moja. Mifano inayofuata imezingatia unyambulishaji wa vitenzi vya Kigīchūgū katika hatua ya pili, ya tatu na ya nne.

#### **4.5.1 Mfuatano wa Viambishi Nyambulishi Viwili**

Kama anavyopendekeza Waweru (2011) kuhusu mifuatano nyambulishi katika Gīkūyū, Kigīchūgū pia kinaweza kubali mifuatano ya viambishi nyambulishi viwili vifikavyo kumi na moja. Mifuatano hii ni pamoja na;

##### **a. Kauli ya Kutendea na Kutendwa (TDA+TDW)**

Mofimu zinazowakilisha kauli ya kutendea katika Kigīchūgū ni {-īr-} na {-er-} na kauli ya kutendwa ni {-w-}. Mifano ifuatayo inaonyesha kuwa Kigīchūgū hukubali mfuatano huu kama ilivyo katika lugha nyingine za Kibantu. Kwa mfano,

2. andik -īr -w -a

andik -TDA -TDW -I

andikiwa

24. men -er -w -a

men -TDA -TDW -I

chukiwa

30. ob -er -w -a

ob -TDA -TDW -I

fungiwa

4. bak- ūr- w- a  
bak-TDA-TDW-I  
pakiwa

Mfuatano huu katika Kigīchūgū unakubaliana na mfuatano wa Kiolezo kama anavyourejelea Asiimwe (2011) jinsi ulivyopendekezwa na Hyman (2003) yaani kauli ya kutenda hutangulia kauli ya kutendwa. Hii ina maana kuwa mofimu katika kauli ya kutenda hufanganishwa kwenye mzizi kwanza ikifuatwa na mofimu katika kauli ya kutendwa. Mfuatano huu katika Kigīchūgū ilitumiwa kuonyeha kuwa kitendo fulani kilifanywa kwa niaba ya mtu au kitu.

**b. Kauli ya Kutenda na kauli ya Kutendua (TDA+TDU)**

Kigīchūgū huambikwa mofimu {-ūr-} na {-er-} katika kauli ya kutenda na mofimu {-ūr-} na {-or-} katika kauli ya kutendua. Mofimu hizi huweza kufuatana katika Kigīchūgū ingawa mfuatano hukiuka uliopendekezwa na Hyman (2003). Hii ni kwa sababu Hyman (mtaje) alipendekeza mfuatano wa utenda kuja kabla kutendua lakini mfuatano huu katika Kigīchūgū huanza kwa kauli ya kutendua ikifuatwa na kauli ya kutenda. Kwa mfano,

30. ob –or –er -a  
ob –TDU –TDA -I  
fungulia

5. bat –ūr -ūr -a  
bat –TDU –TDA -I  
kwamulia

58. tum –ūr -ūr -a  
tum –TDU –TDA -I  
shonolea

22. kūnj- ūr- ūr- a  
kūnj- TDU- TDA- I  
kunjulia

Kutokana na mifano hii, ni dhahiri kwamba Kigīchūgū hukubali mfuatano wa kauli ya kutendea na kutendua. Kimantiki, kauli ya kutendua katika Kigīchūgū hutokea kabla ya kauli ya kutendea. Hali hii inaafiki Kanuni ya Kioo inayodai kwamba mpangilio wa mofimu katika lugha mbalimbali unafaa kuakisi miundo kisemantiki. Katika Kigīchūgū, iwapo kauli y TDA ingetokea kabla ya TDU basi vitenzi hivi havingekuwa na maana.

**c. Kauli ya Kutendesa na Kutendea (TSH+TDA)**

Mfuatano huu huchukua mofimu {-ithi-} na {-i-} katika kauli ya kutendesa katika Kigīchūgū na mofimu {-īr-} katika kauli ya kutendea. Kwa mfano,

14. end –ith –īr –I –a

end –TSH –TDA –tsh –I

pendezea

34. rīm –ith –īr –I –a

rīm – TSH – TDA – tsh-I

lim-ish-i-a

9. būr –ith –īr –I –a

būr –TSH –TDA –tsh –I

pigishia

13. cor- ith- īr- i- a

cor-TSH- TDA- tsh- I

choreshea

Katika mifano iliyotolewa, mofimu nyambulishi katika TSH inatengwa na mofimu ya TDA. Hii ni kwa sababu TSH huishia kwa irabu na vilevile kauli ya TDA huanza kwa irabu, hivyo kuhifadhi muundo wa KV katika Kigīchūgū baada ya kupitia mageuzi ya kifonolojia na kimofolojia.

Kigīchūgū pia huwa na usababishi mfupi ambao huwakilishwa na mofimu {-i-}. Katika mfuatano huu kauli ya kutendea hutokea kabla ya kauli ya kutendesha kinyume na uliopendekezwa na Hyman (2003). Kwa mfano,

21. kom -er -I -a

kom -TDA -TSH -I

lalishia

60. unan -īr -I -a

unan -TDA -TSH -I

vunjishia

48. thamb- īr- i- a

thamb- TDA – TSH- I

safishia

55. tin- īr- i- a

tin-TDA- TSH- I

katishia

#### d. **Kauli ya Kutendea na Kutendana (TDA+ TDN)**

Katika Kigīchūgū, mofimu za TDA ni {-īr-} na {-er-} na mofimu za TDN ni {-an-}. Kama anavyoeleza Waweru (2011), lugha ya Gikuyu hukubali mfuatano wa TDA na TDN ingawa mfuatano huu hukiuka ule uliopendekezwa na Hyman (mtaje). Katika Kigīchūgū, maumbo haya hujitokeza kama ifuatavyo;

44. tem -an -īr -a

tem -TDN -TDA -I

katiana

16. gūr -an -īr -a

gur -TDN -TDA -I

nunuliana

38. rug –an –ĩr -a  
rūg –TDN –TDA -I  
pikiana

46. thak- an- ĩr- a  
thak- TDN- TDA- I  
chezeana

Kauli ya kutendana huja kabla ya kauli ya kutenda katika Kigīchūgū. Kulingana na mfumo wa Hyman (2003), ingetarajiwa kuwa kauli ya kutenda ingetokea kabla ya kauli ya kutendana. Hii haiwezekani kwa kuwa kisemantiki vitenzi hivi havingeleta maana iliyokusudiwa ya kuonyesha kuwa watu fulani wametendeana kitendo kile kimoja. Mfuatano huu katika Kigīchūgū unadhihirisha kuwa mofimu moja pekee {-ĩr-} ya utenda ndiyo hutumiwa.

#### e. **Kauli ya Kutendesa na Kutendwa (TSH+ TDW)**

Kauli ya TSH na TDW huwakilishwa kwa mofimu {-ith-} na {-w-} katika Kigīchūgū. Kama ilivyobainika katika sehemu ya 4.4.2, irabu /u/ ambayo ndio umbo la ndani katika kauli TDW huyeyushwa na kuwa /w/. Hata hivyo, ilibainika kwamba irabu /u/ hutumiwa kama kinyambulishaji cha TDW katika vitenzi ambavyo mizizi yake huishia kwa irabu /i/. Mfuatano wa TSH na TDW katika Kigīchūgū ulionyeshwa ifuatavyo;

52. thom –ith -w -a  
thom –TSH –TDW -I  
someshwa

32. rathim –ith –w -a  
rathim –TSH –TDW -I  
barikishwa

39. rūgam –ith –w -a  
rūgam -TSH –TDW -I  
simamishwa

Mfuatano huu wa TSH na TDW unaaafiki uliopendekezwa na Hyman (2003) kimofolojia na kisemantiki. Kulingana na Baker (1985) katika Kanuni ya Kioo inayoongoza mfuatano wa mofimu za unyambulishaji, mofu ya TSH na TDW zitokezapo katika mzizi, ni lazima TSH ijitokeze karibu na mzizi kisha ifuatwe na TDW. Mifano iliyotolewa katika Kigīchūgū inadhibitisha hali hiyo.

**f. Kauli ya Kutendesa na Kutendua (TSH+ TDU)**

Mofimu nyambulishi za kutendesa na kutendua katika Kigīchūgū ni {-ith-} na {-ūr-} au {-or-}. Kisemantiki na kimofolojia, kauli ya kutendua huja kabla ya kauli ya kutendesa katika vitenzi vya Kigīchūgū. Kwa mfano,

6. bing –ūr –ithi -a

bing -TDU -TSH -I

fungulisha (mlango)

30. ob –or –ithi -a

ob –TDU -TSH -I

fungulisha (kamba)

36. rog -or –ithi - a

rog –TDU -TSH -I

rogoesha

22. kūnj- ūr- ithi- a

kūnj- TDU- TSH- I

kunjulisha

Katika mifano hii, mfuatano uliopendekezwa na Hyman (keshatajwa) wa kauli TSH kuja kabla ya kauli TDU umekiukwa ili kudumisha maana. Katika vitenzi vya Kigīchūgū, kauli ya TSH haiwezi kutangulia kauli ya TDA lakini upeo hubadilika kulingana na lugha husika.

**g. Kauli ya Kutendesa na Kutendana (TSH+ TDN)**

Mfuatano wa kauli tendeshi na tendana hukubalika katika Kigīchūgū. Mofimu {-ithi-} na {-i-} hutumiwa katika TSH na mofimu {-an-} katika TDN. Kwa mfano,

1. ak –ith –an –i -a

ak –TSH –TDN –tsh -I

jengeshana

29. nyu –ith –an –i -a

nyu –TSH –TDN –tsh -I

nyweshana

28. nyit –ith –an –i -a

nyit –TSH –TDN –tsh -I

shikishana

33. rīb- ith- an- i – a

rīb- TSH- TDN- tsh- I

lipishana

Kutokana na mifano hii, ni dhahiri kwamba Kigīchūgū hukubali mfuatano wa TSH na TDN. Mfuatano wa mofimu hizi katika Kigīchūgū unakubaliana na kanuni ya Kiolezo kuwa kauli tendeshi hutangulia kauli tendana kama unavyopendekezwa na Good (2005). Itokeapo hivi, kauli hii huonyesha kuwa kuna wahusika wawili wanaoshirikiana kukitenda kitendo kile kimoja.

**h. Kauli ya Kutendua na Kutendwa (TDU+ TDW)**

Kauli ya TDU na TDW huwakilishwa na mofimu nyambulishi {-ūr-} au {- or-} katika kauli ya kutendua na {-w-} katika kauli ya kutendwa katika Kigīchūgū. Mifano hii inadhihirisha mfuatano huo.

22. kūnj –ūr –w -a

kūnj –TDU -TDW -I

kunjuliwa

6. bing -ür -w -a  
bing -TDU -TDW -I  
funguliwa

30. ob -or -w -a  
ob -TDU -TDW -I  
funguliwa

1. ak- ūr- w - a  
ak- TDU- TDW- I  
jenguliwa

Kutokana na mifano hii, kauli ya kutendwa huja baada ya kutendua katika unyambulishaji wa vitenzi vya Kigīchūgū. Hata hivyo, mfuatano huu wa TDU na TDW haukulaliki katika baadhi ya vitenzi, kwani kauli ya TDU hutokea katika vitenzi vichache katika Kigīchūgū. Katika mifano hii, mhimili wa kwingineko kulingana na nadharia ya M.L iliyoasisiwa na wa Kiparsky (1922) na kuendelezwa na Katamba na Stonham (1993) umetumikizwa. Hii ni kwa sababu, baada ya unyambulishajiwa vitenzi katika kauli ya TDW katika vitenzi vya Kigīchūgū, irabu /u/ hutumiwa. Kwa vile Kigīchūgū hukubali mfuatano wa K-V, irabu /u/ huyeyushwa na kuwa /w/ ili kuepuwa mfuatano wa irabu mbili.

**i. Kauli ya Kutendua na Kutendana (TDU+TDN)**

Kigīchūgū, huruhusu mfuatano wa kauli ya TDU ambayo mofimu zake ni {-or-} na {-ür-} na kauli ya TDN ambayo huwakilishwa na mofimu {-an-}. Katika mfuatano huu, kauli ya TDU huja kabla ya TDN. Mofimu hizi yaani {-or-} na {-an-} hujitokeza zikifuata vitenzi sielekezi katika Kigīchūgū kama inavyodhahirika katika mifano ifuatayo;

30. ob -or -an -a  
ob -TDU -TDN -I  
funguana

36. rog –or –an -a  
tog –TDU –TDN -I

rogoana

51. thik –ür –an -a  
thik –TDU –TDN -I  
zikuana

57. tum- ūr- an- a  
tum- TDU- TDN- I  
shonoana

#### j. Kauli ya kutendua na kutendeka

Mofimu nyambulishi katika kauli ya TDK na TDU ni {-īk-} au {-ek-} na {-or-} au{-ür-}. Katika mfuatano wa vinyambulishi hivi katika Kigīchūgū, kauli ya TDU huja kabla ya TDK kama inavyoonyeshwa kwenye mifano ifuatayo;

30. ob-or-ek-a  
ob-TDU-TDK-I  
funguka

36. rog-or-ek-a  
rog-TDU-TDK-I  
rogoka

57. tum- ūr- īk- a  
tum – TDU- TDK- I  
shonoka

1. ak- ūr- īk- a  
ak- TDU- TDK- I  
jenguka

**k. Kauli ya kutendesha na kutendeka**

Kauli ya TSH huwakilishwa kwa viambishi {-ithi-} na kauli ya TDK huwakilishwa kwa viambishi {-ik-} au {-ek-}. Katika mfuatano wa vinyambulishi katika lugha ya Kigīchūgū, kauli ya TSH hupachikwa kwanza ikifuatwa na kauli ya TDK. Kwa mfanano,

34. rīm-ith-ik-i-a

rīm-TSH-TDK-I

limishika

52. thom-ith-ik-i-a

thom-TSH-TDK-I

somesheka

41. rūng- ith- ik- i-a

rūng- TSH- TDK-tsh- I

lainishika

14. end-ith – ik – i- a

end- TSH- TDK-tsh- I

pendesheka

Katika Kigīchūgū, kauli ya TDK haifuatani na kauli nyingine kwa urahisi isipokuwa kauli ya TDU na TSH. Hii ni kwa sababu kama anavyooleza Asiimwe (2011), kauli ya TDK huwa inalenga kuondoa mtenda kwa hivyo haiwezi kuandamana na mofimu nyingine kwa sababu mazingira huwa hayaruhusu.

**4.5.2 Mfuatano wa Viambishi Nyambulishi Vitatu**

Kigīchūgū vilevile hukubali mfuatano wa kauli tatu katika kitenzi kimoja kwa wakati mmoja. Mfuatano huu ulielezwa kama ifuatavyo;

**a. Kauli ya Kutendesha, Kutenda na Kutendana (TSH+TDA+TDN)**

Katika mfuatano wa kauli tatu, Kigīchūgū kinakubaliana na pendekezo la Hyman (2003) la TSH, TDA na TDN. Hata hivyo, mfuatano wa viambishi nyambulishi vitatu katika Kigīchūgū unapingana na wa Hyman (kehatajwa) kwa kiasi kwa vile

unaruhusu mpishano. Tokeo la mfuatano huu katika Kigīchūgū unakuwa TSH, TDN na TDA hivyo basi kuathiri maana ya kitenzi kama ilivyo katika mifano ifuatayo.

47. tham –ith –an –īr –i -a

tham –TSH –TDN –TDA –tsh -I

hamishiana

43. taar –ith –an –īr –i -I

taar –TSH –TDN –TDA –tsh -I

chagulishiana

24. men –ith –an –īr –i -a

men –TSH –TDN –TDA –tsh -I

chukishiana

56. tongor- ith –an- īr- i- a

tongor- TSH- TDN- TDA-tsh-I

ongozesheana

Kanuni ya utokeaji ya mfuatano huu ni kwamba TSH inajitokeza baada ya mzizi wa kitenzi ikifuatwa na TDN na baadaye TDA.

**b. Kauli ya Kutendesha, Kutendana na Kutendwa (TSH+ TDN+ TDW)**

Kauli ya TSH, TDN na TDW zinaweza kufuatana kama Waweru (2011) anavyopendekeza. Katika mifano ifuatayo ya Kigīchūgū, pendekezo la mfuatano wa Hyman (2003) limeafikiwa. Hii ina maana kwamba kimofolojia kauli ya TSH huja baada ya mzizi, ikifuatwa na TDN kisha TDW ambayo huja mwishoni mwa kitenzi. Kwa mfano,

24. men –ith –an –w -a

men –TSH –TDN –TDW -I

kosanishwa

9. būr –ith –an –w -a

būr –TSH –TDN –TDW -I

piganishwa

2. andīk –ith –an –w -a  
andīk –TSH –TDN –TDW -I  
andikanishwa

30. ob- ith- an- w- a  
ob-TSH-TDN-TDW-I  
funganishwa

c. **Kauli ya Kutendesha, Kutendua na Kutendana (TSH+ TDU+ TDN)**  
Kigīchūgū hutumia mofimu nyambulishi {-ithi-} kuwakilisha kauli tendeshi, mofimu {-ūr-} na {-or-} katika kauli ya kutendua na mofimu {-an-} katika kauli ya kutendana. Mfuatano huu ni ule uliopendekezwa na Hyman (keshatajwa) ingawa kimofolojia Kigīchūgū kinaruhusu mpishano huru. Matokeo ya mfuatano huu kimofolojia katika Kigīchūgū ni kwamba kauli ya TDU huja baada ya mzizi wa kitenzi, ikifuatwa na kauli TSH na baadaye kauli ya TDN kama inavyodhihirika katika mifano.

30. ob –or –ith –an –i -a  
ob –TDU -TSH –TDN –tsh -I  
fungulishana

51. thik –ūr –ith –an –i -a  
thik –TDU –TSH -TDN -tsh-I  
zikulishana

22. kunj -ūr –ith –an –i -a  
kunj –TDU –TSH –TDN –tsh –I  
kunjulishana

1. ak- ūr- ith- an- i- a  
ak- TDU- TSH- TDN-tsh-I  
jengulishana

**d. Kauli ya Kutendesha, Kutendea na Kutendwa (TSH+ TDA+TDW)**

Kimofolojia, mfuatano wa kauli hizi ni TSH, TDA na TDW kama tu ilivyobainika katika Kigīchūgū. Kauli hizi huwakilishwa na mofimu tofauti kama ilivyoelezewa katika sehemu ya 4.4. Mofimu hizi ni {-ithi-}, {-īr-} au {-er-} na {-w-} ambayo muundo wake wa ndani ni {-u-} lakini hupitia uyeyushaji ili kuzuia mfuatano wa irabu mbili. Mfuatano huu katika Kigīchūgū ulionyeshwa kwa mifano ifuatayo;

1. ak –ith –īr –w -a

ak –TSH –TDA –TDW -I

jengeshewa

12. coker –ith –īr –w -a

coker –TSH –TDA –TDW -I

rudishiliwa

22. kūnj –ith –īr –w -a

kunj –TSH –TDA –TDW -I

kunjishiwa

7. bo –ith- īr- w- a

bo –TSH- TDA- TDW- I

ombeshewa

**e. Kauli ya Kutendesha, Kutendua na Kutendwa (TSH+ TDU+ TDW)**

Mfuatano huu unakubalika katika Kigīchūgū ingawa sio katika vitenzi vyote. Mfuatano huu huwa na mofimu ya TSH {-ith-}, TDU {-or-} au {-ūr-} na TDW{-w-}. Mfuatano wa kimofolojia kama unavyodhihirishwa na mifano ya vitenzi katika Kigīchūgū ni kwamba kauli ya TDU hupachikwa kwanza baada ya mzizi, ikifuatwa na kauli ya TSH na baadaye kauli ya TDW. Kwa mfano,

6. bing –ūr –ith -w -a

bing –TDU –TSH –TDW -I

fungulishwa

22. kūnj -ūr -ith -w -a  
kūnj -TDU -TSH -TDW -I  
kunjulishwa

51. thik -ūr -ith -w -a  
thik -TDU -TSH -TDW -I  
\*zikulishwa

1. ak- ūr-ith-w-a  
ak-TDU- TSH- TDW-I  
jengulishwa

Mfuatano huu umekiuka uliopendekezwa na Hyman (2003) ili kudumisha maana katika Kigīchūgū. Vilevile Kanuni ya kwingineko kama inavyopendekezwa na Kiparsky (1982 katika nadharia ya ML imetumikizwa. Hii inadhihirika ambapo irabu /u/ ambayo ingefuata mofimu {-ith-} katika mfuatano wa viambishi, inayeyushwa na kuwa /w/ ili kuepuka mfuatano wa irabu mbili na kuhifadhi muundo wa K-V kama inavyopendekezwa katika Kigīchūgū.

**f. Kauli ya Kutendesha, Kutendua na Kutendea (TSH+ TDU+ TDA)**

Kigīchūgū hukubali mfuatano wa kauli ya TSH, TDU na TDA. Utaratibu wa mfuatano huu katika Kigīchūgū ni kwamba kauli ya TDU hujitokeza kwanza ambapo hupachikwa baada ya mzizi, ikifuatwa na kauli TSH na baadaye TDA. Mifano ifuatayo inadhihirisha mfuatano huo katika Kigīchūgū.

6. bing -ūr -ith -īr -i -a  
bing -TDU -TSH -TDA -I  
fungulishia

22. kūnj -ūr -ith -īr -i -a  
kūnj -TDU -TSH -TDA -I  
kunjulishia

30. ob –or –ith –ĩr –i -a  
ob –TDU –TSH –TDA -I  
fungulishia

51. thik –ũr –ith –ĩr –i -a  
thik –TDU –TSH – TDA -I  
zikulia

**g. Kauli ya Kutendua, Kutendea na Kutendwa (TDU+ TDA+TDW)**

Katika unyambulishaji wa vitenzi vyta Kigĩchūgū, mfuatano huu hukubalika ambapo TDU hufuata moja kwa moja mzizi wa vitenzi. TDA hufuata TDU kwani huonyesha yambwa tendewa na baadaye TDW kama ilivyoonyeshwa katika mifano hii:

6. bing –ũr –ĩr –w -a  
bing –TDU –TDA –TDW -I  
funguliwa (mlango)

30. ob –or –er –w -a  
ob –TDU –TDA –TDW -I  
funguliwa (kamba)

57. tum –ũr –ĩr –w -a  
tum –TDU –TDA –TDW -I  
shonolewa

22. kũnj –ũr –ĩr –w -a  
kunj –TDU –TDA –TDW -I  
kunjuliwa

**h. Kauli ya Kutendea, Kutendana na Kutendwa (TDA+ TDN+TDW)**

Kigĩchūgū hukubali mfuatano wa kauli TDA ambayo huwakilishwa kwa mofimu nyambulishi {-ĩr-} na {-er-}, kauli TDN ambayo mofimu yake ni{-an-} na kauli TDW ambayo huwakilishwa kwa mofimu {-w-}. Ingawa mfuatano huu ni kama ulivyopendekezwa na Hyman (2003), Kigĩchūgū kimeruhusu mpishano ambapo kauli

ya TDN hufuata mzizi moja kwa moja, ikifuatwa na TDA na kisha TDW. Mfuatano huo umeonekana katika vitenzi kama ifuatavyo:

9. būr –an –īr –w -a

bur –TDN –TDA –TDW -I

piganiwa

2. andīk-an-īr-w-a

andīk –TDN –TDA –TDW -I

andikaniwa

40. rum –an –īr –w –a

rum –TDN –TDA –TDW –I

tusianiwa

23. kuw- an- īr- w- a

kuw- TDN- TDA-TDW- I

bebaniwa

**i. Kauli ya Kutendua, Kutenda na Kutendana (TDU+ TDA+ TDN)**

Mfuatano huu huwa na mofimu ya TDU {-ūr-} au {-or-}, TDA {-īr-} au {-er-} na TDN {-an-}. Mofimu hizi huambishwa kwenye mzizi wa vitenzi vya Kigīchūgū kwa mfuatano wa TDU –TDN -TDA. Mfuatano huu unakubalika katika Kigīchūgū ingawa sio katika vitenzi vyote kwani kauli ya TDU ambayo huonyesha kinyume cha kauli ya kutenda haijitokezi katika vitenzi vingi. Mifano ifuatayo inaonyesha mfuatano huo.

1. ak –ūr –an –īr -a

ak –TDU –TDN –TDA -I

jenguliana

36. rog –or –an –īr -a

rog –TDU –TDN –TDA -I

rogoleana

57. tum –ūr –an –īr -a  
tum –TDU –TDN –TDA -I  
shonoleana

6. bing –ūr –an –īr -a  
bing –TDU –TDN –TDA -I  
funguliana

#### **4.5.3 Mfuatano wa Viambishi Nyambulishi Vinne**

Kigīchūgū ni mojawapo ya lugha za Kibantu zinazokubali mfuatano wa kauli nne. Kauli hizi ni kama vile;

##### **a. Kauli ya Kutendesha, Kutendana, Kutendea na Kutendwa (TSH+ TDN+ TDA+ TDW)**

Mfuatano wa vinyambulishi hivi katika Kigīchūgū ni TSH –TDN -TDA-TDW. Mfuatano huu ni kinyume na uliopendekezwa na Hyman (2003) na Good (2005) wa TSH –TDA -TDN na TDW. Mpishano katika Kigīchūgū umetokea ili kuleta kuhifadhi maana ya vitenzi. Mifano ifuatayo inadhihirisha hilo:

24. men –ith –an –īr –w -a  
men –TSH –TDN –TDA –TDW -I  
koseshanwa

9. būr –ith -an –īr –w -a  
būr –TSH –TDN –TDA –TDW -I  
pigishianwa

2. andīk -ith -an –īr –w -a  
andīk –TSH –TDN –TDA –TDW –I  
andikishianwa

48. thamb-ith-an-īr-w-a  
thamb-TSH- TDN- TDA-TDW-I  
safishianwa

Katika mifano hii, mofimu {-u-} ambayo huwa ni mofimu ya ndani katika kauli ya TDW imepitia uyeyushaji na kuwa {-w-} kwa vile imefuatana na irabu. Mifano hii husababisha kitensi kuonekana kama vitenzi viwili vinavyokwenda sambamba hasa ikitumiwa katika sentensi. Kwa mfano,

3. a) Mwana wa Kamau **nīandīkithanīrwa** nī Njoroge na Muthoni makīandīkana.
- b) Mwana wa Kamau Nf- andīk- TSH- TDN- TDA- TDW-I nī Njoroge na Muthoni makīandīkana
- c) Mtoto wa Kamau **ameandikishianwa** na Njoroge na Muthoni wakati wanapoandikana.

Katika sentensi hii, inaonekana kuwa Njoroge na Muthoni wanaandikana lakini wakati huohuo wanafanya kazi ya kumwandika mtoto wa Kamau.

**b. Kauli ya Kutendua, Kutendesha, Kutendea na Kutendwa (TDU+ TSH+ TDA + TDW)**

Kigīchūgū vilevile hukubali mfuatano wa kauli ya TDU –TSH -TDA na TDW kama inavyoonyeshwa katika mifano hii:

30. ob –or –ith –īr –w -a  
ob –TDU -TSH –TDA –TDW -I  
funguanishiwa ( kamba)
22. kūnj –ūr –ith –īr –w -a  
kūnj –TDU –TSH –TDA –TDW -I  
funguanishiwa
1. ak –ūr –ith –īr –w -a  
ak –TDU –TSH –TDA –TDW -I  
jengulishiwa
57. tum- ūr- ith-īr –w- a  
tum- TDU- TSH- TDA- TDW-I  
shonoleshewa

Mifano hii inadhihirisha wazi kuwa kauli mbalimbali zinaweza kufungamanishwa katika kitenzi kimoja na kuleta athari kisemantiki.

#### **4.6 Kanuni za Mfuatano wa Viambishi Nyambulishi**

Mfuatano wa viambishi nyambulishi kama wanavyosema Kihore, Massamba na Msanjila (2012) huongozwa na kanuni mbalimbali. Kanuni hizi ni kama vile:

##### **4.6.1 Kanuni ya Kiambishi Nyambulishi {-w-}**

Kama wanavyosema Kihore, Massamba na Msanjila (2012: 129), katika miandamano yoyote ya viambishi nyambulishi na mzizi wa vitenzi, kiambishi nyambulishi {-w-} lazima kitokee kama kiambishi nyambulishi cha mwisho pale inapobidi kitokee katika umbo la kitenzi. Hali hii ni sawa katika Kigīchūgū ambapo ilibainika kuwa kauli ya TDW ilitokea mwishoni mwa vitenzi katika mifuatano iliyojadiliwa. Kwa mfano,

2. andīk-īr-w-a —— andikiwa

54. tig-ith-an-w-a —— achanishwa

49. thar-ith-an-īr-w-a —— bomoleshewa

Mifano hii inaonyesha mifuatano wa kauli mbili, tatu na nne na katika mifuatano yote, kiambishi nyambulishi {-w-} kimetokea mwishoni mwa vitenzi.

##### **4.6.2 Kanuni ya Viambishi Nyambulishi {-īr-} na {-er-}**

Kanuni inaeleza kuwa mofimu {-īr-} na {-er-} hutumika baada ya mizizi ya vitenzi vinavyoishia kwa konsonanti katika vitenzi vya Kigīchūgū. Kwa mfano,

52. thom-er-a —— somea

47. tham-īr-a —— hamia

58. twar-īr-a —— pelekea

Vinyambulishi hivi vya kauli ya TDA huweza kufauatana na kauli mbalimbali kama ilivyofafanuliwa katika sehemu ya 4.5.1 (a-d), 4.5.2 (a, d, f- i) na 4.5.3 (a) na (b).

#### **4.6.3 Kanuni ya Viambishi Nyambulishi Radidi**

Kama wanavyosema Kihore, Massamba na Msanjila (2012: 130), kanuni ya viambishi nyambulishi radidi inasema kwamba upo uwezekano wa baadhi ya viambishi nyambulishi kurudiwa katika mwandamano katika umbo moja. Hali hii pia inajitokeza katika Kigīchūgū hasa mwandamano unaohusisha kauli ya TSH. Kwa mfano katika sehemu ya 4.5.1 (c)) na (g), TSH inapoandamana na TDA na TDN, urudiaji wa TSH hutokea. Kwa mfano,

2. andīk –ith -īr -i -a  
andīk –TSH –TDA –TSH -I  
andikishia
  
29. nyw –ith –an –i -a  
nyw –TSH –TDN –TSH -I  
nyeshana

Vilevile katika sehemu ya 4.5.2 (a) na (c), hali ya urudiaji wa TSH inajitokeza katika mfuatano wa TSH -TDN -TDA na TDU –TSH -TDN. Kwa mfano,

47. tham –ith –an –īr –i -a  
tham -ESH –AN -EA -ESH -I  
hamishiana
  
22. kūnj –ūr –ith –an –i -a  
kunj -UA –ESH –AN –ESH -I  
kunjulishana

Katika urudiaji huu mofimu {-i-}, ambayo huonyesha usababishi mfupi katika Kigīchūgū ndiyo iliyorudiwa. Kama anavyooleza Wesana-Chomi (2013:73), kinyambulishi cha kauli ya TSH kinafaa kutokea kabla ya kinyambulishi cha kauli ya TDA na pia kabla ya kauli ya TDN. Hali hii imejadiliwa kwa kina katika mifano ya sehemu ya 4.5.1, 4.5.2 na 4.5.3 iliyotangulia katika Kigīchūgū.

#### **4.6.4 Kanuni ya Kiambishi Nyambulishi {-an- }**

Kama anavyosema Wesana-Chomi (2013:72), kiambishi kinyambulishi {-an-} hupachikwa kwenye vitenzi vyenye sifa maalumu tu ambavyo mizizi yake inaweza kupokea kinyambulishi {-an-}. Sifa hiyo ni kwamba kitenzi sharti kitaje tendo linalohusisha wahusika wawili au zaidi. Kila mhusika ni mtenda tendo na pia ni mtendwa. Katika vitenzi vya Kigīchūgū, kinyambulishi hiki kinaweza kutanguliwa na TDA, TSH na TDU katika mfuatano wa viambishi nyambulishi viwili kama ilivyoonyeshwa katika mfano 4.5.1 (d), (g) na (i) au kikafuatana na viambishi nyambulishi vitatu na vinne kama ilivyo katika mifano 4.5.2 a, b, c, h na i na 4.5.2 (a).

#### **4.7 Hitimisho**

Sura hii imechanganua mofolojia ya unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū. Fonimu za Kigīchūgū yaani konsonanti na irabu zilifafanuliwa kwa kina. Fonimu hizi zimeainishwa kwani ndizo zilitumika katika unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū. Viambishi tamati katika unyambulishaji wa vitenzi vya Kigīchūgū vilijadiliwa katika kauli sita; kutendea, kutendwa, kutendesha, kutendana, kutendeka na kutendua. Katika uchanganuzi wa data, viambishi mbalimbali vilivyotumika katika kauli hizi pia vilionyeshwa kwa kutilia maanani irabu zinazopatikana kwenye mizizi ya vitenzi. Ilibainika kuwa kuna uchopekaji wa fonimu kama vile /r/ katika kauli ya unyambulishaji ya kutendea na /k/ katika kauli ya kutendeka. Uchopekaji huu ulitumikizwa ili kuhifadhi muundo wa K-V katika Kigīchūgū. Vilevile, uyeyushaji na udondoshaji wa irabu umetumikizwa ambapo katika kauli ya kutendwa irabu /u/ inayeyushwa na kuwa /w/ katika baadhi ya vitenzi vya Kigīchūgū vilivyoishia kwa irabu /i/ na kufuatwa na irabu /u/. Kwa upande mwengine katika kauli ya kutendwa, irabu /i/ ilidondolewa na irabu /u/ kuachwa kama kiambishi cha kauli hiyo ili kuzuia mfuatano wa irabu tatu na pia kuhifadhi maana ya vitenzi husika. Vitenzi vya Kigīchūgū huweza kuambikwa viambishi vinyambulishi viwili, vitatu na vinne kwa wakati mmoja. Hali hii ni tofauti na lugha nyingine za Kibantu ambazo hukubali mfuatano hadi viambishi vitatu. Mifuatano iliyokubalika katika Kigīchūgū ilielezwa kulingana na kanuni ya Kioo kwa mujibu wa Baker (1985). Hata hivyo mpishano umeruhusiwa ambao ni kinyume na mfuatano wa Hyman (2003) ili kuhifadhi maana ya kitenzi.

**SURA YA TANO**  
**MAANA ZINAZOWAKILISHWA NA MAUMBO YA UNYAMBULISHAJI**  
**WA VITENZI KATIKA KIGICHUGU**

### **5.1 Utangulizi**

Kama ilivyodokezwa katika Sura ya Nne, Kigīchūgū husheheni vitenzi ambavyo hufuata mifanyiko tofauti katika unyambulishaji wake. Maumbo ambayo huundwa kutokana na mifanyiko ya unyambulishaji huweza kuwakilisha maana tofauti. Sura hii itajadili maana hizo kwa kina.

Kama wanavyosema Kihore, Massamba na Msanjila (2012), utaratibu wa unyambulishaji katika Kiswahili unaweza kwenda hadi hatua nne, na kuwa kiambishi nyambulishi kinachoongezwa katika kila hatua huongeza maana ya ziada. Hali hii pia hujitokeza katika unyambulishaji wa vitenzi vya Kigīchūgū. Maana zilizojadiliwa ni kama vile zinavyojitokeza katika kauli sita za unyambulishaji ambazo ni kutendea, kutendwa, kutendesha, kutendana, kutendeka na kutendua.

### **5.2 Kauli ya Kutendea**

Kauli ya Kutendea huonyeshwa kwa viambishi {-īr-} au {-er-} katika lugha ya Kigīchūgū. Kama anavyooleza Khamis (2008) na Charwi (2013), kauli ya utendea husababisha vitenzi si elekezi kuwa elekezi. Hali hii inadhahirika katika Kigīchūgū kama ifuatavyo:

4. a) Mami **nī-a-ra-rug-a**. -si elekezi

Mama anapika.

- b) Mami **nīa-ra-rug-īr-a** mwana. –elekezi

Mami Nf- Nj- rug- TDA-I mwana.

Mama anapikia mtoto.

5. a) Kamau **nī-a-ra-kuu-ir-e**. -si elekezi

Kamau alibeba.

- b) Kamau **nīa-ra-ku-īr-e** nyina. –elekezi

Kamau Nf- Nj- ku- TDA-I nyina.

Kamau alimbebea mamake.

Mifano hii inaonyesha kuwa vitenzi ambavyo si elekezi vikipitia unyambulishaji katika kauli ya TDA vitenzi hivyo hubadilika kuwa elekezi. Vitenzi vya Kigīchūgū vilivyo katika kauli ya TDA huonyesha kuwa kitendo huwa kimefanywa kwa niaba ya au kwa manufaa ya kitu au mtu mwingine. Kwa mfano:

13. cora (chora)	—	cor- <b>er</b> -a (chorea)
		cor-TDA- I
41. rūnga (lainisha)	—	rūng- <b>īr</b> -a (lakia)
		rūng- TDA- I
15. giria (pangusa)	—	gir- <b>īr</b> -i-a (pangusia)
		gir-TDA- I

Kulingana na misingi ya Nadharia ya Kioo (Baker 1985), unyambulishaji kimofolojia unafaa kuafiki unyambulishaji kisintaksia. Hali hii imeonyeshwa katika sentensi kama,

6. Githaka **nī-a-cor-er-a** Wambui mbica.  
Githaka Nf-Nj-cor-TDA-I Wambui mbica.  
Githaka amemchorea Wambui picha.

#### 7. **Nī-a-tūng-īr-a** nyina ageni.

- Nf- Nj-tūng-TDA-I nyina ageni.  
Amelakia mamake wageni.

8. Kinyua **nī-end-er-i-a** Bundi kīratu.  
Kinyua Nf- end-TDA-I Bundi kiratu.  
Kinyua amemuuzia Bundi kiatu.

Katika mifano iliyotolewa, kauli ya TDA inafuata mzizi moja kwa moja kama ilivyojadiliwa kattika sura ya nne. Sentensi zinaonyesha dhana ya mtu kufanya kitendo kwa niaba ya mtu mwingine. Kwa mfano, katika (6), Githaka alichora picha kwa niaba ya Wambui au ikawa na maana kuwa Wambui alinufaika kutokana na picha iliyochorwa na Kamau. Vilevile (7) na (8) zinaonyesha dhana ileile. Vitenzi vya Kigīchūgū katika kauli ya TDA huonyesha kuwa watu au vitu viwili vinahusika. Katika vitu au watu hawa, mmoja huwa hafanyi chochote bali wa pili ndiye

anayetenda kitendo kinachomwathiri yule asiyetenda. Kitendo kinachofanywa humfaidi yule asiyekitenda au hutendwa kwa niaba yake. Kauli ya TDA kama ilivyojadiliwa katika Sura ya Nne huweza kuambatana na vinyambulishi vingine pia ili kuleta maana ya kitendo kufanywa kwa manufaa ya au kitendo kufanywa kwa niaba ya. Kauli hizi ni kama vile. TSH+TDA, TDA+TDN, TDU+TDA, TSH+TDA+TDW mionganoni mwa zingine. Mfuatano huu wa viambishi unaweza kuonyeshwa katika sentensi kama;

9. Kamau **nī-a-rīm-ith-īr-i-a** Gitari.

Kamau Nf-Nj- rīm-TSH-TDA-tsh-I Gitari.

Kamau amemlimishia Gitari.

10. **Nī-ma-gūr-an-īr-a** matunda.

Nf-Nj-gūr-TDN-TDA-I matunda.

Wamenunuliana matunda.

Mifano hii inaonyesha unyambulishaji kisintaksia na jinsi unavyoakisi unyambulishaji kimofolojia, kama inavyopendekezwa na Kanuni ya Kioo kwa mujibu wa Baker (1985). Hali hii inaonyesha kuwa mofimu zenye uamilifu kimaana katika vitenzi zimebekwa karibu na kitenzi ikilinganishwa na mofimu ambazo hazina uzito kiuamilifu. Mifuatano katika sentensi hizi inaonyesha kuwa kitendo kilitendwa kwa niaba ya au kwa manufaa ya mtu au kitu fulani.

### 5.3 Kauli ya Kutendwa

Kauli ya kutendwa huonyeshwa kwa kinyambulishi {-w-} katika Kigīchūgū. Vitenzi katika kauli ya TDW humaanisha kuwa kitendo kinampata mpokeaji. Hii ina maana pia kuwa tendo linampata mtu au kitu bila ye ye kikitenda kitendo hicho. Kwa mfano,

9. būr-w-a

būr –TDW-I

pigwa

34. rīm-w-a

rīm-TDW-I

limwa

2. andīk-w-a

andīk – TDW-I

andikwa

Mifano hii kama ilivyojadiliwa katika sura ya nne, inaonyesha kwamba mhimili wa kwingineko katika nadharia ya ML kwa mujibu wa Kiparsky (1982) ulitumikizwa. Mifano iliyoorodheshwa ya Kigīchūgūinaonyesha kuwa irabu /u/ iliyejushwa na kuwa /w/ kwa sababu baada ya uambishaji, irabu mbili zilifuatana yaani /u/ na /a/.

Mifano hii inaweza kutumiwa katika sentensi kama;

11. Kamau **nī-a-būr-w-a.**

Kamau Nf- Nj- būr-TDW-I.

Kamau amechapwa.

12. Mūgunda **nī-wa-rīm-w-a.**

Mūgunda Ng-Nj- rīm-TDW-I

Shamba limelimwa.

13. Ibuku **nī-rīr-andīk-w-a.**

Ibuku Ng-Nj- andīk-TDW- I

Kitabu kinaandikwa.

Mifano hii inadhihirisha mtu na vitu vinavyopokea kitendo moja kwa moja. Hata hivyo, kinyambulishi {-w-} huweza kufuatana na vinyambulishi vingine aidha katika mfuatano wa vinyambulishi viwili, vitatu, au vinne katika Kigīchūgū. Data hii inaafiki mawazo ya Hyman (2003) kuhusu vitenzi katika lugha za Kibantu kuwa na uwezo wa kuchukua viambishi nyambulishi mbalimbali katika mfuatano aliopendekeza wa CARP (usababishi, Utendea, utendano na Utendwa) ingawa alisema kuwa baadhi ya lugha hurusu mpishano. Kwa mfano;

10. but-īr-w-a

but-TDA-TDW-I

futiwa

22. kūnj-ūr-īr-w-a  
kūnj-TDU-TDA-TDW-I  
kunjuliwa

30. ob-or-ith-īr-w-a  
ob-TDU-TSH-TDA-TDW-I  
fungulishiwa

Hali hii inaweza kuonyeshwa katika sentensi kama;

14. **Nī-a-but-īr-w-a**  
Nf-Nj- but- TDA-TDW-I  
Amefutiwa.

15. **Nī-ma-kūnj-ūr-īr-w-a** nguo  
Nf-Nj- kūnj-TDU-TDA-TDW-I nguo  
Wamekunjuliwa nguo.

Sentensi hizi zinaafiki unyambulishaji kimofolojia katika mfuatano wa viambishi nyambulishi. Hali hii ni kwa misingi ya Kanuni ya Kioo kwa mujibu wa Baker (1985). Mifano hii inaonyesha kuwa kinyambulishi {-w-} kikifuatana na vinyambulishi vingine huleta maana ya kitendo kutendwa kwa niaba ya au manufaa ya mtu au kitu fulani. Vilevile kanuni ya kiambishi nyambulishi {-w-} imejitokeza pale ambapo kiambishi {w} kimetokea kama kiambishi nyambulishi cha mwisho katika mifuatano kama wanavyosema Kihore, Massamba na Msanjila (2012), kuwa katika muundo wowote wa kitenzi katika hali ya kutendwa, kiambishi {-w-} kinachowakilisha hali hiyo lazima kitokee mwishoni.

#### **5.4 Kauli ya Kutendesha**

Kauli ya kutendesha huonyeshwa kwa viambishi {-ithi-} au {-i-} katika Kigīchūgū. Vitenzi katika kauli ya TSH humaanisha kuwa kitendo kimesababishwa na mtu au kiyu fulani. Katika lugha ya Kigīchūgū, vitenzi katika kauli hii huweza kuonyesha kuwa aidha mtenda amefanya kitendo hicho kwa kulazimishwa au kwa kusaidiwa kukitenda. Kwa mfano,

34. rīma (lima) — rīm-**ithi**-a (limisha)  
rīm- TSH-I

33. rība (lipa) — rīb-**ithi**-a (lipisha)  
rīb- TSH-I

8. bura (pangusa) — bur-**ithi**-a (pangusisha)  
bur- TSH-I

Mifano hii imetumiwa katika sentensi kuonyesha kuwa kitendo kimesababishwa na mtu au kitu fulani. Kwa mfano:

Waithera **nī-a-rīm-ithi-a** mūgūnda wake.

16. Waithera Nf- Nj- rīm-TSH- I mūgūnda wake.

Waithera amelimisha shamba lake.

Katika sentensi hii, kitendo cha kulimisha kimesababishwa na Waithera. Vilevile kauli ya TSH inaweza kutumika katika sentensi kuonyesha kulazimishwa au kusaidiwa kwa mtenda. Kwa mfano,

17. Njoroge **nī-a-bur-ithi-a** Mwaniki nyūmba.

Njoroge Nf- Nj- bur- TSH-I Mwaniki nyūmba.

Njoroge amepangusisha Mwaniki nyumba.

Sentensi hii inaweza kuwa na maana kuwa aidha Njoroge amemsaidia Mwaniki kupangusa nyumba au amemlazimisha Mwaniki kupangusa nyumba. Kauli ya TSH huweza kufuatana na kauli nyambulishi zingine aidha katika mfuatano wa vinyambulishi viwili, vitatu au vinne kama ilivyojadiliwa katika Sura ya Nne. Ifanyikavyo hivi, maana katika kauli ya TSH huweza kuongezeka. Kwa mfano, kauli ya TSH inapofuatana na TDA kama vile katika mifano #rugithīria# (pikishia) au #andīkithīria# (andikishia) humaanisha kuwa kitendo kimetendeshwa kwa niaba ya mtu au kitu fulani. Vitenzi hivi vinaweza kutumiwa katika sentensi kama ifuatavyo:

18. Wanjiru **nī-a-rug-ith-īr-i-a** nyina irio.

Wanjiru Nf-Nj- rug- TSH-TDA- tsh -I nyina irio.

Wanjiru amempikishia mamake chakula.

19. Mwalimu **nī-andīk-ith-īr-i-a** Kamau marūa.

Mwalimu Nf-andīk- TSH- TDA-tsh-I Kamau marūa.

Mwalimu amemwandikishia Kamau barua.

Mifano katika sentensi hizi inaonyesha kuwa mfuatano wa viambishi nyambulishi katika sentensi unaakisi mfuatano wa viambishi nyambulishi kimofolojia kama inavyopendezwa na Kanuni ya Kioo kwa mujibu wa Baker (1985). Mfuatano huu vilevile unakubaliana na pendekezo la Hyman (2003) unaopendekeza kwamba mofimu nyambulishi ya TDA haiwezi kutangulia mofimu nyambulishi ya TSH.

Kauli ya TSH huweza pia kufuatana na kauli zingine kama vile, TDU+TSH, TSH+TDN, TSH+TDA+TDW, TSH+TDN+TDW, TDU+TSH+TDN, Miongan mwa zingine. Kama ilivyobainika katika Sura ya Nne, mifuatano hii huonyesha kuwa aidha yambwa ililazimishwa au kusaidiwa kutenda kitendo fulani.

### **5.5 Kauli ya Kutendana**

Kauli ya kutendana huwakilishwa kwa mofimu {-an-} katika Kigīchūgū. Khamis (2008) anarejelea kauli hii kama unyambulishaji ambatani. Anasema kuwa unyambulishaji ambatani unaeleza mchakato wa unyambulishi unaounda kitenzi chenye kiambishi tamati -an- katika Kiswahili. Anaeleza kuwa kitenzi kilichonyambulishwa huleta maana ya kutendana, kushirikiana, kuvutana, kutengana na kadhalika kufuatana na maana ya shina la kitenzi. Katika Kigīchūgū, vitenzi katika kauli ya kutendana huonyesha kitendo kinachokwu na washiriki wawili wanaotendeana au kushirikiana katika kitendo hicho. Charwi (2013) anaeleza kuwa kisintaksia, kauli ya kutendana huondoa yambwa kutoka nafasi yake na kuihamisha kwenye kiima na wote yaani yambwa na kiima hupewa dhima mbili kwa wakati mmoja, yaani mtenda na wakati huohuo huwa mtendwa. Hali hii pia inadhihirika katika Kigīchūgū kama inavyoonyeshwa katika mifano ifuatayo;

20. a) Njeri **nī-ak-īr-a** Njoki nyūmba.

Njeri Nf- ak-TDA-I Njoki nyūmba.

Njeri amemjengea Njoki nyumba.

b) Njeri na Njoki **nī-m-ak-an-īr-a** nyūmba.

Njeri na Njoki Nf-Nj- ak-TDN- TDA-I nyūmba.

Njeri na Njoki wamejengeana nyumba.

Katika sentensi (16) Njeri ambaye katika (15) alikuwa mtenda amepewa dhima mbili kwani katika (16) amekuwa mtendwa pia. Vilevile, Njoki ambaye katika (15) alikuwa mtendwa, katika (16) amepewa dhima ya mtenda.

Charwi (2013) anaendelea kueleza kuwa kauli ya TDN hukipotezea kitenzi sifa ya kuhitaji yambwa na pia huleta mabadiliko ya nafasi ya yambwa moja. Kwa mfano:

21. Kinyua na Karimi **nī-m-end-an-a**.

Kinyua na Karimi Nf-Nj-end-TDN-I

Kinyua na Karimi wanapenana.

Kauli ya TDN katika Kigīchūgū kama kauli zingine huweza kuambatana na viambishi nyambulishi vingine aidha katika hatua ya pili, tatu hata ya nne. Mifuatano hii huleta maana ya kitendo kufanyika baina ya watu wawili au zaidi au kitendo kutendeka kwa niaba ya au kwa manufaa ya mtu au kitu kingine. Mifuatano hii ni kama vile, TSH+TDA, TSH+TDN, TSH+TDN+TDW, TDU+TSH+TDN mionganini mwa mifuatano mingine.

## 5.6 Kauli ya Kutendeka

Kauli ya kutendeka huonyeshwa kwa viambishi {-īk-} au {-ek-} katika Kigīchūgū. Vinyambulishi hivi huonyesha kutendeka kwa tendo au uwezekano wa tendo hilo kutendeka. Khamis (2008) anasema kuwa katika Kiswahili, kiambishi tamati -ik-kinaongezewa kwenye mzizi kuonyesha mabadiliko ya kinyambulishi yaliyotokea. Anatoa mfano wa kitenzi #vunja# na #vunjika# kuonyesha dhima tofauti. Kitonzi #vunja# anakieleza kama kitonzi elekezi na #vunjika# kama kitonzi si elekezi. Anajadili pia unyambulishaji uwezo ambapo alieleza kuwa ni unyambulishaji unaohusiana na unyambulishi tendeka. Anaeleza unyambulishi uwezo kama sheria ya kuunda neno ambalo athari yake ni kuingiza dhana ya uwezo kwenye maana ya kitonzi kilichonyambulishwa. Hali hii inadhahirika katika vitenzi vya Kigīchūgū kama vile,

30. oba	—	ob- <b>ek-</b> a	(fungika)
		ob- TDK-I	
52. thoma	—	thom- <b>ek-</b> a	(someka)
		thom- TDK- I	
17. ina	—	in- <b>ik-</b> a	(imbika)
		in-TDK- I	
13. cora	—	cor- <b>ek-</b> a	(choreka)
		cor- TDK- I	

Mifano hii inaonyesha kuwa aidha kitendo kimetendeka au kina uwezekano wa kutendeka. Kwa mfano katika sentensi,

22. a) Mūkwa **nī- w- ob- ek- a.**

Mūkwa Ng- Nj- ob-TDK- I

Kamba imefungika.

b) Mūkwa **nī- ū- kw- ob- ek- a.**

Mūkwa Ng-Nj- ktw- ob- TDK- I

Kamba itafungika.

23. a) Ībuku **nī- rī- ra- thom- ek- a.**

Ībuku Ng-Nj- ktw- thom- TDK- I

Kitabu kinasomeka.

b) Ībuku **nī- rī- kū- thom- ek- a.**

Ībuku Ng- Nj- ktw- thom- TDK- I

Kitabu kitasomeka.

Katika sentensi hizi, mfano (22:a) na (23:a) zinaonyesha kutendeka kwa kitendo na sentensi (22:b) na (23:b) zinapoongezewa mofimu ya wakati zinaonyesha uwezekano wa kutendeka kwa kitendo. Kama ilivyolezwa katika Sura ya Nne, hii ni kauli ambayo haichukui mfuatano wa mofimu nyambulishi nyingi katika Kigīchūgū. Mfuatano wa viambishi nyambulishi katika kauli ya TDK ni kama vile, TDU+TDK

na TSH+ TDK ili kuleta maana ya kitendo kutendeka au uwezekano wa kitendo kutendeka. Mfuatano huu unaweza kuonyeshwa katika sentensi;

24. Mūrango **nī- wa- bing- ūr- īk- a.**

Mūrango Ng- Nj- bing-TDU- TDK- I.

Mlango umefunguka.

25. Mūgūnda **nī- wa- rīm- ith- īk- i- a.**

Mūgūnda Ng- Nj- rīm- TSH- TDK- tsh- I.

Shamba limelimishika.

### 5.7 Kauli ya Kutendua

Kauli ya kutendua huonyeshwa kwa mofimu {-or-} na {-ūr-} katika Kigīchūgū. Kauli hii katika Kigīchūgū huwa na maana ya tendo kuwa kinyume. Kiambishi {-or-} hupachikwa kwenye mzizi wa vitenzi vyenye irabu /a/, /e/, /i/ na /u/. Kwa mfano,

6. binga - —— bing- **ūr-** a (fungua)

bing- TDU-I

1. aka —— ak- **ūr-** a (jengua)  
ak- TDU- I

5. bata —— bat- **ūr-** a (kwamua)  
teg-TDU-I

30. oba —— ob- **or-** a (fungua)  
ob-TDU-I

Vitenzi hivi vilitumiwa katika sentensi kuonyesha dhana hiyo ya kinyume kama ifuatavyo:

26. a) Njoroge **nī- a- bing- a** mūrango.

Njoroge amefunga mlango.

b) Njoroge **nī- a- bing- ūr- a** mūrango.

Njoroge Nf- Nj-bing-TDU-I mūrango.

Njoroge amefungua mlango.

27. a) Mutahi **nī- ak- a** nyūmba.

Mutahi amejenga nyumba.

b) Mutahi **nī- ak- ūr- a** nyūmba.

Mutahi Nf-ak- TDU- I nyūmba.

Mutahi amejengua nyumba.

28. a) Ciana **nī- ci- a- teg- a** mūtego wa mbīa.

Watoto wametega mtego wa panya.

b) Ciana **nī- ci- a- teg- ūr- a** mūtego wa mbīa.

Ciana Nf- Nj- teg- TDU- I mūtego wa mbīa.

Watoto wametegua mtego wa panya.

Kauli ya TDU katika mfuatano wa viambishi vya vitenzi vya Kigīchūgū huweza kuambatana na kauli ya TDA, TSH, TDW, TDN katika mfuatano wa kauli mbili, TDU+TSH+TDW, TDU+TSH+TDN, TDU+TDA+TDW na TDU+TDN+TDA, katika mfuatano wa viambishi nyambulishi vitatu na TDU+TSH+TDA+TDW katika mfuatano wa viambishi nyambulishi vinne. Kauli ya TDU inapofuatana na kauli ya TDA huonyesha kuwa kitendo kimetendwa kwa niaba ya mtu au kitu, na inapofuatana na TSH huonyesha kuwa mtu anayetenda kitendo hicho amekifanya kwa kusaidia au kulazimisha. Kwa mfano,

30. ob-or-er-a (fungulia)

Wanjiku **nī- ob- or- er- a** Wambui mūkwa.

Wanjiku Nf- ob- TDU- TDA- I Wambui mūkwa.

Wanjiku amemfungulia wambui kamba.

22. kūnj-ūr-īr-a (kunjulia)

Njeri **nī- egū- kūnj- ūr- īr- a** mwana nguo.

Njeri Nf- Nj- kūnj- TDU- TDA-I mwana nguo.

Njeri atamkunjulia mtoto nguo.

6. bing-ūr-ithi-a (fungulisha)

Mwalimu **nī- a- bing- ūr- ithi- a** arutwo bahasa.

Mwalimu Nf-Nj- bing- TDU-TSH- I arutwo bahasa.

Mwalimu amewafungulisha wanafunzi bahasha.

Mifano katika sentensi (a) inaonyesha kuwa vitendo vilitendwa kwa niaba ya, na mifano katika sentensi (b) inaonyesha kuwa vitendo vilitendwa kwa mtu kuasidia au kulazimishwa. Kauli ya TDU vilevile inaweza kuambatana na TDW ili kuleta maana kuwa kitendo kinampata mpokeaji kama inavyoonyeshwa kwenye mifano ifuatayo,

30. ob-or-w-a

ob- TDU- TDW- I

funguliwa

Wanjiru **nī- ob- or- w- a** njara.

Wanjiru Nf-ob- TDU-TDW-I njara.

Wanjiru amefunguliwa mkono.

22. kūnj-ūr-w-a

kūnj-TDU-TDW-I

kunjuliwa

Nguo **nī- ci- a- kūnj- ūr- w- a** nī Wairimu.

Nguo Ng- Nj-kūnj-TDU-TDW-I nī Wairimu.

Nguo zimekunjuliwa na Wairimu.

Kauli ya TDU inapoambatana na kauli ya TDN humaanisha kuwa washiriki wawili wanatendeana jambo kwa kushirikiana au wakatendeana kitendo kwa niaba ya, kama ilivyoonyeshwa kwenye mifano ya sentensi zifuatazo:

30. ob-or-an-īr-a

funguliana

Njeri na Wairimu **nī- m- ob- or- an- īr- a** mīkwa.

Njeri na Wairimu Nf- Nj- ob- TDU-TDN-TDA- I mīkwa.

Njeri na Wairimu wamefunguliana kamba.

57. tum-ūr-an-īr-a

shonoleana

Wanjiku na Muthoni **nī- me- gūtum- ūr- an- īr- a** nguo.

Wanjiku na Muthoni Nf-Nj-tum-TDU- TDN- TDA-I nguo.

Wanjiku na Muthoni watashonoleana nguo.

Kauli ya TDU inapoambatana na kauli ya TSH+TDN humaanisha kuwa washiriki wawili wanasadiana kutendeana kitendo kile kimoja. Hali hii inaonyeshwa kwenye mifano ifuatayo ya Kigīchūgū.

30. ob-or-ith-an-i-a

ob-TDU-TSH-TDN-I

fungulishiana

Aciari **nī- ma- r- ob- or- ith- an- i- a** mīkwa.

Aciari Nf- Nj-ob-TDU- TSH- TDN- tsh- I mīkwa.

Wazazi wanafungulishiana Kamba.

22. kūnj-ūr-ith-an-i-a

kūnj-TDU-TSH-TDN-I

kunjulishiana

Muthoni na Wanja **nī- ma- ra- kūnj- ūr- ith- an- i- a** nguo ciao.

Muthoni na Wanja Nf- Nj- kūnj- TDU- TSH- TDN- tsh- I nguo ciao.

Muthoni na Wanja wanakunjulishiana nguo zao.

6. bing-ūr-ith-an-i-a

bing-TDU-TSH-TDN-I

fungulishiana

Arimu arīa erī **nī- ma- ra- bing- ūr- ith- an- i- a** mīrango.

Arimu arīa erī Nf- Nj- bing-TDU- TSH- TDN-tsh-I mīrango.

Walimu wale wawili wanafungulishiana milango.

Kwa upande mwingine, kauli ya TDU inapoambatana na TDA+TDW huonyesha kuwa kitendo kimetendwa kwa niaba ya mtu fulani au kitu fulani. Hali hii inaonyeshwa kwenye mifano ifuatayo ya sentensi katika Kigīchūgū.

6. bing-ūr-īr-w-a  
bing-TDU-TDA-TDW-I  
funguliwa  
Mūrutwa **nī- a- bing- ūr- īr- w- a** mūrango.  
Mūrutwa Nf- Nj- bing- TDU- TDA- TDW- I mūrango.  
Mwanafunzi amefunguliwa mlango.

30. ob-or-er-w-a  
ob-TDU-TDA-TDW-I  
funguliwa (kwa mfano kamba)  
Nyawira **nī- e- kw- ob- or- er- w- a** mūkwa.  
Nyawira Nf- Nj- ktw- ob-TDU- TDA- TDW- I mūkwa.  
Nyawira atafunguliwa kamba.

57. tum-ūr-īr-w-a  
tum-TDU-TDA-TDW-I  
shonolewa  
Njoki **nī- a- tum- ūr- īr- w- a** nguo nī Wawira.  
Njoki Nf- Nj- tum- TDU- TDA- TDW- I nguo nī Wawira.  
Njoki ameshonolewa nguo na Wawira.

Mifano ya sentensi katika kauli hii inaonyesha kuwa unyambulishaji kimofolojia unaakisi unyambulishaji kisintaksia katika vitenzi vya Kigīchūgū.

## 5.8 Hitimisho

Katika sura hii, maana zinazowakilishwa na kauli sita za unyambulishaji ambazo ni: kutendea, kutendwa, kutendana, kutendesha, kutendeka na kutendua zimejadiliwa. Maana hizi zimejadiliwa kulingana na Kanuni ya Kioo. Mifuatano inayokubalika na kauli mbalimbali za unyambulishaji na maana inayotokana na mifuatano hiyo pia zimeelezwa. Imebainika kuwa mofimu za unyambulishaji katika Kigīchūgū huleta athari kisintaksia. Imebainika kuwa mofimu za kauli ya TDA huathiri kitenzi si elekezi kuwa elekezi na huleta maana ya kitendo kufanywa kwa niaba ya mtu au kitu. Kauli ya TDW imeonyesha kuwa kitendo hufanywa kwa kuelekea kwa mtu au kitu

fulani bila yeye kukitenda kitendo husika. Kwa upande mwingine, kauli ya TSH imebaini kuwa aidha kitendo kimesababishwa na mtu au kitu fulani au pia imeonyesha kuwa aidha mtenda amefanya kitendo kwa kulazimishwa au kusaidiwa kukitenda. Kauli ya TDN imeonyesha kuwa washiriki wawili hushirikiana kukitenda kitendo kimoja. Kauli ya kutendeka nayo imebainisha kuwa kitendo kimetendeka au kuna uwezekano wa kutendeka kwa kitendo. Mwishowe, kauli ya kutendua, huwa na maana ya tendo kuwa kinyume.

## **SURA YA SITA**

### **MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **6.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti**

Utafiti huu ulifanywa kuhusu unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū. Malengo ya utafiti huu yalikuwa ni kufafanua mifanyiko inayohusika katika utaratibu wa unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū na kujadili maana zinazowakilishwa na maumbo ya unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū. Utafiti huu ulidhamiria kuchangia katika kuongeza maarifa ya kiutafiti yanayohusu sarufi ya Kigīchūgū. Utafiti huu ulifanyiwa maktabani na pia nyanjani. Mtafiti alienda nyanjani ili kuthibitisha vitenzi ambavyo alizalisha kwa kuwa ana uelewa na umilisi wa Kigīchūgū.

Utafiti huu ultumia miongozo mbalimbali ili kuhakikisha usahihi wa data na habari za utafiti. Kwanza, mtafiti alitumia Nadharia ya Mofolojia Leksia. Nadharia hii ilisaidia kwani ni nadharia zalishi na nyambulishi na ni nadharia inayoonyesha uhusiano wa sheria zinazojenga maumbo ya kimofolojia na sheria zinazodhibiti namna maumbo haya yanavyotamkwa. Pili, mtafiti aliongozwa na Kanuni ya Kioo. Kanuni hii ilisaidia kwani ni kanuni inayoonyesha mpangilio maalum unaofuatwa katika unyambulishaji wa vitenzi katika lugha za Kibantu.

Utafiti huu umegawika katika sura sita. Sura ya Kwanza ambayo ni utangulizi, imeshughulikia masuala kama vile; Usuli wa mada, Suala la utafiti, Malengo ya utafiti, Maswali ya utafiti, Upeo wa utafiti na Maelezo ya istilahi pia yamefafanuliwa. Sura ya Pili imejadili mwauo wa maandishi. Mwauo huu ulibainisha kuwa unyambulishaji wa vitenzi vya Kigīchūgū ni sehemu ambayo haijafanyiwa utafiti wa kitaaluma. Dhana ya unyambulishaji wa vitenzi kulingana na wataalamu mbalimbali imeangaziwa katika sura hii. Kazi tofauti kuhusu unyambulishaji wa vitenzi zimeangaziwa ili kuonyesha mchango wake katika utafiti huu. Sura hii pia iliangazia nadharia zilizoongoza utafiti huu ambazo ni Nadharia ya Mofolojia Leksia na Kanuni ya Kioo. Sura ya Tatu ilishughulikia mbinu za utafiti na mbinu za uchanganuzi wa data. Sura ya Nne na Tano zilihu uwasilishaji na uchanganuzi wa data. Data iliwasilishwa na kuchanganuliwa kwa maelezo. Katika Sura ya Nne, uchanganuzi wa data ulifanywa kwa kuzingatia mifanyiko katika unyambulishaji wa vitenzi vya

Kigīchūgū. Jumla ya fonimu ishirini na nne za Kigīchūgū zilitambulishwa. Fonimu hizi ni Konsonanti kumi na saba na vokali ya saba. Utafiti ulibaini kuwa Kigīchūgū hakina fonimu /h/ kama ilivyo katika lahaja zingine za Kikuyu hivyo basi uwepo wa Konsonanti kumi na saba badala ya kumi na nane. Kutokana na maelezo, utafiti huu unadhihirisha kuwa vitenzi vya Kigīchūgū huwa na mofimu nyambulishi. Mofimu hizi huambishwa baada ya mzizi wa kitenzi. Kutokana na utafiti huu, mtafiti alibaini kuwa Kigīchūgū kina mofimu nyambulishi za TDA, TDW, TSH, TDN, TDK na TDU. Utafiti huu ulibaini kuwa vitenzi vya Kigīchūgū hukubali mfuatano wa mofimu nyambulishi katika hatua ya pili, tatu na hata ya nne.

Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa mofimu ya TDA ndiyo inayofuatana na mofimu nyambulishi nyingi ikilinganishwa na nyingine. Utafiti ulibaini kuwa kubadilisha mpangilio katika mfuatano wa mofimu nyambulishi hutatiza maana inayokusudiwa. Utafiti vilevile ulionyesha kuwa mofimu nyambulishi katika Kigīchūgū zinafuatana kulingana na uzalishaji na uelekezi. Kanuni zinazoruhusu na kuzuia mifuatano hii zilijadiliwa katika utafiti. Sababu za kifonolojia ni mojawapo ya vizuizi kwani mofimu nyingine haziwezi kufuatana kwa sababu zinafanana kifonolojia.

Katika Sura ya Tano, maana zinazowakilishwa na maumbo ya unyambulishaji zilijadiliwa. Maana zilizojitokeza ni pamoja na kitendo kufanywa kwa niaba ya au kwa manufaa ya kitu au mtu. Maana hii iliwalishwa na mofimu ya TDA. Maana ya pili ilionyesha kuwa mtenda aidha alilazimishwa au alisaidiwa kutenda kitendo fulani. (TSH). Tatú, wahusika wawili kushirikiana kutenda kitendo kimoja ambayo ilionyeshwa kwa mofimu za TDN. Maana ya kinyume pia ilijadiliwa kwa kuwalishwa kwa mofimu za TDU. Uwezekano au kufanyika kwa kitendo ilionyeshwa kwa mofimu nyambulishi TDK. Mwisho, ni maana ya kitendo kumpata mtu bila yeze kuitenda nayo huwalishwa kwa na mofimu nyambulishi za TDW. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa kiwango cha Mofolojia kinachohusika na unyambulishaji wa vitenzi huweza kushirikiana na viwango vingine vya kiisumu kama vile Fonolojia, Sintaksia na Semantiki.

## **6.2 Hitimisho**

Kutokana na utafiti huu, kuna mambo kadhaa ambayo tunaweza kuhitimisha tukizingatia unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū. Kwanza, Kigīchūgū ni lugha ambishi kwani huchukua viambishi awali na tamati. Hata hivyo, utafiti huu uliegemea katika upachikaji wa viambishi tamati katika vitenzi. Uchopekaji wa viambishi tamati ulisababisha kuongezeka kwa maana katika vitenzi vya Kigīchūgū. Utafiti huu aidha ulibaini kuwepo kwa kauli sita za unyambulishaji katika Kigīchūgū. Kauli hizi ni pamoja na; kauli ya Kutendea, Kutendwa, Kutendesha, Kutendana, Kutendeka na Kutendua. Kauli hizi katika Kigīchūgū hukubali mifuatano ya vinyambulishi viwili, vitatu na vinne isipokuwa kauli ya Kutendeka inayochukua mofimu nyambulishi mbili tu.

## **6.3 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye**

Kutokana na upeo wa utafiti huu, utafiti wa baadaye unaweza kushughulikia mambo yafuatayo:

- i. Katika dhana ya uambikaji, kuna aina mbili za uambikaji; uambishaji na unyambulishaji wa vitenzi. Kwa vile utafiti huu umeshughulikia unyambulishaji wa vitenzi katika Kigīchūgū, utafiti wa baadaye unaweza kufanywa ili kueleza jinsi dhana ya uambishaji inavyojitokeza katika Kigīchūgū.
- ii. Utafiti wa baadaye unaweza kufanywa katika viwango vingine vya kiisimu kama vile, Sintaksia, Semantiki, Pragmatiki na Uchanganuzi wa Usemi katika Kigīchūgū.
- iii. Utafiti wa baadaye unaweza kufanywa ili kupambanua mifanyiko ya utoni.

## MAREJELEO

- Asiimwe, C. (2011). *Unyambulishaji wa Vitenzi katika Lugha ya Runyankole. Tasnifu ya Uzamili.* (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Baker, M. (1985). The Mirror Principle and the Morpho-Syntactic Explanations. *Linguistic Inquiry* 16.3:373-415
- Buberwa, A. (2014). *Ruwaza za Kimofolojia za Majina ya Mahali ya Kihaya: Mtazamo wa Mofolojia Leksika katika Massamba, D.P.B na Bakize, L.H (wah).* *Kiswahili*, 77, (uk 41-61). Taasisi ya Taaluma za Kiswahili: Dar es Salaam.
- Charwi, Z. M. (2013). *Unyambulishaji na Dhana ya Uelekezi katika Lugha ya Kikuria, katika Omari, S na Peterson, R (wah).* *Kioo cha Lugha*, 11, (uk 58-77). Taasisi ya Taaluma za Kiswahili: Dar es Salaam.
- Chiumbo, M. (2016). An analysis of Verbal Extensions in Malawian Tonga: Towads Mirror Principle and Templatice morphology. Eduardo Mondlane University. Maputo, Mozambique.
- Chomsky, N. (1957). *Syntactic Structure*. The Hague: Muonton
- Chomsky, N. (1988). *Knowledge of Language, Its nature, Origin and age*. New York: Praeger.
- Gatumu, D.W. (2014). Morphosyntactic Verb Inflections for Tense and Aspect in Kimbeere. (Unpublished M.A Dissertation). University of Nairobi.
- Gawasike, A. (2012). Dhana ya Uambikaji katika Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (haijachapishwa)
- Gichuru, T.M. (2010). Uchanganuzi wa Nomino Ambatani za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Gicheru, D. K. (1999). Ulinganisho wa Muundo wa Kikundi Nomino cha Kiswahili Sanifu na wa cha Kikuyu cha Kabete.Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Nairobi. (haijachapishwa)
- Gitonga, J. (2014). Upatanishi katika sentensi ya Kichuka.tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Chuka. (haijachapishwa)
- Good, J. (2005). Reconstructing Morpheme Order in Bantu. The Case of Causativization and Applicativization. *Diachronica* 22: 3-57.
- Guthrie, M. (1967). *Classification of the Bantu Languages*. London: Pall Mall
- Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

- Hartman, R. (1972). *Dictionary of Language and Linguistics*. London: Applied Science Publishers.
- Heine, B. na Mohlig, W.J.G.(ed) (1980). *Language and Dialect Atlas of Kenya*. Berlin: Dietrich Reimer Verlag.
- Hyman, L. M. (2003). Suffix ordering in Bantu: A morphocentric approach. In Booij, Geert & Marle, Jaap Van (eds). *Year of Morphology* (pp 245-281). Dordrecht: Kluwer.
- Jepkoech, N.S. (2018). The Morphosyntax of the Keiyo Verb. (Unpublished M.A Thesis). Moi University
- Kamau, T, G. (1996). The Major Phonological Processes of Kindia and Kigichugu Dialects of Gikuyu: A Comparative Study. (Unpublished M.A Thesis). Kenyatta University.
- Karuru, D.W. (2012). Phonological and Morphological adaptation of loanwords in Gĩ-Gĩchūgū: An application of Source Similarity Model. (Unpublished M.A Dissertation). University of Nairobi.
- Katamba, F., & Stonham, J. (1993). *Morphology*. London: The Macmillan Press Ltd.
- Khamisi, A.M. (2008). *Maendeleo ya Uhusika*. Dar es salaam: TUKI.
- Kiango, J.G. (2008). Sarufi ya Vinyambuo Vitenzi vya Kiswahili: Mitazamo Mbalimbali kuhusu Kanuni za Unyambuaji, katika Ogechi, O.N. Shitemi, L.N. na Simala, K.I. (wah). *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Eldoret: Moi University Press.
- Kihore, Y.M., Massamba, D.P.B na Msanjila Y.P. (2012). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA) Sekondari na Vyuo*. Dar es salaam: TUKI.
- Kiparsky, P. (1982). From Cyclic Phonology to Lexical Phonology. In Ver der Hulst and Smith (ed) *The Structure of Phonological Representation*. Dordrecht: Foris Publications.
- Lyons, J. (1968). *An Introduction to Theoretical Linguistics*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Maringah, E. (1987). Muundo wa kitenzi cha Kimbeere. Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Egerton.
- Massamba, D.P.B., Kihore, Y.M., & Msanjila, Y.P. (2003). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (fokisa)*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mbaka, N.K. (2015). The Morpho-Syntax of Causative Constructions in Gichuka. M.A Thesis (Unpublished). Chuka University.

- Mbwillow, S.N. (2017). Uambikaji kama Dhana Kuu: Tofauti ya Uambikaji na Unyambulishaji. Inapatikana katika www.academia.edu. Ilipakuliwa Julai, 30 2019.
- Mgalla, R. S. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Milroy, L. (1987). *Language and Social Network*. Oxford: Blackwell.
- Munene, A. S. (2011). Uanishaji wa Mofimu za Kisarufi katika Kitenzi cha Kichuka. Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Chuka.
- Mutahi, K. E. (1983). *Sound Change and Classification of Mt. Kenya Dialects*. Berlin: Dietrich Reimes.
- Mwihaki, A. N. (1998). Loan Words and Nativization: A Generative View of the Phonological Adaptation of Gikuyu Loan Words. (Unpublished M.A Thesis). Kenyatta University.
- Mwita, L. C. (2014). Najivunia kuwa Mkenya: Utosarufi, Mtindo au Mabadiliko ya Lugha? Katika Simala, I, Chacha, L na Osore, M. (wah). *Miaka Hamsini ya Kiswahili Nchini Kenya* (uk 179-187). Nairobi: Twaweza communications.
- Ngamau, A. W. N. (2004). A morpho- syntactic analysis of Agreement in Gikuyu in the Minimalist Program. (Unpublished M.A Thesis). University of Nairobi.
- Ngowa, N. J. (2008). Mnyambuliko wa Vitenzi vya Kigryama. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (haijachapishwa)
- Njoroge, D. (1978). Kikuyu Deverbatives and other Nominalizations. (Unpublished M.A Thesis). University of Nairobi.
- Njuguna, M. W. (1992). Mofofonolojia ya Kiswahili sanifu na Kikuyu sanifu; Mathalani Kikikuyu cha Kabete: Ulinganishi. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (haijachapishwa)
- Nurse, D., & Philippson, G. (eds.) (2003). *The Bantu Languages*. London: Routledge.
- Oichoe, M. P. (2005). Ulinganishi wa Kirai Tenzi cha Kiswahili na Ekegusii Kimofosintaksia: Mtazamo wa Uminimalisti. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (haijachapishwa)
- Ruri, M. N. (2011). Konsonanti katika Lahaja ya Kindia. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Chuka. (haijachapishwa)
- Schadeberg, T. C. (2003). Derivation, in Nurse,D and Philippson G.(eds.), *The Bantu Languages* (pp 71-86). London: Routledge.
- TUKI. (1990). *Kamusি Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es saalam: TUKI

Wachera, S.K. (2008). Tone as a distinctive feature in the lexion of Gĩ-Gĩchūgũ dialect, Gĩkũyũ Language. (Unpublished M.A Dissertation). University of Nairobi.

Waihiga, G. (1999). *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Waithaka, N. M. (2009). Utohozi Mofolojia wa Maneno Mkopo ya Gikuyu kutoka Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta (haijachapishwa)

Waweru, N. M. (2011). Gikuyu Verbal Extensions: A Minimalist Analysis. (Unpublished PhD Thesis). Kenyatta University.

Wesana-Chomi, E. (2013). *Kitangulizi cha Mofolojia ya Kiswahili*.: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI

**KIAMBATISHO I**  
**TAKWIMU ZA TASNIFU**

Jumla ya maneno.....	23,358
Kurasa (zikiondolewa za mwanzo, marejeleo na viambatisho).....	87
Jumla ya vitenzi vilivyochanganuliwaa.....	60

**KIAMBATISHO II**  
**JEDWALI LA USAILI WA VITENZI VYA KIGÍCHŪGŪ**

Vitenzi/kauli	tendea	tendeka	tendwa	tendana	tendesha	tendua
<b>thaka</b>	thakīra	thakīka	thakwa	-	thakithia	-
<b>rima</b>	rīmīra	rīmīka	rīmwa	-	rīmithia	rīmūria
<b>thika</b>	thikīra	thikīka	thikwa	thikana	thikithia	thikūria

**KIAMBATISHO III**  
**MNYAMBULIKO WA VITENZI VYA KIGICHUGU**

	Kitenzi	Maana	Kauli za unyambulishaji wa vitenzi					
			Tendea	tendwa	tendesha	tendana	tendeka	tendua
1	aka	jenga	akīra	akwa	akithia	-	akīka	akūra
2	andīka	andika	andīkīra	andīkwa	andīkithia	-	andīkīka	-
3	aria	ongea	arīria	arwa	arithia	-	arīkia	-
4	baka	paka	bakīra	bakwa	bakithia	bakana	bakīka	-
5	bata	kwama	batīra	batwa	batithia	-	batīka	batūra
6	binga	funga	bingīra	bingwa	bingithia	bingana	bingīka	bingūra
7	boya	omba	boera	bowa	boithia	-	boeka	-
8	bura	panguza	burīra	burwa	burithia	burana	burīka	-
9	būra	chapa	būrīra	būrwa	būrithia	būrana	būrika	-
10	buta	futa	butira	butwa	butithia	butana	butika	-
11	ceera	tembea	ceerera	ceerwa	ceerithia	-	ceereka	-
12	cooka	rudi	cookera	cookwa	cookithia	-	cookeka	-
13	cora	chora	coreka	corwa	corithia	corana	coreka	-
14	enda	penda	endera	endwa	endithia	endana	endeka	-
15	giria	pangusa	girīria	girua	girithia	girania	girīkia	-
16	gūra	nunua	gūrīra	gūrwa	gūrithia	-	gūrīka	-
17	ina	imba	inīra	inwa	inithia	-	inīka	-
18	inama	inama	inamīra	inamwa	inamithia	-	inamīka	-
19	kena	furahi	kenera	-	kenithia	-	-	-
20	kethia	salimu	ketheria	kethua	kethithia	-	ketheka	-
21	koma	lala	komera	komwa	komithia	-	komeka	-
22	kūnja	kunja	kūnjīra	kūnjwa	kūnjithia	kūnjana	kūnjīka	kūnjūra
23	kuua	beba	kuīra	kuuwa	kuithia	kuana	kuīka	-
24	mena	chukia	menera	menwa	menithia	menana	meneka	-
25	menya	fahamu	menyera	menywa	menyithia	menyana	menyeka	-
26	munda	dunga	mundīra	mundwa	mundithia	mundana	mundika	-
27	nora	nenepa	norera	norwa	noria	-	noreka	-
28	nyita	shika	nyitīra	nyitwa	nyitithia	nyitana	nyitīka	-
29	nyua	kunywa	nyuīra	nyuwa	nyuthia	-	nyuīka	-
30	oba	funga	obera	obwa	obithia	obana	obeka	obora
31	oca	chukua	ocera	ocwa	ocithia	-	oceka	-
32	rathima	bariki	rathimīra	rathimwa	rathimithia	rathimana	rathimīka	-
33	rība	lipa	rībīra	rībwa	rībithia	rībana	rībīka	-
34	rīma	lima	rīmīra	rīmwa	rīmithia	-	rīmīka	-
35	rīra	lia	rīrīra	rīrwa	rīrithia	-	rīrīka	-

36	roga	roga	rogera	rogwa	rogithia	rogana	rogeka	rogora
37	ruga	pika	rugīra	rugīrwa	rugithia	-	rugīka	-
38	rūga	ruka	rūgīra	rūgwa	rūgithia	rūgana	rūgīka	-
39	rūgama	simama	rūgamīra	rūgamwa	rūgamia	rūgamana	rūgamīka	-
40	ruma	tusi	rumīra	rumwa	rumithia	rumana	rumīka	-
41	rūnga	lainisha	rūngīra	rūngwa	rūngithia	rūngana	rūngīka	-
42	rwara	ugua	rwaria	rwarwa	rwaria	-	rwarika	-
43	taara	chagua	taarīra	taarwa	taarithia	-	taarīka	-
44	tema	kata	temera	temwa	temithia	temana	temeka	-
45	teta	teta	tetera	tetua	tetithia	-	teteka	-
46	thaka	cheza	thakīra	thakwa	thakithia	-	thakīka	-
47	thama	hama	thamīra	thamwa	thamithia	-	thamīka	-
48	thambia	osha	thambīria	thambua	thambithia	-	thambīkia	-
49	tharia	bomoa	tharīria	tharua	tharithia	-	tharīka	-
50	theka	cheka	thekera	thekwa	thekia	thekana	thekeka	-
51	thika	zika	thikīra	thikwa	thikithia	thikana	thikīka	thikūria
52	thoma	soma	thomera	thomwa	thomithia	thomana	thomeka	-
53	thūa	kuna	thūīra	thūwa	thūithia	thūana	thūīka	-
54	tiga	acha	tigīra	tigwa	tigithia	tigana	tigīka	-
55	tinia	kata	tinīria	tinua	tinithia	tinana	tinīka	-
56	tongoria	ongoza	tongoreria	tongorua	tongorithia	-	tongorekia	-
57	tuma	shona	tumīra	tumwa	tumithia	-	tumīka	tumūra
58	tware	peleka	twarīra	twarwa	twarithia	twarana	twarīka	-
59	uga	sema	ugīra	ugwa	ugithia	ugana	ugīka	-
60	una	vunja	unīra	unwa	unithia	-	unīka	-

**KIAMBATISHO IV  
BARUA YA IDHINI YA UTAFITI**



**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,  
TECHNOLOGY AND INNOVATION**

Telephone: +254-20-2213471,  
2241349, 3310571, 2219420  
Fax: +254-20-318245, 318249  
Email: dg@nacosti.go.ke  
Website: www.nacosti.go.ke  
When replying please quote

NACOSTI, Upper Kabete  
Off Waiyaki Way  
P.O. Box 30623-00100  
NAIROBI-KENYA

Ref. No. **NACOSTI/P/19/77319/28736**

Date: **2<sup>nd</sup> April 2019**

Magdalene Wangu Gituru  
Chuka University,  
P.O. Box 109-60400,  
**CHUKA.**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on “*Unyambulishaji wa vitenzi katika Kigichugu*” I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Kirinyaga County** for the period ending **1<sup>st</sup> April, 2020**.

You are advised to report to **the County Commissioner and the County Director of Education, Kirinyaga County** before embarking on the research project.

Kindly note that, as an applicant who has been licensed under the Science, Technology and Innovation Act, 2013 to conduct research in Kenya, you shall deposit **a copy** of the final research report to the Commission within **one year** of completion. The soft copy of the same should be submitted through the Online Research Information System.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read "Boniface Wanyama".  
**BONIFACE WANYAMA**  
FOR: DIRECTOR-GENERAL/CEO

Copy to:

The County Commissioner  
Kirinyaga County.

The County Director of Education  
Kirinyaga County.

*National Commission for Science Technology and Innovation is ISO9001: 2008 Certified*

## **KIAMBATISHO V KIBALI CHA UTAFITI**

<p><b>THIS IS TO CERTIFY THAT:</b></p> <p><b>MS. MAGDALENE WANGU GITURU</b> of CHUKA UNIVERSITY, 0-10300 KERUGOYA, has been permitted to conduct research in Kirinyaga County</p> <p><b>on the topic: UNYAMBULISHAJI WA VITENZI KATIKA KIGICHUGU</b></p> <p><b>for the period ending:</b> <b>1st April,2020</b></p> <p><b>Applicant's Signature</b></p>	<p><b>Permit No : NACOSTI/P/19/77319/28736</b></p> <p><b>Date Of Issue : 2nd April,2019</b></p> <p><b>Fee Received : Ksh 1000</b></p>  <p><b>Director General</b> <b>National Commission for Science, Technology &amp; Innovation</b></p>
---	---



National Commission for Science  
Technology & Innovation

# **KIAMBATISHO VI**

## **RAMANI YA KAUNTI YA KIRINYAGA IKIONYESHA ENEO LA UTAFITI**

